Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Tano – Tarehe 19 APRILI, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano huu wa kumi na tisa niliwatangazia kwamba Miswada sita ya sheria kati ya ile minane iliyopitishwa na Bunge katika mkutano wa kumi na nane ilikuwa imepata kibali cha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Nafurahi tena kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha Muswada wa Sheria uitwao *The Electronic and Postal of Communications Bill*, 2009 na sasa Muswada huo ni sheria na inaitwa *The Electronic and Postal Communications Act, 2010* Na. 3 ya Mwaka 2010. *(Makofi)*

Muswada wa *Electoral Laws* bado upo kule Ikulu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 52

### Mikakati ya Kilimo Kwanza Kuwasilishwa Bungeni

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kukipa kilimo kipaumbele kwa kuanzisha kaulimbiu ya “Kilimo Kwanza”.

Je, Serikali itakuwa tayari kushirikiana na Bunge kwa kuwasilisha mikakati yake Bungeni kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kujadili na kuboreshwa?

**WAZIRI NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, ningependa kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais wakati akizindua Kilimo Kwanza mnamo tarehe 3 Agosti, 2009, Kilimo Kwanza ni azma maalum ya kitaifa ya kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini.

Utekelezaji wa Kilimo Kwanza unahusu sekta ya Umma na binafsi na unajumuisha sera na mikakati mbalimbali zinazolenga kutatua kwa haraka vikwazo mbalimbali vya kilimo hapa nchini. Kwa kuzingatia hali hii Kilimo Kwanza, kinaweka mfumo wa utekelezaji wa nguzo kumi zifuatavyo:-

(i) Dira ya Taifa ya Kilimo Kwanza;

(ii) Kugharamia Kilimo Kwanza;

(iii) Muundo mpya wa taasisi kwa ajili ya usimamizi wa Kilimo Kwanza;

(iv) Mabadiliko ya mfumo wa Kimkakati wa Kilimo Kwanza;

(v) Ardhi kwa ajili ya Kilimo Kwanza;

(vi) Vivutio kwa ajili ya Kilimo Kwanza;

(vii) Viwanda kwa ajili ya Kilimo Kwanza;

(viii) Sayansi, teknolojia na rasilimali watu kwa ajili ya Kilimo Kwanza;

(ix) Miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza; na

(x) Uhamasishaji wa Watanzania kwa ajili ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, kama ifuatavyo:-

Kwa kuzingatia kuwa nguzo kumi za kilimo kwanza zinahusu sekta zote, Wizara na Idara zote zimeagizwa kuzingatia utekelezaji wake katika sera, mikakati na Bajeti zao, ambazo kama ilivyokawaida zitawasilishwa na kujadiliwa na Bunge wakati wa mkutano wa Bunge wa kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali.

Aidha, Serikali itakuwa inatoa taarifa za utekelezaji kwa Waheshimiwa Wabunge kila *quarter*, ili waweze kufuatilia na kutathimini utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii basi kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge wote washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa kilimo kwanza katika Majimbo yao ya Uchaguzi. Mojawapo ya nguzo ya Kilimo Kwanza ni kuhamasisha Watanzania waelewe Kilimo Kwanza. Waheshimiwa Wabunge wanayofursa nzuri sana ya kufanya kazi hii kikamilifu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa umilikishwaji wa ardhi na mikopo ya dhana za kilimo ambayo ni nyenzo muhimu katika kuinua kilimo imekuwa na urasimu mkubwa sana. Je, sasa Serikali iko katika mikakati gani kurahisisha mambo haya ili wakulima ama wananchi kwa ujumla waweze kufaidika na dhana hii na suala hili la kilimo kwanza?

**WAZIRI NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa upande wa kumilikisha ardhi kwa upande wa Tanzania hasa wa vijijini kuna tatizo la uwekezaji wa nje utaratibu mzuri tu unafanywa na kituo chetu cha uwekezaji na kwa upande mikopo ikumbukwe kwamba sasa hivi tunapoongea benki ya rasilimali yaani ya TIB imeshafungua rasmi dirisha la mikopo kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Na. 53

**Kuboresha Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo ni chuo pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipanua Chuo hiki ili kiwe cha Kimataifa kwa kutoa vyeti, Stashahada na hata shahada kamili?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu kwa chuo hicho kutoa kozi zote zinazowahusu Madiwani, watendaji wa ngazi zote wa Halmashauri za Wilaya kupitia fedha zinazotolewa kwa ajili ya kujenga uwezo kuliko kila wilaya kuendesha kozi zake yenyewe?

(c) Je, Serikali haioni ni muhimu watendaji wote wakuu wanaojiriwa kama wakurugenzi, Maafisa mipango, na kadhalika, wapate mafunzo ya kazi kupitia hapo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo ni Chuo pekee kinachotoa mafunzo ya Serikali za Mitaa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Kwa kutambua hilo, tayari Serikali inayo mipango ya kukipanua Chuo cha Serikali za Mitaa ili kiwe cha Kimataifa kwa kutoa Elimu ngazi ya cheti, Stashahada na Shahada. Katika kufikia azma hii, Serikali imeanza na ujenzi wa Miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha wa 2008/2009 na 2009/2010, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 2,300,000,000 ili kujenga bweni lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 200, ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 400 na bohari yenye ofisi 6 za watumishi. Ujenzi huu unafanywa na mkandarasi kutoka China ajulikane kama M/s *Hainan International Limited.* Utekelezaji wa Miradi hii umefikia asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, mbali na mradi hiyo inayotekelezwa kupitia Bajeti ya kawaida ya Serikali, Chuo pia kimeanza utekelezaji wa miradi inayopata fedha kutoka mfuko wa pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) kwa udhamini wa Serikali kwa gharama ya shilingi Bilioni 39.8. ambazo ni gharama za mshauri, malipo kwa wakandarasi pamoja na gharama zingine za kiutawala.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni pamoja na mabweni yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 200, maktaba yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 300, mgahawa wanafunzi wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 300, nyumba za watumishi 15, viwanja vya michezo, barabara za ndani, mabwawa ya maji machafu, miundombinu ya umeme na maji pia sehemu ya kuegesha magari.

Sanjari na ujenzi wa miundombinu, chuo kinaandaa kozi mpya katika ngazi ya cheti, stashahada za shahada. Vilevile, kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kuongeza idadi ya walimu.

(b) Mheshimiwa Spika, chuo kitakapokuwa kimekamilisha ujenzi wa miundombinu, kikatoa kozi zote zinazohusu Madiwani, watendaji wa ngazi zote wa Halmashauri na hivyo kupunguza gharama zinazotokana na kila Halmashauri kuendesha kozi zake yenyewe. Aidha, Halmashauri za wilaya kupitia Wakurugenzi wake

zinatakiwa kubaini mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wake wakiwemo Madiwani na Watendaji wote na kuwaingiza katika mpango wa Bajeti kupitia kasma ya kujenga uwezo (*Capacity Building)* na kuyawasilisha katika chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo ambapo kinaweza kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo hayo kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika kazi.

(c)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo kitoe mafunzo ya kazi kwa watumishi wa ngazi zote katika Mamlaka za Serikali za mitaa wanapoajiriwa. Hata hivyo, jitihada zinazoendelea kuimarisha miundombinu ya chuo hivi sasa zitaongeza uwezo wa chuo kutoa mafunzo kwa watendaji wa Serikali ili kuwaongezea ufanisi katika kazi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba chuo hiki cha Serikali za Mitaa Hombolo vile vile kitatoa mafunzo kwa ajili ya madiwani wetu. Je, sasa atakubaliana na mimi kwamba baada ya Uchaguzi tu madiwani hawa wapewe mafunzo ili kupunguza migongano na kujua mipaka yao badala ya kusubiri muda mrefu wanakaribia kumalizia muda ndiyo mafunzo yanatolewa?

Kwa kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya utendeshaji wa chuo hiki ni kidogo na mwaka jana Kamati yangu ilifanya kazi ya kuchambua Bajeti hii. Je, kwa Bajeti ya 2010/2011 Serikali imeliangalia hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa haya mafunzo yanatolewa na Mheshimiwa Lubeleje anapendekeza hapa kwamba mara tutakapokuwa tumemaliza uchaguzi Madiwani waweze kupata fursa ya kwenda kwa ajili ya kupata mafunzo katika chuo hiki. Nimeeleza hapa kwamba chuo hiki kimeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia Madiwani pamoja na watendaji wengine wa Halmashauri.

Mimi sioni tatizo lolote kama Halmashauri zenyewe zitakuwa zimeonyesha *interest* katika jambo hili. Ninachosema hapa ni kwamba mlango uko wazi hii itakuwa ni sehemu ya Bajeti yao na nimesema Bajeti wanayoweza kutumia hapa ni ya Capacity *Building* na tuko tayari sisi kuwapokea na kwa kweli tutaandaa utaratibu mzuri ili Madiwani wetu waweze kupata mafunzo katika chuo hiki ndiyo maana kimeundwa kimetengenezwa kwa ajili ya kazi hiyo.

La pili anazungumzia kuhusu suala la kuangalia Bajeti, Bajeti ni utaratibu unaokuonyesha jinsi hela zitakavyopatikana na zitakavyopatikana na hapa kama kutakuwa na *sealing* tutafuata *sealing* ya Serikali hatuwezi kwenda nje ya hapo. Matumaini yangu ni kwamba huu utaratibu tuliozungumza wa *Local Authorities Provident Fund* ambao unaingia katika mkataba na Serikali na Serikali inadhamini huu utakuwa umesaidia zaidi kwa sababu tumezungumza habari ya bilioni 39.2 ndiyo maana

tunasema kwamba kazi inafanyika kule. Nataka nikuambie leo hivi tunavyozungumza hapa ninaondoka na Mheshimiwa Lubeleje pamoja na Kamati yake ya Utawala na Sheria kwa ajili ya kwenda kujua mambo yanayoendelea katika chuo kile. Na haya yote anayouliza hapa maswali haya atakwenda kupata majibu pale saa sita kamili basi litakuwa tayari tunaondoka naye tunakwenda mpaka Hombolo ili kwenda kuangalia mambo yanayofanyika pale. *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge taarifa hiyo ni ya kweli kabisa nilitoa idhini kwa Kamati iende Hombolo leo.

Na. 54

**Vyombo vya Habari Kuandaliwa kwa Uchaguzi Mkuu wa 2010**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka huu wa 2010 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu hapa Tanzania ambapo huwa kunatokea vitendo vya chokochoko na kupakana matope kupitia vyombo vya habari.

(a) Je, vyombo vyetu vya habari nchini vimeandaliwa vipi kimafunzo juu vya sheria mpya za Uchaguzi ili haki kitendeke kwa watu wote?

(b) Je, hadi hivi sasa hapa nchini kuna vituo vya Radio vingapi, magazeti ya aina ngapi na vituo vingapi vya televisheni?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake iliyopewa kisheria, katika nyakati tofauti huwa inakutana na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari ili kutoa taarifa muhimu zinazohusu mchakato wa Uchaguzi. *(Makofi)*

Katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2010, Tume hiyo tayari imekwishakutana na vyombo vya habari mwezi Desemba mwaka jana na kuvipatia taarifa juu ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na maandalizi ya Uchaguzi huo.

Aidha, Tume hiyo pia imepanga kukutana tena na vyombo vya habari kwa mashauriano na kupeana taarifa za maandalizi ya uchaguzi na sheria mpya za uchaguzi. Utoaji taarifa kwa vyombo vya habari kuhusiana na mchakato wa uchaguzi utakuwa

unaendelea kadri taarifa hizo zinapopatikana tukiamini kwamba, vyombo hivyo ni njia pekee ya kuwafikishia ujumbe wananchi kwa haraka na maeneo mengi zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa kuna vituo 58 vya *Radio,* na 28 vya televisheni. Kati ya hivyo, vipo vinavyomilikiwa na Serikali, watu binafsi, vyama vya Siasa, dini na taasisi mbalimbali. Kwa upande wa magazeti yapo ya aina mbalimbali kama vile yanayoandika habari za kiuchumi, siasa, dini, mazingira, afya, michezo na kadhalika. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ingawje kasi ya kutoa elimu kwa waandishi wa habari bado sijaridhika ni ndogo sana.

Gazeti moja lilitoa taarifa na picha ya viongozi wawili wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na kuandika mbele ya gazeti lenyewe ya kwamba wanawasubiri wananchi katika majimbo yao ili waende wakawaage. Sasa hili suala hatulioni kama ni sehemu ya kampeni ambayo inaanza kuchafua baadhi ya viongozi tuliokuwa nao hapa? (*Makofi*)

Kwa kuwa, jukumu la Mbunge yeyote ni kutekeleza ahadi na ilani ya Uchaguzi mpaka tarehe Bunge litakapofungwa. Je, kwanini mtindo umeanza wakati wa Bunge wanatekeleza majukumu yao katika maeneo yao wanaonekana wanatoa rushwa katika maeneo hayo? (*Makofi*)

Je, isingekuwa vizuri ofisi inayohusika ikatoa maelekezo sahihi ili tukapunguza kesi ambayo zinaweza kujitokeza kabla na baada ya Uchaguzi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu maswali ya nyongeza ya kaka yangu Paul Peter Kimiti, kama ifuatavyo:-

Kuhusu gazeti ambalo limetoa taarifa kwamba wanawasubiri wakawaage majimboni kwao ni kwamba je, hii si kampeni?

Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 inaruhusu Mtanzania yeyote ambaye ameona hakutendewa haki kulalamika kwa Waziri mwenye dhamana ya habari kwamba sikutendewa haki.

Kwa hiyo, wale ambao wameathirika na taarifa zile za kwenye gazeti wanashauriwa na hawajachelewa au walipaswa wakati ule kulalamika kwa Waziri wa Habari kwamba habari zilizoandikwa zimenichafua katika Jimbo langu na kama mnavyofahamu Waziri wa Habari akipata habari kama hizo huchukua hatua. *(Makofi)*

La pili, kwa nini Mheshimiwa Mbunge katika maeneo yake wanapoonekana wanatoa misaada wanaandikwa kwamba wametoa rushwa, ninavyofahamu mimi Mbunge

aliyepo madarakani na Diwani aliyepo madarakani ni ruksa kusaidia watu wake kwa kadri ya uwezo wake mpaka tarehe ya siku Bunge linapovunjwa. (*Makofi*)

Mimi ni Mbunge kama ninyi na mnafahamu hata mkifanya ziara katika maeneo yenu mnaandikiwa barua mbalimbali za kuombwa misaada, sasa Mbunge makini hawezi akaombwa msaada na wapiga kura wake akakaa kimya. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri naomba kuongezea majibu kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria mliyotunga Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 21(3) cha Sheria ya gharama za uchaguzi, kinasema:-

*"For the purposes of this section an act or transaction shall not be deemed to constitute prohibited practice if it is proved to have been designed to advance the interest of the community fund raising self help, self reliance or social welfare projects within the constituency and to have been done, this is important, to have been before the nomination process or election campaign as the case may be. " (Applauses)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili tayari liko kwenye Sheria na Sheria inawalinda watu hawa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la upendeleo Mheshimiwa Savelina S. Mwijage. Kwanza nguo hiyo uliyovaa kwa kweli imekukaa vizuri sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninakushukuru sana, na nimevaa kwa makusudi mazima na anayeuliza swali ndiye mwenyewe! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kipindi cha Uchaguzi wanaopata matatizo makubwa sana na wasiojua Sheria ni watu wa vijijini yaani Wapiga Kura wale waliopo vijijini na ndiyo wanapata shida na vyombo vya habari kwa mfano magazeti na televisheni havifiki mara kwa mara, wananyanyasika kweli hasa upande wa Kambi ya Upinzani. Je, Serikali inawasaidiaje?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, kama ifuatavyo:-

Nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli kwamba katika ile Waingereza wanasema *access to information* yaani kupata taarifa, waliopo vijijini Wanawake na wanaume hawana fursa ya kupata habari kama walivyo watu wa mjini ambako kuna umeme na televishen na kadhalika. Sasa yale niliyoeleza ni yale tu yanayoweza kufanywa na upande wa Serikali kwamba Serikali inawasaidiaje nafikiri wakati wa uchaguzi kuna vipindi mbalimbali katika redio ya Serikali ambayo inaelezea masuala ya uchaguzi.

Sasa mahali ambapo watu wote tunafika kwa urahisi ni vyama vya siasa kwa hiyo ninaomba ili kuhakikisha ujumbe huu unawafikia wananchi wote wenye itikadi zote, naomba vyama vyote vya siasa tushirikiane kuwaelimisha Wanachama wetu na washabiki wetu kuhusu masuala haya. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, imedhihirika waziwazi kwamba kuna mchezo mchafu ambao unafanywa hasa dhidi yangu na wahariri wa magazeti yafuatayo Rai, Tazama Tanzania na Mkakati, nilikuwa namsubiri Mheshimiwa Waziri aje hapa ili tuanze kazi. Kwa hiyo, nipatie nafasi ili tuweze kushughulikia suala hilo. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa kuna Rai kwako sasa sijui utasemaje!

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William Hezekiah Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Nilipojibu maswali ya awali nilieleza kwamba Sheria ya magazeti ya mwaka 1976 inamruhusu mwananchi yeyote ambaye ameona hakutendewa haki yaani amekuwa *offended* na chombo chochote kile cha habari kupeleka malalamiko yake kwa Waziri mwenye dhamana ya Habari. Wiki yote tupo hapa kwa hiyo namhakikishia Kaka yangu Shellukindo kwamba kipindi tukiwa hapa yale mambo yake ayaweke sawa tuyapate na Serikali itayafanyia kazi kwa mujibu wa Sheria za nchi. (*Makofi*)

Na. 55

**Fedha Zinazotumika Kuagiza Samani Nje ya Nchi**

**MHE. GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutoa Bungeni takwimu zinazoonyesha kiasi cha fedha zinazotumika kuagiza samani (*furniture*) zitokanazo na mbao ama mbao bandia nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu swali namba 4920 la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge lako Tukufu ya kwamba Serikali haiagizi moja kwa moja samani kutoka nje ya nchi, kinachofanyika huwa ni kutangaza zabuni kwa kutumia Sheria ya Manunuzi Namba 21 ya mwaka 2009 ambapo makampuni yanayoomba huteuliwa na Wizara kwa ajili ya kuleta samani hizo kwa ajili ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 Serikali ilitumia kiasi shilingi 5,207,390,750.50 kwa ajili ya ununuzi wa samani za Ofisi na majumbani zilizonunuliwa kwenye maduka yanayouza samani hizo. Kati ya samani hizo zilizonunuliwa zimo samani zinazotokana na mbao bandia toka nchi za nje.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu haya mafupi yanayoeleweka lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi tuna *export* mbao kwa sababu tunazo mbao za kutosha na tunafanya hivyo tukijua kabisa kwamba tunatoa kitu chenye thamani na baadaye tunakuja kununua fanicha hizo kwa bei kubwa sana kuliko thamani ya mbao tunazopeleka.

Je, Serikali haioni haja kwamba kuna haja sasa ya kushawishi hawa wanapenda kununua mbao zetu yaani wawekezaji wa ndani na nje wakawekeza viwanda hivyo hapa Tanzania ili na sisi tuka *export furniture* badala ya ku-*export raw materials* ya mbao?

Kwa kuwa, hata vijiti vile vya kuchokonolea meno tu sasa vinatoka nje na kwa kuwa tunavyo viwanda vidogovidogo vya wajasiriamali wadogowadogo ambao wangeweza kufanya kazi nyingine ambazo kwa kweli kwa hakika kwa uwezo na kwa hali ya uchumi wa nchi yetu tunaweza kwa hawa wajasiliamali wadogowadogo.

Je, Serikali haioni sasa kwamba kuna haja ya kuzuia hizo *furniture* zinazokuwa *imported* ili zitengenezwe na Watanzania kwa mfano vitanda vya Watanzania ndiyo vikauzwa visionekane vitanda vingine huko kwenye maduka yanayouza *furniture*?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George B. Simbachawene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu wauzaji wa bidhaa hizi za nje wawekeze humu ndani ya nchi, wazo hilo tumelipokea tutaendelea kulifanyia kazi na kulisisitiza kwamba lifanikiwe na kwamba tayari sasa hivi Serikali katika njia hiyo imejaribu kuchukua hatua mbalimbali kama vile ambavyo Mheshimiwa Dr. Chami alivyozitaja wakati akijibu swali namba 48 la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, kuhusu fenicha hizi hizi za nje.

Alielezea kwamba katika mikakati ya Serikali ni pamoja na kuasisi *TANTRADE Development Authority* ambayo itasimamia na kuhamasisha utengenezaji wa samani humu ndani na sisi tutumie samani zetu wenyewe.

Lakini pia Wizara ya Miundombinu imeanza kuandaa *specifications* kwa ajili ya samani ambazo zitatumika na ofisi za Serikali ya nyumba za Serikali na hii itachukuliwa umuhimu sana samani zile ambazo zinatokana na mbao zetu wenyewe humuhumu ndani na kutoa nafasi nzuri kwa ajili kampuni zetu za ndani kama vile Magereza, JKT na *SIDO* ziweze kuuzia Serikali samani.

Kwa hiyo, tutachukua hatua pamoja na hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameipendekeza lakini pia tayari mchakato wa Serikali umeanza ili tu-*focus* katika kutumia samani zinazotokana na mbao zetu wenyewe humu ndani. Kuhusu swali la pili la Serikali kuzuia samani kutoka nchi za nje tutafanya hivyo mara tu tutakapokuwa tumejihakikishia kwamba tuna samani za kutosha kutoka hapa hapa nchini.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda nimwulize swali moja la nyongeza.

Je, Waziri anaelewa kwamba fanicha zote zinazoagizwa pamoja na kwamba Serikali haiagizi moja kwa moja lakini pesa zinazolipwa huko China, Malaysia na kadhalika ni pesa za kigeni ambazo tungeweza tukaagiza mali nyingine nyeti kama madawa na vitu vingine kwa matumizi ya wananchi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaelewa kwa kuamua kwamba fanicha zote za Serikali zitengenezwe kwenye viwanda vilivyopo hapa nchini ni kujaribu kuwapa vijana ajira na kukataza pesa kidogo tulizonazo za nje zitumike kwa matumizi mazuri ya bidhaa ambazo wananchi wanazihitaji?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, kama ifuatavyo:-

Naafiki kabisa kwamba kununua bidhaa kutoka nje ni kutumia raslimali chache ya fedha za kigeni tulizo nazo na kwamba mchakato ambao Serikali imeuanza sasa hivi kwa njia mbalimbali ambazo nimezieleza hapo awali ni pamoja na zile ambazo Mheshimiwa Dr. Chami alikuwa amezieleza ndani ya Bunge hili la kumi na tisa linalenga kabisa katika kuhakikisha kwamba ifike muda ambapo tutatumia raslimali zetu wenyewe humu nchini kutengeneza samani na kwa maana hiyo kupunguza utumizi wa pesa za nje kwa ajili ya kununua samani hizi.

Na. 56

**Kambi za Kuangalia Usalama wa Reli Kuvunjwa**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kambi ambazo zilikuwepo kwenye njia ya reli kuanzia Manyoni hadi Singida kwa ajili ya kuangalia usalama wa reli na usalama wa abiria wa treni zimevunjwa na mwekezaji kwa madai kwamba treni ya Dodoma hadi Singida haina maslahi kwake:-

Je, Serikali inasemaje juu ya usalama wa abiria wa treni zinazotumia reli hiyo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na kuundwa kwa Kampuni ya *TRL*, Kampuni hiyo haijuvunja kambi za kuangalia usalama wa reli na abiria wanaotumia njia hiyo, bali ilipunguza idadi ya wafanyakazi wanaohusika na matengenezo ya njia na kuacha wachache ambao wanaendelea kuangalia usalama wa reli. Kazi za matengenezo ya njia zilikasimiwa kwa mkandarasi. Kwa sasa kuna kambi kumi na moja (11) kila moja ikiwa na *keyman* mmoja ambaye anaangalia masuala ya usalama wa njia katika eneo alilopangiwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mkataba wa Mkandarasi aliyepewa kazi ya kutengeneza reli hiyo kutoka Manyoni hadi Singida kuanzia Agosti, 2008 ulisitishwa ilipofika Mei, 2009 kutokana na hali ngumu ya kampuni kifedha.

Mheshimiwa Spika, njia hiyo kwa sasa iko chini ya uangalizi wa Mkaguzi (*Sub Permanent Way Inspection*) mmoja aliyepo Manyoni ambaye anasaidiwa na Wasukuma Toroli (*Trolleymen*) watatu (3). Ukaguzi wa njia unaendelea kufanyika mara kwa mara, licha ya kusimamia kwa huduma za treni, hii ikiwa ni pamoja na matengenezo ya njia kila haja inapojitokeza. Serikali imekwishaiagiza Menejimenti ya *TRL* kuhakikisha kwamba usalama wa mtandao mzima wa reli unapewa umuhimu unaostahili.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa, wakati treni ilipokuwa inapita ilikuwa inakwenda mwendo mdogo sana kwa sababu mara nyingi ilikuwa inakuta mawe yamewekwa njiani na kulazimika kusimama kuondoa yale mawe pamoja na kwamba waangalizi wapo na Wasukuma toroli wapo. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kumwita Mkandarasi huyu kumpa maelekezo haya ili aweze kutimiza wajibu wake kwa watu wa Singida wanaotumia treni hiyo?

Kwa kuwa, hata treni hii ya Manyoni Singida imesimama sasa ni muda mrefu na sababu zake hatuzijui. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kueleza sababu za treni hii kuacha kutoa huduma ili wananchi wanaotegemea treni hii wafahamu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dada yangu Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwawakilisha wananchi wake wa Singida na kufuatilia kwa karibu sana masuala ya wananchi wa Singida, namshukuru sana na ninampa pongezi kwa juhudi zake hizo. (*Makofi*)

Kujibu swali lake la kwanza kuhusu mkandarasi ambaye amepewa kazi ya matengenezo kama alivyosema kwamba Mkandarasi huyo amesitishwa na sasa tuna mtu mwingine ambaye anafanya kazi hiyo. Tumepokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge tutaisimamia kikamilifu ili kuhakikisha kwamba anafanya kazi nzuri, najua kwamba kwa sababu ya mabadiliko ambayo yatatokea hivi karibuni baada ya Serikali kukubali kununua hisa za *RITES* kwamba tunajipanga upya kwa ajili ya kuiendesha Reli hiyo tutahakikisha kwamba na *branch* hii ya Manyoni hadi Singida inatoa huduma kwa njia ya ufanisi.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe na taarifa ya nyongeza kwamba kwa hivi sasa tupo njiani kuweza kukamilisha matengenezo ya reli kutoka Kilosa hadi Gulwe, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikagua miundombinu hiyo na sasa hivi tunatarajia mpaka ikifikia katikati ya mwezi ujao tutakuwa tumekamilisha urudishaji wa miundombinu. Kwa hiyo, tutajiandaa kuanza ajili ya kurudisha huduma ya reli katika reli yetu ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba lini huduma ya Manyoni hadi Singida itarudi; tutahakikisha kwamba, wakati tunarudisha miundombinu, tutaifanyia kazi huduma ya Manyoni - Singida ambayo iliacha kutolewa kwa sababu ya hali mbaya ya kifedha ya Shirika ambalo lilikuwa linatoa huduma hiyo (TRL). Kwa kuwa sasa Serikali imeamua iendeshe yenyewe kwa kipindi hiki cha mpito, basi na Manyoni - Singida nayo tutaiingiza katika programu hii.

Na. 57

**Mradi wa PASHA Juu na Mimba za Utotoni**
**Kupelekwa Mikoani**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mradi wa PASHA unaofadhiliwa na GTZ chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi umefanya kazi nzuri sana kuelimisha vijana mashuleni kuhusu athari za mimba za utotoni, maambukizi ya UKIMWI na stadi za maisha katika Mikoa ya Tanga, Lindi na Mtwara:-

Je, Serikali iko tayari sasa kupeleka Mradi huo katika Mikoa mingine yenye athari za mimba mashuleni kama vile Mkoa wa Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa PASHA unafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Mpango wa Kuboresha Afya za Watanzania *(Tanzania and German Program to Support Health – TGPSH)*, ambao upo katika Mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara na Mbeya. Mradi wa PASHA ulianza shughuli zake mwaka 2003 katika shule zote za sekondari Mkoa wa Tanga.

Mwaka 2006 Mradi ulipanua shughuli zake kuelekea Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa kuwa Mradi wa PASHA unalenga pia Mkoa wa Mbeya, hivyo awamu ya tatu ya PASHA, 2010/2013 itahusisha pia Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mradi wa PASHA katika Mkoa wa Mbeya tayari umeshakubaliwa na Serikali zote mbili. Hivi sasa mchakato wa shughuli hizi tayari umeshaanza kwa kuwahusisha wadau wa Mkoa wa Mbeya, wakiwemo Watendaji katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa hususan Afisa Elimu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi huu unahitaji fedha kwa ajili ya kuendeshea mafunzo kwa waelimishaji rika ambao ni wanafunzi na wanasihi ambao ni Walimu, shughuli zake zitasambazwa katika Mikoa mingine kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kipaumbele kitatolewa kwa Mikoa ambayo itakuwa tayari kuchangia gharama za mafunzo ya Mradi huo.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yake. Vile vile namshukuru kwa kukubali ombi langu la kupeleka Mradi wa PASHA katika Mkoa wa Mbeya. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa suala la mimba mashuleni kwa wanafunzi linakera sana na linaudhi sana; je, Serikali sasa ipo tayari kupitia Wizara hii kushirikisha Mashirika mengine yasiyo ya Kiserikali ili nayo yaweze kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi katika maeneo yao ili kuwanusuru hawa watoto wa shule ambao tunawapoteza kielimu na kiafya?

(ii) Kumekuwa na mazungumzo ya muda mrefu kuhusu wanafunzi wanaopata mimba mashuleni; je, ni lini Serikali sasa itaruhusu wanafunzi wa kike wanaopata mimba waweze kuendelea na masomo yao mara baada ya kujifungua?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, kipekee kwa namna anavyoshughulikia suala hili la mimba hasa katika mkoa wake. Vivyo hivyo pongezi ziwaendee Wabunge wote ambao kwa mara kadhaa, kwa nyakati tofauti, wamekuwa wakilizungumzia suala hili. Naomba niseme tu kwamba, Serikali yetu Tukufu ipo tayari siku na wakati wowote kupokea Mashirika yote ambayo yako tayari kutusaidia kutoa elimu ambayo itawezesha wasichana kutopata ujauzito.

Mheshimiwa Spika, suala la wanafunzi kupata mimba ni kubwa, linasikitisha, linafedhehesha na nisingependa kulizungumzia sana hili kwa sababu unapolijadili sana suala la mimba linaonesha kutokuwajibika ama kwa mabinti wenyewe au kwa wazazi au kwa jamii kwa ujumla. Hivyo, niseme kwa pamoja tushirikiane kutoa elimu kuwanasihi watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwarudisha shuleni wanafunzi wanaopata mimba ni suala la kisera na la kisheria. Hivi tunapozungumza, wiki iliyopita tumemaliza kikao na Kamati yetu ya Bunge ya Huduma za Jamii tukilijadili. Maoni yao yatafanyiwa kazi na bado tunaendelea kupokea. Tatizo kubwa lipo kwenye mambo matatu; ni baada ya muda gani wanafunzi hawa warudi shuleni ili wasiathiri afya za watoto wao na warudi shule zipi ili kuepusha unyanyapaa; lakini pia ni nani atachukua jukumu la kumlea mtoto yule kuhakikisha hatumpotezi. Haya yote yakishapata majibu yake na sisi pia tusingependa kuwaona mabinti hawa wanapoteza nafasi yao na haki yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba tu nimsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zetu, hebu tutumie mamlaka tuliyonayo kuzungumza na mabaraza, kuzungumza na wazazi wenzetu, lakini pia kuzungumza na watoto wenyewe ili wajitambue maana tukisema tunaelekeza lawama upande mmoja tutakuwa tunakoseana. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mradi huu wa PASHA baada ya kupelekwa katika mashule hayo shule husika kuendeleza Mradi huo kivyakevyake imepelekea wanafunzi kudai michango mingi sana kutoka kwa wazazi kwa ajili ya safari, si tu ndani ya nchi lakini pia nje ya nchi; je, Wizara inalitambua hilo na kama inalitambua inaratibu vipi ili kuhakikisha vijana wetu wanakuwa na usalama wanaposafiri nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Mradi wa PASHA kama tulivyoeleza, unahudumiwa na Serikali mbili. Mradi huu una malengo ya kuhamasisha pamoja na mambo mengine, kuepuka mimba za utotoni na maambukizi mapya ya UKIMWI. Michango inayotakiwa kwa ajili ya safari za nje au za ndani ni ridhaa ya mzazi na mwanafunzi mwenyewe. Kwa hiyo, kusema kwamba, tuzuie michango kwa wale wenye uwezo tutakuwa tunawanyima fursa na kusema kwamba tuseme Serikali ilipie pia na sisi hatuna uwezo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, Mradi ule madhumuni yake ni kutoa tahadhari, kuelimisha au kwa Kiingereza wanasema *awareness*. Mheshimiwa Mbunge, naomba tushirikiane, mzazi ambaye hana uwezo asijilazimishe.

Na. 58

**Sababu za Kuongezeka kwa Umaskini Nchini**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Ripoti ya "*Household Budget Survey*" iliyoangalia hali ya kiuchumi kwa maana ya kipato kwa kila Mtanzania inaonekana kuwa umaskini umeongezeka kutoka watu maskini milioni 11 mpaka milioni 12.9 mwaka 2007:

Je, Serikali italiambia Bunge ni sababu gani za msingi zimefanya umaskini wa Mtanzania kuongezeka kwa kiasi hicho badala ya kupungua?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti wa matumizi ya kaya (*Household Budget Survey*) ya mwaka 2007, imeonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka 35.7% mwaka 2000/2001 hadi 33.6% mwaka 2007, ingawa idadi ya Watanzania walio maskini imeongezeka kutoka milioni 11.4 mwaka 2001 hadi kufikia milioni 12.9 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zinazosababisha watu wengi kushindwa kupiga hatua za maendeleo kwa haraka, hivyo kusababisha wengi kubaki kwenye umaskini. Baadhi ya sababu hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Tija ndogo katika uzalishaji (*Low Productivity*) inayosababishwa na uwekezaji mdogo (Mitaji), pamoja na matumizi duni ya teknolojia kwa walio wengi;

(ii) Ukuaji mdogo wa mapato ya Serikali ukilinganisha na mahitaji yetu. Hali hii imesababisha uwekezaji hasa katika miradi ya miundombinu kama vile barabara, reli, bandari na nishati kuwa mdogo;

(iii) Ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo husababisha mazao mengi ya wakulima kubaki mashambani na hatimaye kuharibika;

(iv) Wananchi wengi kutokuyafikia masoko kwa urahisi;

(v) Sekta binafsi kushindwa kuhimili ushindani wa Kimataifa;

(vi) Ongezeko kubwa la idadi ya watu lisiloenda sambamba na viwango vya kupungua kwa umaskini; na

(viii) Wananchi wengi kutokuwa na elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto nyingi zilizopo, Serikali imechukua hatua mbalimbali zitakazowaongezea wananchi tija na hatimaye kupungua kwa kiwango cha umaskini. Baadhi ya hatua hizo ni:-

(i) Kutoa mikopo kwa wananchi na kuanzisha dirisha la mikopo kwa ajili ya kilimo katika *Tanzania Investment Bank*;

(ii) Kutoa mbegu na miche bora na iliyofanyiwa utafiti;

(iii) Kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wajasiriamali;

(iv) Kuendeleza elimu ya uzazi wa mpango; na

(v) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, umaskini unaoonekana kwa Watanzania wengi ni wa kipato, ambao kupungua kwake utachukua muda pamoja na kuhitaji mchango mkubwa na juhudi binafsi za wananchi wenyewe.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa takwimu hizi inaonekana ni wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Nne imeshindwa kutekeleza ahadi ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Je, Serikali ya CCM inasemaje kuhusu ahadi hiyo? *(Makofi)*

(ii) Kwa mujibu wa Ripoti ya MKUKUTA inaonesha kwamba Sekta ya Kilimo ilitakiwa ikue kwa asilimia 10 badala yake imekua kwa asilimia 4.4 na ndicho kinachotoa ajira zaidi ya asilimia 80 kwa Watanzania walio wengi. Je, Serikali haioni kuwa kubadili kaulimbiu leo kutoka "Kilimo Uti wa Mgongo" kuwa "Kilimo Kwanza" haitasaidia Watanzania kuondokana na umaskini badala yake tulihitaji kutumia fedha zetu za ndani za maendeleo kuliko kutegemea Wafadhili kama alivyoonesha katika bajeti mwaka jana na Wafadhili huwa hawatoi fedha kama inavyotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kuna *variables* nyingi sana ambazo ukizi-*integrate* ndizo zinazokupa maisha bora kwa kila Mtanzania. Suala la mapato ni moja ya maisha bora kwa kila Mtanzania, elimu, afya vyote hivi vinaonesha kwamba Serikali imepiga hatua na ndiyo inaonesha maisha bora kwa kila Mtanzania yameweza kufikiwa. Namwomba sana Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya avute subira. Ninataka nimwambie kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, kubadili kipato cha Mtanzania kunahitaji juhudi binafsi za Mtanzania mwenyewe. Nitatoa mfano, jana tulikuwa tunasikia Watanzania wanafanya shughuli kubwa za harusi, leo Watanzania hawa hawa wanafanya shughuli kubwa hata za mazishi. *We have to change our mind-set* katika kubadili maisha yetu; siyo suala la Serikali peke yake, lakini na Watanzania wenyewe nao wana wajibu wa kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya alizungumzia juu ya kubadili kaulimbiu; leo “Kilimo Kwanza”, kesho hivi; ninataka nimwambie kwamba, programu yoyote ile lazima iende na kaulimbiu ili wananchi wa kawaida waweze kukuelewa unataka kufanya nini. Katika hali kama hii, tumegundua kwamba, Watanzania wengi wako kwenye kilimo. Serikali imesema sasa kaulimbiu ni “Kilimo Kwanza” kwa maana gani; kwa maana kwanza tunataka kutanua kilimo lakini pili tunataka tu-*integrate* kilimo na sekta nyingine ili huyu Mtanzania wa kawaida aweze kuondokana na umaskini kupitia kilimo. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa sababu ahadi ya maisha bora kwa kila Mtanzania ilikuwa ni kaulimbiu katika hayo aliyoyaeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuwaelewesha Watanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 kutoka Chama cha Mapinduzi na ikifupisha Ilani yake ya Uchaguzi; na kwa kuwa katika majibu yake ametoa sababu za msingi zaidi ya saba zilizopelekea umaskini huu kuongezeka hadi kufikia watu milioni 12.9 na akichukulia kwamba hizo hoja zote saba zilikuwa katika sehemu ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM kwamba zitashughulikiwa katika kipindi cha miaka hii mitano; haoni kwamba ikiwa hadi hii leo zinaendelea kwa kikwazo na kinachopelekea Watanzania kuwa maskini kwamba wakati umefika kwa mwaka huu kutoa wito hapa kwa Wizara yake kuwaambia Watanzania watafute chama mbadala ambacho kitawaondoshea Watanzania katika umaskini huu uliokithiri? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Laah!!!! Waheshimiwa, hili swali limevuka mpaka kabisa, kwa sababu linaelekea elekea kwenye Kampeni ya Uchaguzi na pia kwa mujibu wa kanuni linajaribu kuwahisha shughuli ambazo bado hatujazifikia; kwa hiyo, naliondoa tunaendelea.

Na. 59

**Fedha za Kusaidia Maendeleo Katika Maeneo Maalum**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika maeneo maalum yenye mazingira magumu ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ludewa:-

Je, utekelezaji wa maamuzi hayo mazuri umekwamishwa vipi katika Wilaya ya Ludewa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, umeninyima fursa ya kumjibu Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, lakini haya tutajibizana nje huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza maamuzi yake juu ya utengaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika maeneo maalum, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ludewa.

Katika bajeti ya mwaka 2009/2010, Serikali imetenga jumla ya shilingi 680 milioni za kusaidia maendeleo katika Wilaya ya Ludewa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kutekeza miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa nyumba za Watumishi, mahitaji ya kujenga nyumba 15, shilingi 300 milioni zimetengwa kwa ajili ya kujenga nyumba 10;

(ii) Ujenzi wa Hosteli katika Shule ya Sekondari ya Manda, shilingi 220 milioni zimetengwa;

(iii) Kuweka umeme wa jua/*generator* katika hosteli ya Manda pamoja na majengo mengine ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, shilingi 100 milioni zimetengwa; na

(iv) Ununuzi wa Boti, shilingi 60 milioni zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2010, Hazina imekwishatoa fedha zote hizo. Hata hivyo, jukumu la utekelezaji wa miradi hiyo ni la Halmashauri yenyewe.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI**: Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanakonga sana mioyo ya Wananchi wa Ludewa hususan wale wa Kata za Manda na Mbunge wao. Sina budi kuishukuru sana Serikali kwa umakini wake wa kujali wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni pamoja na Wilaya ya Ludewa.

Kwa vile tatizo la uduni wa maendeleo katika Wilaya ya Ludewa linatokana na mawasiliano duni hususan miundombinu ya barabara, pamoja na mawasiliano ya majini; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaambia lolote Wananchi wa Ludewa kama Serikali inaweza kuzingatia yafuatayo:-

(i) Tumeomba tujengewe daraja ili kuboresha miundombinu hiyo tuondokane na shida ya kuwa kwenye maeneo ya periphery; tumeomba Serikali itatusaidie fedha kwa ajili ya Daraja kati ya Mbinga Mashariki na Ludewa, Kijiji cha Masimalafi?

(ii) Boti moja kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa, Ludewa, kilomita zaidi ya 100; boti moja haitoshi; Waziri anaweza kutusaidia au Serikali mtuongezee boti ya pili? Naomba kama inawezekana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja, maombi haya tunaendelea kuyashughulikia ili itakapowezekana, tuweze kutenga hela kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, lakini kuhusu boti, sasa hivi katika Ziwa Nyasa kuna boti mbili ambazo zinatembea; moja ni MV Songea na nyingine ni MV Iringa. Zimefanyiwa matengenezo na zinafanya kazi vizuri, lakini nafahamu kwamba, hazitoshi mahitaji ya usafiri wa wananchi katika eneo hilo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kulifanyia kazi tatizo hili ili tuone namna ambavyo tunaweza kuwapunguzia shida ya usafiri wa wananchi ambao wanatumia boti hizi kwenye Ziwa Nyasa.

Na. 60

**Wizi wa Mafuta ya Transfoma**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu TANESCO imekuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na wizi wa mafuta ya transfoma na hatimaye transfoma hizo kulipuka baadaye:-

(a) Je, TANESCO inachukua hatua gani kuzuia wizi huo?

(b) Kwa kuwa *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* wamegundua mfumo wa *electronic* wa kulinda transfoma hizo lakini TANESCO wamekaa kimya baada ya kuelezwa mfumo huo; je, jamii iwaeleweje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludocik John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi la wizi wa mafuta ya transfoma na Serikali inashukuru kwa ushirikiano unaooneshwa na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla katika kupambana na hujuma hizi. Mlinzi wa mali ya umma ni kila mwananchi, sote tunawajibika katika kuhakikisha kuwa miundombinu yetu ipo salama.

Mheshimiwa Spika, TANESCO imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na tatizo la wizi wa mafuta ya transfoma zikiwemo:-

(i) Kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na vipeperushi, kuomba ushirikiano wa wananchi katika kulinda miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme;

(ii) Kutoa motisha ya fedha kwa wananchi wanaotoa taarifa za kusudio au tukio la hujuma katika miundombinu ya umeme;

(iii) Kujenga vizuizi kuzunguka transfoma;

(iv) Kuhamisha transfoma na kuziweka mahali ambapo watenda hujuma wataonekana na jamii kirahisi;

(v) Kushirikiana na Jeshi la Polisi katika ukaguzi wa miundombinu ya umeme na hasa nyakati za usiku; na

(vi) Kuandaa mpango wa kubadili na kuanza kutumia aina ya transfoma zinazotumia mafuta na kuweka tranfoma zinazotumia hewa *(dry type).*

(b) Mheshimiwa Spika, kifaa kilichooneshwa na DIT ni kifaa cha mfano *(proto type)* na wala si zao halisi la matumizi *(commercial equipment*). Pendekezo la DIT lilijadiliwa na Uongozi wa Shirika na ukatolewa uamuzi kuwa zabuni iandaliwe kwa ajili ya kuitangaza na kuwe na ushindani kupatikana na vifaa vya aina hii kama Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 inavyotaka.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia pamoja na majibu ya swali hili kuchukua zaidi ya mwaka mmoja karibu na miezi minne lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa utafiti wa wataalam katika taasisi zetu za hapa Tanzania hata ukiwa mzuri namna gani haupati kuungwa mkono na taasisi ambazo zinatumia utaalam ule kwa sababu tu hakuna *ten percent* itakayofikiwa. Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha taasisi zinazopatikana katika vyuo vya kilimo pamoja na taasisi nyingine za ufundi zinaungwa mkono na kuweza kutumika katika kurahisisha maisha ya Watanzania?

(ii) Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba upo mpango wa kupata transfoma zinazotumia upepo badala ya zile zinazotumia mafuta; na kwa sababu TANESCO imeshatumia pesa nyingi mno kwa ajili ya kubadilisha transfoma ambazo zinaungua kwa sababu zimeibwa mafuta; je, TANESCO haioni ni vyema wakachukua hatua za haraka kuhakikisha kwamba sehemu zile ambazo mafuta yanaibwa sana wabadilishe haraka sana ili tuweze kutumia transfoma ambazo zinatumia upepo ili wananchi waendelee kupata umeme wakati wote katika maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la kwamba taasisi za utafiti kwenye vyuo vya kilimo, ufundi na kadhalika zinafanya kazi na kusema kweli sote tunajua kwamba ni kweli zinafanya kazi nzuri. Mimi sidhani kama tatizo la *accommodation* ya *research* hii ni ukosefu wa *ten percent* maana *ten percent* yenyewe inatoka wapi! Kwa sababu kwa ufahamu wangu, hizi taasisi za utafiti mara nyingi zinafanya kazi nzuri, lakini nadhani hili jambo Naibu Waziri wa Fedha amelizungumzia hapa amesema kuna suala la *mind-set* ambalo linahusu jamii nzima na utendaji mzima wa kazi, lakini pia kuweka *allocation* kubwa zaidi ya bajeti ili ikidhi kazi, kwa sababu kusema kweli utafiti huu unapunguza gharama kwa njia nyingi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa ana nafasi yake humu ndani

kama Mbunge ya kushinikiza matumizi ya utafiti ambao ni *locally induced,* nadhani hii kazi inatuhusu sote na siyo ya Serikali peke yake.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ambalo linasema kubadilisha transfoma kwenda kwenye transfoma za *dry type;* kwanza kabisa, niseme hili ni jambo la fedheha sana; ni jambo la aibu. Hii ni kwa sababu matumizi ya mafuta haya ya transfoma, utafiti unaonesha kwamba kwanza wanaoiba wanayatumia kwenye *welding* lakini wengine wanakwenda kuchanganywa na dawa nyingine na kutumika kama dawa ya ngozi na mkorogo. Wanasema akinamama, lakini siku hizi hata akinababa wanatumia mkorogo.

La mwisho, mafuta haya hutumika kupikia *chips* kwani huaminika kwamba hayaungui upesi, hayachafui *chips* na yanaweza kukaanga *chips* nyingi ukilinganisha na mafuta ya kawaida. Sasa haya ni mambo ambayo ni lazima sisi sote tukubaliane kwa pamoja tupige vita, siyo *solution* tumeingia gharama nyingi kununua transfoma ya kutumia mafuta sasa tuyabadilishe kwa sababu watu wanataka kutumia mkorogo na kukaangia *chips!*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na wadau wengine kuboresha hali ya ulinzi, bado nasisitiza kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wengine wote, tuna majukumu ya kulinda miundombinu inayopatikana kwa gharama kubwa sana.

**MHE. OSCAR R. MUKASA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa tatizo la ubunifu wa DIT ambalo limeshindwa kuchukuliwa na kuingia kwenye matumizi ya Shirika la TANESCO ni mfano tu wa tatizo kubwa tulilonalo miongoni mwa watafiti wetu la kutoka kwenye utafiti kwenda kwenye ubunifu lakini hatua ya pili kutoka kwenye matumizi; je, Serikali hasa kupitia Wizara ya Sayansi na Teknolojia inatueleza nini kuhusu kujenga uwezo wa Tume ya Sayansi na Teknolojia katika kukabiliana na tatizo hili linalotunyima fursa ya kuendana na dunia ya sasa ya Sayansi na Teknolojia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tatizo la utafiti kwenda kwenye ubunifu na ubunifu kwenda kwenye matumizi kwamba, utafiti ule unapokuwa *local* unapunguza gharama nyingi sana *vis-a-vis* matumizi ya utafiti unaofanywa nje ya nchi ambao unakuwa na hati miliki na gharama zake ni kubwa na kadhalika. Tunapoufanya wenyewe pia unakuwa na *content* ya *local knowledge*. Kwa hiyo, ninachosema Serikali imepokea hili jambo na kama tunavyozidi kuhimiza matumizi ya utafiti wa ndani, ninadhani sisi kwenye Wizara ya Nishati na Madini tumelipokea kwa upande wetu kwa matumizi ya utafiti kwa mambo yanayotuhusu pale Wizarani, lakini ninaamini na wenzangu Serikalini wameyasikia na ni jambo ambalo tunalifanyia kazi.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa katika Jiji la Dar es Salaam mgao wa umeme unaaendelea na umeme ukikatika eneo fulani asubuhi aidha utarudishwa saa sita mchana au jioni au usiku na pengine mpaka asuhuhi. Sasa hivi kuna tabia ya umeme kukatika mara kwa mara katika eneo ambalo tayari linaeleweka lina

mgao na hii hupelekea kuharibu vifaa vya wananchi vinavyotumia umeme. Je, ni sababu zipi za kiufundi zinazopelekea TANESCO kukata umeme eneo ambalo tayari limeshajulikana lina mgao baada ya dakika tano na kurudisha baada ya dakika kumi na kukata tena baada ya dakika kumi na kurudisha baada ya dakika thelathini?

**SPIKA:** Sina hakika kama linahusiana na transfoma lakini Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mgao ni jambo ambalo linapangwa kitaalam kwa ajili ya kuboresha akiba ya umeme kulingana na matumizi yaliyopo. Sasa hili analolizungumzia Mheshimiwa Chaurembo ni jambo la ubovu kwa sababu mgao haupangwi ukatokea baada ya saa moja halafu baada ya dadika kumi ukarudi halafu dakika kumi na tano ukakatika tena. Kwa hiyo, ukiona jambo hili limetokea, basi ujue moja kwa moja kwamba, hili sasa ni tatizo la kiufundi na kama ilivyo, kwa utaratibu matatizo kama haya ya kiufundi yanapotokea, TANESCO wanatakiwa kuja kufanya marekebisho mara moja na kama hawakuja basi kuna utaratibu wa wateja kufikisha taarifa ili tatizo hilo lieleweke na lifanyiwe kazi mara. Kwa hiyo, hili si tatizo la mgao ni tatizo la kiufundi.

Na. 61

**Ahadi ya Mheshimiwa Rais Kupeleka Umeme Ngorongoro (Loliondo)**

**MHE. KAIKA SANING’O TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa vigezo vya kuharakisha maendeleo ya kuchumi na ustawi wa jamii katika Wilaya ni pamoja na Barabara, Umeme, Madini, Mazao ya Kilimo, Mifugo, Utalii na wananchi kufanya kazi kwa bidii na maarifa; na kwa kuwa tarehe 20 Machi 2007 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi Wananchi wa Ngorongoro (Loliondo) kwamba watapatiwa umeme:-

(a) Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme Loliondo itatekelezwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza ahadi zote za Serikali hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu 2010?

(c) Je, Serikali itatuhakikishiaje kwamba itaweza kufikisha umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya zote nchini ikiwepo Loliondo kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005/2010?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning’o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Serikali imetenga fedha za kununua mitambo minne yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1.25 kila moja

itakayofungwa Loliondo. Majenereta hayo ni sehemu ya mitambo 17 itakayonunuliwa kwa ajili ya Kigoma/Ujiji (5), Kibondo (2), Kasulu (2), Sumbawanga na Nkasi (4) na Lolindo (4). Aidha, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, imetenga fedha za utekelezaji wa Miradi ya Umeme ukiwamo Mradi wa Kusambaza Umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro (Loliondo), Kibondo, Kasulu na Nkasi, pamoja na vijiji vitakavyopitiwa na njia hiyo ya umeme. Mradi wa Loliondo utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 11 yenye umbali wa kilomita 15 na ujenzi wa kituo cha kufua umeme kwa kutumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, kazi ya zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kujenga njia ya umeme ilitangazwa mwishoni mwa mwezi Julai, 2009. Mkandarasi kwa ajili ya ufungaji wa majenereta yote 17 ni Kampuni ya *Zwart Technick* ya Uholanzi. Kutokana na ufinyu wa bajeti, ilionekana ununuzi wa majenereta ufanyike kwa awamu kwa kuanza na ununuzi wa majenereta tano kwa ajili ya kigoma, ambapo kazi ilianza Septemba, 2009 na itakamilika Juni, 2010; Serikalli ilitoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa majenereta 12 yaliyobaki Desemba, 2009.

Mheshimiwa Spika**,** baada ya maelezo hayo ya awali, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika**,** ahadi ya Mheshimiwa Rais imekwishaanza kutekelizwa kama ilivyoelezwa hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, mipango na ahadi za Serikali zinalenga kuongeza kasi ya kufikia maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya nchi yetu na kunyanyua viwango vya maisha ya Watanzania. Hivyo, Serikali inatekeleza ahadi zake kama ilivyoahidi kulingana na uwezo bila kujali iwapo ni kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu au la.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kwa kutumia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* na Washirika wengine wa maendeleo kuhakikisha kwamba, inafikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini ikiwemo Loliondo kama ilivyoahidiwa katka Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005/2010. Utekelezaji wa miradi ya kufikisha umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya zote umeshaanza na uko katika hatua mbalimbali.

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri na yenye kutia matumini. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Mpango wa awali wa TANESCO kuipatia umeme Mkao Makuu ya Wilaya Ngorongoro, yaani Loliondo ilikuwa ni mpaka mwaka 2015, lakini Waziri anatuambia kwamba Mkakati wa Serikali ni kununua majenereta 17 kwa awamu kutokana na ufinyu wa fedha zinazotengwa katika bajeti. Je, Serikali haioni ufinyu huo wa bajeti utapunguza kwa kiasi kikubwa ile azma ya Serikali ya kupeleka umeme Loliondo katika kipindi hiki cha kutekeleza Ilani ya Uchaguzi?

(ii) Naomba nifahamu utafiti uliofanyika katika Mto Pinging kwa ajili ya maji ya mto huo kama unaweza kusaidia umeme katika Mji wa Waso na Loliondo; je, nini matokeo ya utafiti huo na je; anaweza kusaidia katika kutekeleza azma ya kupeleka umeme Loliondo na Waso?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, mimi nadhani labda Mheshimiwa Mbunge hakunielewa, kwa sababu kama mpango wa awali ulikuwa kupeleka umeme mwaka 2015 kwenda Loliondo; nilichosema ni kwamba, kulikuwa na maeneo mbalimbali jumla yalikuwa majenereta 17 ya Loliondo ni manne. Sasa tulichofanya kwa sababu ni ahadi ya mwaka 2008/2009, tulianza na utekelezaji wa majenerata matano kwanza za Kigoma zikatolewa pesa Septemba 2009, zikanunuliwa. Tatizo lake ni kwamba, ukitoa pesa ndiyo inaanza *process* ya kutengeneza, kwa hiyo, mara nyingi akilipa leo majenerata yatapatikana baada ya miezi 12 au mwaka mmoja na nusu.

Mheshimiwa Spika, sasa nilichosema ni kwamba, kwa sababu hili jambo liliishaanza kufanyiwa kazi, Septemba tumeanza na majenereta matano ya Kigoma, *process* hiyo itakwisha Juni, 2010. Tulichosema hapa ni kwamba, Desemba, 2009, Wizara ya Fedha imetoa pesa za kulipia majenereta na tayari yameshalipiwa. Kwa hiyo, yale majenereta 12 pamoja na manne ya Loliondo na manne ya Nkasi na Sumbawanga na manne ya Kasulu na Kibondo, tayari yapo kwenye *process* ya kuyakamilisha. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba, zitakuwa zimefungwa ifikapo Desemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali nimesema pia kwamba, REA ndiyo wanatumika kusambaza zile nyaya pale. Kwa hiyo, haitoshi tu peke yake kwamba, uende ukaweke jenereta Loliondo, bado kuna kama kilomita 15 ambazo umeme huo inabidi uende maeneo mbalimbali ya Loliondo. Kazi hiyo inafanywa na REA na tayari kazi hiyo imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa upande wa Loliondo mimi nadhani mpaka itakapofika mwisho wa mwaka huu, *Inshallah* mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la maji ya Mto Kili; suala hili linahusiana na utekelezaji wa sera na kazi ya REA. Popote ambapo pana uwezekano wa kupata maji ikawa ni chanzo cha umeme, tunaangalia kama kuna uwezekano wa kupatikana *mini-hydro*.

Tumeangalia hivi kwa maeneo ya Namtumbo, tumeangalia kwa maeneo ya kule kwa Mheshimiwa Nsanzugwanko na maeneo ya Kigoma juu ambako kuna maji na

Nzovwe pale Sumbawanga. Kwa hiyo, hili nalo lina-*qualify* kuingia katika kufanyiwa kazi na REA.

Mimi naomba nilipokee niwape REA walifanyie utafiti kama ni chanzo cha umeme ambao utatosha kupeleka umeme Waso na Loliondo na kama ni jambo ambalo linawezekana, siku zote umeme wa chanzo cha maji ni nafuu zaidi na mwepesi zaidi kuliko umeme wa jenereta.

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda, naona ni vyema tuendelee. Sasa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali linalofuata ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Kimbita, linaulizwa na jirani yake Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro.

Na. 62

**Upungufu wa Maji Kutokana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa Duniani**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO (K.n.y. MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mabadiliko makubwa ya hali ya hewa duniani yamesababisha kuwepo na upungufu mkubwa wa maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo pamoja na umwagiliaji:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliepusha Taifa na janga hilo kubwa?

(b) Je, Serikali kupitia Halmashauri zote nchini iko tayari kubaini mabwawa yote ya zamani na kupembua na kusanifu mapya?

(c) Je, ujenzi wa Bwawa la Boloti na mabwawa mengine madogo madogo katika Wilaya ya Hai utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Archt. Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Jimbo la Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanatokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha athari kubwa kwa vyanzo vya maji nchini. Tathmini iliyofanywa hapa nchini, inaonesha kwamba, kati ya miaka 50 mpaka 60 iliyopita, kumekuwepo na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto 1°C, ikiambatana na upungufu wa mvua na kupungua kwa kina cha maji katika maziwa na mabwawa yetu.

Aidha, tathmini inaonesha kwamba, katika miaka 50 hadi 100 ijayo kutakuwa na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto 1°C hadi 3°C katika nchi yetu. Ongezeko hilo litaanzia Kaskazini Mashariki kwenda Kusini Magharibi.

Kutokana na mabadiliko hayo, Serikali imeona umuhimu wa kuliweka jambo hilo katika mipango yake ili kubaini njia za kukabiliana na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Archt. Fuya Godwin Kimbita, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inachukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga mbalimbali kwa kuainisha suala la mabadiliko ya tabianchi katika Mipango ya Mabonde na Maji. Hatua za utekelezaji zinazochukuliwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi.

(ii) Kuendeleza mafunzo ya wataalam na wananchi ili kuongeza uelewa na weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

(iii) Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

(iv) Kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji; hatua zinazochukuliwa ni kuwa Ofisi na Bodi za Maji za mabonde zinawashirikisha wananchi na wadau wengine katika kuendeleza na kusimamia matumizi ya rasilimali za maji na kulinda vyanzo vya maji kwa kusimamia sheria zilizopo, kuhakiki vyanzo vya maji ili kutathmini kiwango cha uchafuzi.

(v) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu yenye kipaumbele ya menejimenti ya rasilimali za maji kwa kutumia vyanzo vikubwa na vya uhakika kama vile mabwawa.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kuwa hatua hizi zitaliepusha taifa letu katika janga hilo kubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa itaendelea kuendeleza na kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kubaini mabwawa ya zamani ili hatua za kuyafufua zichukuliwe. Hadi sasa Serikali tayari imebaini mabwawa ya zamani 626 katika mabonde yafuatayo: Bonde la Rufiji (3), Wami/Ruvu (156), Bonde la Kati (104), Ziwa Tanganyika (35), Ziwa Victoria (132), Pangani (134) na Ruvuma na Pwani ya Kusini (62). Mabwawa hayo yalipembuliwa na kati yake 132 yameonekana yamechakaa, yanavuja na mengine yamepasuka.

Aidha, Serikali kwa kutumia Sheria ya Rasilimali za Maji Na. 11 ya 2009 inaendelea kubaini mabwawa yanayohifadhi majitaka yanayotokana na shughuli za migodi *(Tailings Dams)*. Serikali tayari imekagua Migodi ya *Williamson Diamond*

*Limited* na *El-Hallal Diamond Limited* iliyopo Wilaya ya Shinyanga, *Resolute Gold Mine Limited* (Nzega), *North Mara Gold Mine* (Tarime), *Geita Gold Mine* (Geita), Tulawaka *Gold Mine* (Biharamulo), Bulyanhulu *Gold Mine* (Kahama), Buzwagi *Gold Mine* (Kahama) na Kiwira *Coal and Power Limited* (Ileje).

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekamilisha upembuzi yakinifu wa mabwawa mengine 19 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida, Shinyanga na Tabora. Tayari mabwawa yote yameshafanyiwa usanifu, gharama za ukarabati na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Aidha, Serikali imeandaa hadidu za rejea kwa ajili ya kusanifu Mabwawa ya Farkwa (Dodoma), Ndembela (Iringa) na Kidunda (Morogoro).

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1989/1990, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, kupitia Shirika la JICA, ilifanya upembuzi yakinifu wa maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Kanda za Chini za Rombo na Hai. Upembuzi huo ulionesha kuwa kuna uwezekano makubwa wa kujenga Bwawa la Boloti kwenye Mto Lawati. Naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Hai kutumia ripoti ya upembuzi yakinifu iliyokwishafanywa na kuingiza ujenzi wa Bwawa la Boloti katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ya Hai kwa ajili ya utekelezaji.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hatua nzuri ambazo Wizara inachukua, inatambulika kwamba uharibifu wa mazingira unatokana na kuharibika misitu ambayo inakadiriwa kuwa ekari 500,000 kwa mwaka, inaleta athari kubwa na inaleta mmomonyoko wa ardhi na mmomonyoko wa ardhi unasababisha udongo kujaa kwenye mabwawa; je, Serikali inalijua tatizo hili na inachukua hatua gani ili kuepusha janga hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inalijua tatizo hili na tunajua kabisa kwamba, matatizo yanayosababisha mmomonyoko wa ardhi hayapo tu katika maeneo yale yenye mabwawa, yanaanzia katika *catchments*. Yapo katika maeneo ambayo watu wengi, hasa huko kwenye misitu ndiko wanakofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni suala ambalo linatuhusu sisi wote, Halmashauri zote na wananchi wote, kwa sababu kama nilivyosema, sisi tunasema tabianchi, lakini wakati mwingine nasema ni tabiawatu vile vile kwa sababu watu ndiyo wanaofanya kazi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Serikali inalijua hili na ndiyo maana tunashirikiana sasa na Halmashauri zote nchini, mashirika na taasisi nyingine kuwaelimisha wananchi kujiepusha na tabia zote zinazoweza kusababisha uharibifu wa misitu kama vile mioto isiyotakiwa, kilimo kibaya katika *catchments* na katika mito ili angalau tuweze kudhibiti tatizo hili. Najua litachukua muda, lakini hatuwezi kulidhibiti tu kwa kutunga sheria, ni pamoja na kuwaelimisha wananchi. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba tunalijua na Serikali inaendelea kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Tunaendelea, muda wa maswali umefika mwisho, lakini tumalize hili linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora.

Na.63

**Tatizo la Upatikanaji wa Maji Manispaa ya Tabora**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Tabora ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama; na kwa kuwa Manispaa hiyo hutegemea maji kutoka Bwawa la Igombe na Kazima ambayo yamejaa tope na kusababisha maji hayo kuwa na tope chafu na rangi ya kijani ambazo hutoa harufu mbaya pamoja na uchakavu wa mabomba ya kusambaza maji kwenda kwenye hifadhi ya maji *(tanks)*:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tope kwenye mabwawa hayo ili kuwaondolea adha Wananchi wa Manispaa hiyo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuleta mabomba makubwa ya kisasa ili kuondokana na uchakavu wa mabomba hayo mitaani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-
Vyanzo vikuu vya maji kwa ajili ya Manispaa ya Tabora ni mabwawa mawili ya Igombe na Kazima. Bwawa la Igombe lilijengwa na kuanza kufanya kazi mwaka 1958. Ukubwa wa Bwawa hili ni mita za ujazo milioni 47; kati ya hizo mita za ujazo milioni 21 hazitumiki *(Dead Storage)* na sehemu inayoweza kutumika *(Live Storage)* ni mita za ujazo milioni 26.

Bwawa la Kazima lililojengwa mwaka 1952 likiwa na meta za ujazo milioni 1.6 ni chanzo kingine cha maji katika Mji wa Tabora. Chanzo hiki nacho kwa sasa hakifanyi kazi kutokana na kupungua sana kwa kina cha maji. Mabwawa yote mawili yana umri wa zaidi ya miaka 50 tangu yalipojengwa, hivyo kuna kiasi kikubwa cha tope ambacho kinapunguza ujazo wa kuhifadhi maji na kuathiri ubora wa maji. Pia, kuota kwa magugu juu ya maji, hasa wakati wa kiangazi na kuoza kwa mimea iliyobaki wakati wa ujenzi wa bwawa, vinasababisha ugumu katika kutibu na kusafisha maji ya Bwawa la Igombe na hivyo kutumia dawa nyingi ili kufikia ubora unaotakiwa kimataifa kwa mujibu wa *World Health Organization Standards.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchemba, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kutoa tope linalosababisha kupunguza kwa ujazo kwenye mabwawa haya, kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba, gharama ya kutoa tope ni kubwa kuliko kujenga bwawa lingine jipya. Ili kukalibiliana na tatizo la upungufu wa maji, Serikali inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Uswisi

*(SECO)* kufanya uchunguzi wa kina ili kujua kiasi cha tope lililoingia katika Bwawa la Igombe. Lengo la uchunguzi huu ni kujua sehemu ya bwawa ambayo imejaa tope ili kujua kiasi halisi cha maji yanayohifadhiwa sasa katika bwawa ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Manispaa ya Tabora.

Uchunguzi huu utasaidia kubuni chanzo mbadala cha maji kufidia pengo lililopo. Uchunguzi huu pia unafanywa sambamba na usanifu wa miundombinu ya maji itakayoongeza uzalishaji wa maji katika chanzo hicho.

Miundombinu itakayowekwa ni pamoja na mtambo wa kutibu maji, pampu mpya za kusukuma maji, kulaza bomba kuu la maji kutoka kwenye chanzo mpaka kwenye mtambo wa kutibu maji na kufunga *transformer* na jenereta. Matarajio yangu ni kwamba, Mhandisi Mshauri atakamilisha kazi ya usanifu mwezi Mei, 2010 ili kazi ya ujenzi nayo ianze.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa maji, sampuli za maji zinachukuliwa kila mwezi na kupimwa na Ofisi ya Mkemia Mkuu Mwanza na sampuli nyingine zimepelekwa Uswisi ili kubaini sababu za ugumu wa kutibu maji ya Kituo cha Igombe. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuchagua teknolojia nzuri ya kusafisha maji ili kuhakikisha ubora wa maji yanayozalishwa unafikia kiwango cha Kimataifa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo kubwa la upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Tabora, imeweka mpango wa muda mfupi na muda mrefu. Katika kutekeleza mpango wa muda mfupi, mwezi Januari, 2009 Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (TUWASA), ilitumia shilingi 115,200,000 kubadilisha mabomba chakavu katika maeneo ya Cheyo (Barabara za *Hill* na Kilimatinde), yenye urefu wa kilomita 3.4, kazi ambayo imekamilika mwezi Februari, 2010. Aidha, mwezi huu (Aprili, 2010), Serikali imeongeza shilingi 230,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa pampu mbili mpya zitakazofungwa katika Kituo cha Igombe badala ya pampu chakavu zilizopo sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kukarabati mfumo wa maji utakaobadilisha mabomba chakavu yenye urefu wa km 23.4 katika Mitaa ya Jamhuri, Chemchemi Mtaa wa Amani, Kanyenye Mtaa wa Kakola, Rehani B, Mbugani Mtaa wa North na maeneo ya *National Housing*. Kazi hii itasaidia kupunguza tatizo la maji yanayopotea linalosababishwa na uchakavu wa mabomba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye ufafanuzi na yenye kuridhisha, nichukue nafasi hii ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri aliyoifanya alipokuja kwenye ziara yake. Pia, nimpongeze kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa kwa Wakazi wa Manispaa ya Tabora na leo fedha hizo zimekwenda; kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee zimfikie Mheshimiwa Rais; alipokuwa Tabora tarehe 8, Siku ya Wananwake, alitoa tamko la utekelezaji wa muda mrefu wa maji ya Manispaa ya Tabora, kuhakikisha Tabora inapata maji safi na salama. Kubwa, nimpongeze pia Naibu Waziri…

**SPIKA:** Lenga swali tafadhali!

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Nimpongeze Naibu Waziri na yeye pia alikuwepo kwenye msafara huo. Je, yuko tayari kupeleka salamu hizi kwa wahusika ambao nimewataja? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ya swali la msingi na vile vile kumshukuru Mheshimiwa Mchemba, kwa salamu ambazo tutazifikisha pale ambapo zimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza tu maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa alipokuwa akilihutubia Taifa kutoka Tabora; nayo ni kwamba, pamoja na hatua nyingine ambazo inabidi Serikali tuzichukue ili kutatua tatizo la maji Tabora kwa maana ya kuliondoa kabisa, ni kuangalia uwezekano wa kuunganisha Tabora hatimaye na Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria wa Kahama na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, baada tu ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara yangu imeanza kulifanyia kazi hilo na tunaamini huo utakuwa ndiyo ufumbuzi wa kudumu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimenasa, maana maswali mawili yamebaki ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na muda umepita. Tutajitahidi yaweze kushughulikiwa kesho au keshokutwa.

Matangazo; tukianza na wageni; wapo wageni wa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala ambao ni Dr. Stergomena Tax – Katibu Mkuu, yule pale, karibu sana. Naibu Katibu Mkuu, Bwana Uladi Mussa, yule pale, ahsante sana. Naomba sasa waliobaki Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mbalimbali katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki wasimame ili Waheshimiwa Wabunge wawaone. Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao ni walimu 13 kutoka Iringa wakiongozwa na Mwalimu Idd Kanju. Naomba wasimame walimu kutoka Iringa, wale pale. Karibuni sana ndugu zetu walimu na poleni kwa safari na kazi yenu tunaithamini. Tunathamini sana kazi za walimu sisi Wabunge. Yupo pia ndugu yake Mheshimiwa Monica Mbega, ambaye anaitwa Monica Masawe anatoka Moshi.

Tatu ni wageni wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, ambao ni kikundi cha watu saba kutoka Ilala Dar es Salaam, kikundi hiki kinajulikana kama “KITU K” na wanaongozwa na Bi. Babia; naomba wageni wa Ilala wasimame tafadhali. Ahsante sana.

Basi hili fumbo la “KITU K” nadhani Mheshimiwa Zungu analijua; sijui maana yake ni nini lakini basi ndiyo wapiga kura hao na ndiyo fursa yao nao.

Wageni wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Dorah Mushi ni Viongozi wa Chama cha Wachimba Madini Mkoa wa Manyara, Mererani, ambao ni wafuatao nikiwatamka naomba mmoja mmoja wasimame; Ndugu Zephania Munga, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara; Ndugu Abuu Mollel, Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Manyara; Ndugu Bahati Msuya, Muweka Hazina; na Ndugu Elinami Mungure, Mwanasheria wa Haki Madini. Hawa wamejipanga vizuri wana Mwanasheria kabisa; karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Makete na Kyela; Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, nao ni raia wa Ujerumani, Bwana Thomas Reinhardt ambaye ni muwekezaji katika Sekta ya Kitalii kwenye fukwe za Matema za Ziwa Nyasa na ambaye pia anamalizia ujenzi wa Hoteli ya Kitalii iitwayo *Crazy Crocodile Camp Site;* Loh! Sijui kama jina hili lina mvuto sana, lakini *Crazy Crocodile* linatisha, wakati wowote mamba anaweza akakulamba basi tena na maisha yakawa yamekwisha; lakini karibu sana nadhani wanajua kuwadhibiti hao mamba wa Ziwa Nyasa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi zetu za Kibunge; Mheshimiwa Omar Kwaang’, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, nimemruhusu ili Kamati ya Huduma za Jamii iwe na Kikao leo saa tano, yaani hivi punde katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kwa madhumuni ya kujadili Muswada wa Sheria ya Famasi *(The Pharmacy Act, 2010).*

Muswada huu umegawiwa hivi punde na ulitetwa kwa Hati ya Dharura, kwa hiyo, wameitwa baadhi ya Wadau na wengine ndiyo maana Mkutano unafanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa tano leo.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, mkutane leo saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement.*

Mheshimiwa Abdisalaam Khatibu, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara, mkutane saa saba mchana, Ukumbi Namba 227, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Miundombinu wakutane saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, nimeruhusu Kamati hiyo ikutane saa tano asubuhi, Ukumbi Namba 219, kuzingatia Muswada muhimu wa Sheria ya Madini.

Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane nje ya Jengo hili la Bunge, saa tano asubuhi, kwa safari ya kwenda Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, *bus* litakuwepo nje ya Ukumbi wa Bunge karibu na Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ziara ambayo nimeiruhusu ya Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ni leo na mkusanyike kuanzia saa tano asubuhi hii.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo, sasa tuendelee na kazi zinazofuata, nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kauli ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa Kauli ya Serikali Kuhusu Matumizi ya Kiswahili Katika Shughuli Rasmi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ndiyo Lugha pekee ambayo huzungumzwa na kueleweka na idadi kubwa zaidi ya Watanzania nchini kote. Tangu wakati wa Utawala wa Kikoloni katika Karne ya 19 na baada ya kupata Uhuru mwaka 1961, Kiswahili kimeendelea kutumika kama lugha ya mawasiliano mapana kwa Tanzania. Kiswahili siyo Lugha tu bali ni chombo muhimu sana ambacho kimewaunganisha Watanzania wakati wa kupigania Uhuru. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitumia Kiswahili kuwaunganisha Watanzania wote kudai na kupigania Uhuru na Ukombozi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Lugha ya Kiswahili imeimarisha uhusiano na umoja wa jamii za humu nchini na kuifanya nchi ionekane kama ina jamii moja badala ya zaidi takriban ya makabila 130.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Lugha ya Kiswahili imekuwa kielelezo thabiti cha Utamaduni wa Mtanzania na kitambulisho kikuu cha Lugha yetu; hivyo hatuna budi kuikuza na kuiimarisha. Haikuwa kwa bahati nasibu kwamba, Kiswahili kilitangazwa kuwa Lugha ya Tanzania mwaka 1962, kwa kuzingatia umuhimu huu wa Lugha ya Kiswahili, muda mfupi baada ya Uhuru kunako tarehe 10 Desemba, 1962, kwa mara ya kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika wakati huo, alilihutubia Bunge kwa Lugha ya Kiswahili, hatua ambayo ilisababisha kutolewa matamko mbalimbali na Viongozi wa Serikali kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1967, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, Hayati Mzee Rashid Mfaume Kawawa, alitoa Waraka wa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri zama hizo walijulikana kama Mawaziri Wadogo, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Walimu wote na Watumishi wa Serikali wote ambao ulisisitiza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kila Afisa wa Serikali na Viongozi wote wawe mfano mwema katika kutumia Lugha ya Kiswahili. Pili, kusiwe na kuchanganyachanganya lugha na mfano mzuri alisema tuanzie katika mijadala yetu ndani ya Bunge letu Tukufu. Tatu, Maafisa Elimu na Walimu wote wana wajibu wa kuona kuwa watoto na vijana wa shule zote wanakielewa Kiswahili. Mwisho, watu tuone fahali katika Lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1974, aliyekuwa Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, Utumishi, Bwana Julius Mganga, alitoa Waraka wa Utumishi Namba Moja wa 1974, ulioeleza kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Ofisi za Serikali ambapo alisisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, barua kati ya Wizara na Idara ziwe za Kiswahili isipokuwa kama anayeandikiwa ni mgeni. Pili, vibao vyote vya majina ya Ofisi au Wizara na Matangazo kama ya Mahafali na Sikukuu mbalimbali yaandikwe kwa Kiswahili. Tatu, madokezo baina ya Maafisa maofisini yawe ni kwa Lugha ya Kiswahili. Nne, fomu zote za kujaza za Kiserikali ziwe za Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei mwaka 2005, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Mheshimiwa William Lukuvi, aliagiza Taarifa za Mikutano, Semina na Warsha nchini, zitolewe kwa Kiswahili kwa manufaa ya Wananchi. Pia Taarifa za Miradi inayohusu Wananchi ni lazima zitolewe kwa Lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na vipeperushi na nyaraka zinazohusu Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Kikao cha Baraza la Mawaziri tarehe 18 Februari, 2010, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Ali Mohamed Shain, alisisitiza suala la matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na kuwakumbusha Watendaji wa Serikali kuzingatia Waraka wa Hayati Mzee Kawawa, alioutoa akiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Matamko hayo na umuhimu wa Lugha ya Kiswahili ikiwa sasa pia ni Lugha ya Kimataifa inayotumiwa mathalani kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Umoja wa Afrika; Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, inasisitiza matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na kutoa kauli kuwa pamoja na vipengele vilivyosisitizwa hapo awali, vipengele vifuatavyo navyo vizingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, dhifa mbalimbali za Kitaifa, Hotuba, Warsha, Semina na Mikutano ya Kitaifa, iendeshwe kwa Lugha ya Kiswahili. Pili, majina ya Barabara, Mitaa na Mabango, yaandikwe kwa Lugha ya Kiswahili. Tatu, Maafisa wa Serikali na Maafisa wa Umma watumie Kiswahili katika shughuli zao zote kama vile

Vikao vya Bodi za Kurugenzi mbalimbali, mawasiliano ya kiofisi, matangazo ya kazi, mahojiano, kuitwa kwenye usaili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nne, mbao za matangazo na nyaraka zinazobandikwa za Taifa ziandikwe kwa Lugha ya Kiswahili. Tano, Sheria ziandikwe katika Lugha ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na kutafsiri zile zilizoandikwa kwa lugha ya kigeni na pia jitihada za makusudi zifanyike ili shughuli za Mahakama katika ngazi zote ziendeshwe kwa Lugha ya Kiswahili. Sita, mijadala inayohusu shughuli za umma iendeshwe kwa Kiswahili na kumbukumbu zote zihifadhiwe kwa lugha hii ikiwa ni pamoja na nyaraka zilizotumika katika mijadala kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Vyombo vya Habari vinavyotumia Lugha ya Kiswahili vihakikishe vinatumia Kiswahili sanifu na mwanana huku vikizingatia kwa dhati kabisa Sarufi za Kiswahili. Tuzidi kukienzi Kiswahili, Lugha yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na ninatumaini Serikali mtakwenda mbali zaidi, pengine hata mikondo mingine ya kusoma mpaka juu kule, iwepo mikondo ya Kiswahili. Zipo nchi ndogo sana zinasomesha vijana wao sayansi na kadhalika kwa Lugha zao. Sasa sioni kwa nini elimu inabadilika, ikifika juu basi inakuwa ni lugha ya kigeni kitupu; ibaki hivyo lakini iwepo mikondo inayowezesha wanasayansi wazuri wanaoweza kufanya Hisabati, Kemia, Fizikia kwa Kiswahili. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu kwa shughuli inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Famasi wa 2010 *(The Pharmacy Bill, 2010)***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante, Muswada huo wa Sheria ya Famasi umesomwa kwa mara ya kwanza, Katibu kwa hatua nyingine.

## HOJA ZA SERIKALI

## A Z I M I O

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipomaliza shughuli Siku ya Ijumaa, kulikuwa bado kuna orodha ya wachangiaji. Sasa wameongezeka wamekuwa wanane, nilikuwa nataka tumalize shuguli hii saa saba lakini tutaangalia namna itakavyokwenda. Orodha yangu ina Wabunge wafuatao:-

Waheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na mwingine ameleta sasa hivi Mheshimiwa Oscar Mukasa. Sina uhakika kama wote tutapata nafasi, tujihadhari na kurudiarudia ile ya kusema Kenya, meno ya tembo, Doha na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, hayo yamesemwa sana, sasa mtu ukirudiarudia itabidi nitumie Kanuni ili urudi kwenye hoja mpya. Sasa nitaanza na Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, wakati huo Mheshimiwa Raynald Mrope ajiandae.

Samahani, sana kumbe hata Azimio halijasomwa, sikuwepo Ijumaa! Niliarifiwa taarifa hazikukaa vizuri, Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5(2) cha Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kimeainisha hatua za mtangamano za Jumuiya kuwa ni Umoja wa Forodha, ukifuatiwa na Soko la Pamoja kisha Sarafu Moja na hatimaye Shirikisho la Kisiasa.

Kifungu cha 151 cha Mkataba kinazitaka Nchi Wanachama kukamilisha Itifaki katika maeneo ya ushirikiano, zikiainisha malengo, upeo na kanuni za uendeshaji.

Aidha, kifungu hiki kinabainisha kwamba, kila Itifaki itakayoandaliwa, itathibitishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama na hatimaye kuridhiwa na Nchi Wanachama kwa mujibu wa taratibu za kila nchi.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja yalianza rasmi mwezi Aprili, 2008 na kukamilika mwezi Oktoba, 2009. Tarehe 20 Novemba, 2009 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sambamba na Viongozi Wakuu wa Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliweka sahihi Itifaki ya Soko la Pamoja.

Nchi Wanachama zote zinatarajiwa ziwe zimeridhia Itifaki ya Soko la Pamoja ifikapo tarehe 30 Aprili, 2010 ili Itifaki iwe na nguvu ya kisheria na kuanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Julai, 2010 kwa kuzingatia makubaliano yaliyomo ndani ya Itifaki yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inabainisha kwamba Bunge litaridhia itifaki ambazo kwa masharti yake zinahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa kuunda Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ulihusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;
- Baraza la Wawakilishi;
- Wizara;
- Idara zinazojitegemea;
- Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali; na
- Sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha mchakato huu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kushukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi pamoja na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Masilingi Mbunge, kwa michango yenu na ushauri mliotoa wakati nilipowasilisha taarifa mbalimbali kuhusu mwenendo wa mjadiliano wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni yenu yalisaidia Serikali kuboresha msimamo wa Tanzania katika majadiliano na kuhakikisha kuwa maslahi ya Watanzania yanazingatiwa kikamilifu katika Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Aprili 2010 nilipata fursa ya kufanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Itifaki ya Soko la Pamoja ambapo nilieleza kwa kina yaliyomo katika Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha Azimio la kuliomba Bunge kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, naomba kuelezea kwa muhtasari mambo ya msingi yaliyomo katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, uundaji wa Soko la Pamoja; katika uundwaji wa Soko la Pamoja mfumo uliokubalika ni kuunda Soko la Pamoja hatua kwa hatua kulingana na ratiba zitakazokubaliwa na nchi wanachama. Kwa mantiki hii, uondoaji wa vikwazo au ulegezaji wa masharti kwa mwananchi wa Afrika Mashariki kutoka nchi moja kwenda nyingine kwa madhumuni ya kufanya biashara ya huduma, uwekezaji, uanzishaji wa shughuli za kiuchumi, uhamiaji na ukazi si mambo yatakayoruhusiwa kwa asilimia 100 toka siku ya kwanza ya utekelezaji wa Soko la Pamoja bali yatatekelezwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo makuu ya msingi ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Kwa mujibu wa Ibara ndogo za 76(1) na 104(2) za Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki maeneo ya msingi yaliyohusishwa katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo:-

(1) Soko huru la bidhaa ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Goods);*

Mheshimiwa Spika, Soko huru la bidhaa linasimamiwa na Itifaki ya Umoja wa Forodha na Sheria ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa shughuli za Forodha ya mwaka 2004. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha ulianza rasmi mwezi Januari 2005 na kipindi cha mpito cha miaka mitano cha kuondoa Ushuru wa Forodha katika biashara ya bidhaa kwa nchi wanachama kimekwisha rasmi tarehe 31 Disemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe moja Januari, 2010 biashara ya bidhaa zote zinazokidhi matakwa ya vigezo vya uasili wa bidhaa vya Afrika Mashariki baina ya nchi wanachama hazitatozwa Ushuru wa Forodha.

(2) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kusafiri katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya *(Free Movement of persons);*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7 ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki inawahakikishia raia wa nchi wanachama uhuru wa kuingia, kutembea na kupata ulinzi na usalama bila kubaguliwa kwa misingi ya Utaifa wao.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na uhuru tajwa hapo juu raia wa nchi yoyote ya Afrika Mashariki atawajibika kuzingatia yafuatayo:-

(i) Ni lazima awe na Hati halali ya kusafiria;

(ii) Kupita katika vituo rasmi mipakani; na

(iii) Kukamilisha taratibu za uhamiaji;

(iv) Kupata kibali cha kuingia na kukaa nchini kwa kipindi cha miezi sita. Kwa maana hiyo tunaposema uhuru wa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine maana yake tunasema uende lakini utumie taratibu zilizokubaliwa, kwa hiyo hakuna uhuru usiokuwa na mipaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa hati halali za kusafiria zilizokubalika katika ngazi ya Jumuiya ni:-

(i) Hati za kusafiria za nchi wanachama;

(ii) Hati za kusafiria za Afrika Mashariki;

(iii) Hati za muda za kusafiria za Nchi Wanachama;na

Mheshimiwa Spika, uhuru huu wa kuingia na kukaa katika nchi yoyote mwanachama unahusisha raia wanaoingia nchini kwa nia ya kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kutembelea ndugu na jamaa;

(ii) Kutafuta huduma ya matibabu;

(iii) Wanafunzi; na

(iv) Wanaopita kuelekea nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ili kupata kibali cha kuingia nchi yoyote ya Afrika kama mwanafunzi, mhusika atatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kuonyesha uthibitisho wa kupata nafasi ya masomo katika shule, vyuo au taasisi za elimu zilizosajiliwa rasmi.

(ii) Uthibitisho wa ufadhili kwa kipindi cha masomo.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaotimiza masharti hayo watapewa hati ya kuingia na kukaa nchini kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Hati hiyo itakuwa ikiongezwa muda kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja hadi kukamilisha kipindi cha masomo.

Mheshimiwa Spika, uhuru huu wa kuingia, kutembea na kukaa katika nchi wanachama unaweza kukataliwa au kusitishwa kwa sababu za kisera, kiusalama au kiafya.

Mheshimiwa Spika, raia aliyeingia katika nchi nyingine wanachama kwa utaratibu uliotajwa hapo juu hataruhusiwa kuajiriwa au kujiajiri katika nchi husika. Aidha, kibali cha kuingia na kukaa katika nchi yoyote mwanachama kinachopatikana kwa utaratibu uliotajwa hapo juu hakitatozwa malipo yoyote.

(3) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya kazi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Workers*);

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya Itifaki ya Soko la Pamoja inawahakikishia raia wa Nchi Wanachama uhuru wa kupata ajira katika nchi yoyote mwanachama na kutobaguliwa kwa misingi ya Utaifa katika masuala ya ajira na maslahi na haki nyingine za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na uhuru huu mfanyakazi atawajibika kuwa na mambo yafuatayo:-

(i) Hati halali ya kusafiria; na

(ii) Mkataba wa ajira na kupita katika vituo rasmi mipakani ambapo baada ya kukamilisha taratibu za uhamiaji atapewa hati ya kuingia na kukaa ndani ya nchi mwanachama kwa kipindi cha miezi sita wakati akikamilisha taratibu za kupata kibali cha kufanya kazi (*Work Permit*) kwa kazi inayozidi siku 90 au hati maalum (*Special Pass*) kwa kazi isiyozidi siku 90. Aidha, mwenzi na watoto wa mfanyakazi watapaswa kukamilisha taratibu za kupata hati ya utegemezi (*Dependant Pass*). Uhuru wa kupata ajira katika nchi yoyote mwanachama hautahusisha ajira katika sekta ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo uliokubalika wa kuunda Soko la Pamoja hatua kwa hatua kulingana na ratiba tutakazokubaliana, nchi wanachama zimeainisha katika jedwali kada zitakazohusishwa na ufunguaji wa soko la ajira na vipindi husika. Kwa upande wa Tanzania kada hizo na muda wa kufungua ajira ni kama ifuatavyo:-

(i) Walimu wa vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu wenye Shahada ya Uzamivu kuanzia 2010;

(ii) Walimu wa shule za sekondari katika fani ya hisabati, fizikia, biologia na lugha za kigeni kuanzia 2015;

(iii) Walimu wa shule za msingi zinazofundisha kwa lugha ya Kiingereza wenye angalau Shahada ya Kwanza kuanzia 2010 isipokuwa kwa upande wa visiwani;

(iv) Walimu wa Vyuo vya Kilimo, Ufundi Stadi na Utamaduni wana kiwango cha elimu cha angalau Shahada ya Pili katika fani husika kuanzia 2010;

(v) Wahandisi wa madini kuanzia 2011;

(vi) Wahandisi wa majengo kuanzia 2010;

(vii) Wahandisi wengine kuanzia 2012;

(viii) Maafisa Ugani katika sekta ya kilimo kuanzia 2015;

(ix) Wauguzi na Wakunga kuanzia 2010;

(x) Wahudumu wengine wa sekta ya afya kuanzia 2015;
(xi) Kada ya waongoza ndege kuanzia 2012; na

(xii) Kada ya upimaji ramani kuazia 2015.

Mheshimiwa Spika, Kada nyingine zitaendelea kufunguliwa hatua kwa hatua kadri ya mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Uhuru huu wa kufanya kazi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya unaweza kukataliwa au kusitishwa kwa sababu za Kisera, Kiusalama na Kiafya.

(4) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya biashara ya huduma katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya *(Free Movement of Services*);

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 ya Itifaki inahakikisha uhuru wa soko la biashara ya huduma ndani ya Jumuiya kwa kuondoa vikwazo hatua kwa hatua na kutoanzisha vikwazo vipya kwa watoa huduma kutoka katika nchi wanachama. Aidha, nchi wanachama zimeahidi kutowabagua wafanyabiashara ya huduma kwa msingi wa Utaifa wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia nchi wanachama zimekubaliana kuanza kuondoa vikwazo katika sekta saba za huduma zilizoainishwa katika jedwali la uhuru wa biashara ya huduma kama ifuatavyo:-

- Sekta ya huduma za biashara.
- Sekta ya huduma za mawasiliano.
- Sekta ya huduma za ugavi.
- Sekta ya huduma za uwakala.
- Sekta ya huduma za elimu.
- Sekta ya huduma za kifedha.
- Sekta ya huduma za utalii.
- Sekta ya huduma za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, sekta zilizotajwa hapo juu zitafunguliwa hatua kwa hatua kulingana na ratiba ya utekelezaji kama inavyobainishwa katika Jedwali la ufunguaji wa biashara ya Huduma. Kwa hiyo, taasisi zetu za usimamizi wa biashara ya huduma itabidi zizingatie ratiba za ufunguaji wa soko la biashara ya huduma, ili kuepuka wageni kufanya shughuli za huduma ambazo hazijaruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kufungua biashara ya huduma katika sekta ya utalii, hususan uwekezaji katika hoteli na migahawa. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaruhusu wageni kuwekeza katika hoteli na migahawa ya kuanzia hadhi ya nyota tatu isipokuwa kwa maeneo ya visiwani na kwenye mbuga za wanyama ambapo wageni wataruhusiwa kuwekeza katika hoteli zenye hadhi ya kuanzia nyota nne.

(5) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza mitaji katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Capital*);

Mheshimiwa Spika, Nchi Wanachama zimekubaliana kuondoa vikwazo kwa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza kwenye soko la mitaji katika nchi nyingine ndani ya Jumuiya hatua kwa hatua kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji inayoonyeshwa katika jedwali la kuondoleana vikwazo katika uwekezaji wa mitaji. Katika jedwali husika kila nchi imeainisha vikwazo vilivyopo katika soko lake la mitaji na ratiba ya kuviondoa vikwazo hivyo ili hatimaye soko la mitaji liwe huru kwa wawekezaji kutoka nchi za Jumuiya.

(6) Haki ya raia wa Afrika Mashariki kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na uchumi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Right of Establishment*);

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Itifaki inawahakikishia raia wa Afrika Mashariki haki ya kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na uchumi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya kwa kuondoa vikwazo vinavyohusiana na Utaifa wa Kampuni au mjasiriamali husika. Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kuandaa orodha ya vikwazo katika sheria zao na kuviwasilisha katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya Itifaki kupata nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, ili kuruhusiwa kufanya shughuli za kiuchumi na biashara katika Nchi yoyote Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itabidi kuzingatia masharti yafuatayo:-

(i) Kuwa na Hati halali ya kusafiria.

(ii) Kupita vituo rasmi mipakani.

(iii) Kukamilisha taratibu za kuanzisha biashara katika nchi husika kama vile leseni ya biashara, kuwa na mtaji wa kutosha, kusajiliwa kwa ajili ya kodi na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika**,** Ibara ya 15 ya Itifaki inabainisha wazi kuwa suala la upatikanaji na matumizi ya ardhi na majengo litasimamiwa na sheria za nchi wanachama. Kwa sababu hiyo, Raia wa Afrika Mashariki akienda Nchi yoyote Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima azingatie sheria na taratibu zinazosimamia masuala ya ardhi ya nchi husika, kwa maneno mengine hakuna nchi yoyote ya Afrika Mashariki iliyomhakikishia mwana Afrika Mashariki yeyote yule kwamba akienda kwenye nchi ile atapewa ardhi, ardhi itaendelea kusimamiwa na sheria za nchi wanachama.

(7) Haki ya ukazi kwa raia wa Afrika Mashariki katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Right of Residence*).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Itifaki inawahakikishia raia wa nchi wanachama walioruhusiwa kuingia katika nchi nyingine kwa ajili ya ajira kwa mujibu wa Ibara ya 10 ya Itifaki au kwa ajili ya kuanzisha shughuli za biashara na uchumi kwa mujibu wa Ibara ya 13 ya itifaki, haki ya ukazi katika nchi husika. Raia anayetaka kukaa nchi yoyote ndani ya Jumuiya anatakiwa kuomba kwenye mamlaka husika kibali cha ukazi (*Residence Permit*) ndani ya siku 30 tangu tarehe ya kuingia nchini kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kuwa na hati halali ya kusafiria;

(ii) Kuwa na kibali cha kufanya kazi nchini; na

(iii) Kuwa na nyaraka nyingine zitakazohitajika na ofisi za uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa suala la ukazi wa kudumu (*Permanent Residence*) litaendelea kusimamiwa na sheria husika za nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo ya msingi yaliyoainishwa katika mada hii hayazuii Nchi Mwanachama kuchukua hatua za kujihami pale itakapotokea athari katika utekelezaji kijamii, kiusalama na kiafya. Aidha, Nchi Mwanachama inaweza ikachukua hatua za kujihami kudhibiti matokeo yoyote hasi katika utekelezaji, (Kifungu cha 48).

Mheshimiwa Spika, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki linaleta fursa na changamoto mbalimbali kwa nchi wanachama. Katika kujipanga ili kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja kwa ufanisi, Wizara inaandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Mkakati huo utaliongoza Taifa katika kufikia malengo yake ya kuboresha maisha ya wananchi kwa kutumia vema fursa za Soko la Pamoja na kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, chambuzi mbalimbali zimebaini kuwa kiwango cha uelewa wa wananchi kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado ni kidogo. Ili kukabiliana na changamoto hii Wizara imeandaa mkakati wa elimu kwa umma kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaolenga kupandisha kiwango cha ufahamu wa Watanzania kuhusu mtangamano na fursa zinazoletwa na mtangamano huu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2009, (*The Protocol on the Establishment of the East African Community Common Market of 2009).*

KWA KUWA**,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 1999;

NA KWA KUWA**,** Marais wa Nchi Wanachama tarehe 20 Novemba, 2009 waliweka sahihi kwenye Itifaki ya kuanzisha Soko la Pamoja (*The East African Community Common Market);*

NA KWA KUWA**,** Malengo ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Nchi Wanachama hususan katika:-

(i) Kukuza na kuendeleza biashara ya bidhaa na huduma, ajira na uwekezaji mitaji, kuhakikisha urahisi wa ubadilishaji fedha na kuimarisha uwekezaji katika masoko ya uwekezaji mitaji ili kuwa na mfumo mmoja wa kifedha;

(ii) Kuimarisha na kuratibu mahusiano ya kiuchumi na kibiashara miongoni mwa Nchi Wanachama pamoja na kuwianisha sera za jumla na za kisekta kwa lengo la kuleta maendeleo;

(iii)Kupanua wigo wa shughuli za kiuchumi, ikiwemo kuondoa vizuizi vya upatikanaji wa ajira, huduma, kuwianisha sera na sheria za ajira pamoja na kuimarisha viwango na vituo vya pamoja vya ajira na hatimaye kuwa na sera moja ya ajira ya Jumuiya;

(iv)Kuimarisha ushirikiano katika kuendeleza Uchumi, Kilimo na Viwanda ikiwemo kuimarisha uwekezaji, uzalishaji, ushindani na masoko katika ngazi ya Jumuiya na Kimataifa;

(v) Kuwianisha sera za kodi na kuondoa vizuizi vya kiufundi (*technical barriers*) katika masuala ya kibiashara, kutambua viwango na kutekeleza sera ya pamoja ya kibiashara kwa Jumuiya;

(vi)Kujenga uelewa wa pamoja na kuimarisha uhusiano kwa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(vii) Kuimarisha tafiti na maendeleo ya teknolojia na kutumia na kulinda taarifa za tafiti hizo ili kukuza na kuimarisha maendeleo; na

(viii) Kuweka taratibu za ufuatiliaji wa shughuli za soko la pamoja ili kuhakikisha kuwa ziko katika misingi ya Itifaki ya kuanzisha Soko la Pamoja (*The East African Community Common Market).*

NA KWA KUWA, Malengo ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kurahisisha zoezi la watu kutoka mpaka mmoja hadi mwingine, ili kuwa na mfumo mmoja wa uratibu wa mipaka, ikiwemo:-

(i) Raia wa Nchi moja Mwanachama kuruhusiwa kuingia katika mipaka ya nchi nyingine Mwanachama pasipo kutakiwa kuwa na visa**;**

(ii) Uhuru wa kutoka katika sehemu moja kwenda sehemu nyingine wakiwa ndani ya Nchi nyingine Mwanachama;

(iii)Uhuru wa raia wa Nchi moja Mwanachama kukaa ndani ya nchi nyingine Mwanachama na kuondoka bila vizuizi, isipokuwa tu uhuru huo utazingatia mipaka itakayowekwa na Nchi Mwanachama, ambayo mtu huyo atatembelea, kutokana na sababu za sera za Kiserikali, usalama wa nchi pamoja na usalama wa afya ya Umma; na

(iv) Kuhakikisha ulinzi wa raia kutoka Nchi Wanachama wakati atakapokuwa ndani ya nchi nyingine mwanachama kwa kuzingatia sheria za nchi ambayo raia huyo atakuwa ametembelea, isipokuwa tu, uhuru huo hautazuia raia huyo kuchukuliwa hatua za kisheria iwapo atakuwa amekiuka sheria za nchi husika.

NA KWA KUWA, masharti mbalimbali yaliyoko katika Itifaki yanahifadhi haki ya Wanachama kuendelea kuzingatia Sera na Sheria za nchi zao katika:-

(a) Kuruhusu raia wa Nchi Mwanachama kutembelea Nchi nyingine Mwanachama kwa kutumia pasi au vitambulisho vya uraia wa Nchi Wanachama ambazo zitakubaliana;

(b) Kutoruhusu umiliki na matumizi ya ardhi ya kila Nchi Mwanachama isipokuwa kwa kufuata sheria na taratibu za Nchi Mwanachama;

(c) Kuruhusu raia wa Nchi Mwanachama kufanya kazi na kuishi katika Nchi nyingine Mwanachama;

(d) Kufungua milango ya kufanya biashara na kuondoa taratibu na vikwazo vilivyowekwa na sheria na vya kiutendaji.

NA KWA KUWA, kwa kuridhia Itifaki ya kuanzisha Soko la Pamoja *(The East African Community Common Market)*, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itawawezesha Watanzania na Taifa kwa jumla kunufaika zaidi na fursa zitokanazo na ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo soko kubwa la pamoja la bidhaa, mitaji, huduma na ajira na vile vile kutoa fursa zaidi za uwekezaji pamoja na ushirikiano katika nyanja za kiuchumi na kijamii;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakusudia kushirikiana na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kubuni sera na kuweka mikakati madhubuti ya utekelezaji itakayowezesha kukua kwa uchumi na kuondoa umaskini;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki ya kuanzisha Soko la Pamoja (*The East African Community Common Market)* kutaimarisha ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kujenga umoja wa kikanda wenye nguvu na sauti kubwa zaidi katika nyanja za Kimataifa;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki ya kuanzisha Soko la Pamoja *(The East African Community Common Market)* na kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuwepo kwa Itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Tisa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa linaazimia Kuridhia Itifaki ya

Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2009, (*The Protocol on the Establishment of the East African Community Common Market of 20*09).

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha hoja hii kuhusu Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2009, (*The Protocol on the Establishment of the East African Community Common Market of 2009*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja**.**

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa hoja hiyo ya Azimio la kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, limeungwa mkono na sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Zungu tupate maoni ya Kamati kuhusu Azimio hili.

**MHE. MUSA A. ZUNGU – (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu, nataka kuwasalimia wananchi wa Jimbo la Ilala na kueleza mimi niko imara hapa Bungeni kutetea maslahi yao na wajue mimi ni mtumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya nataka kupongeza timu zote mbili zilizocheza mechi jana kwa kuonyesha mchezo safi wa kiwango cha juu sana. Si kwa matokeo yaliyoonekana bali timu zote mbili hizi zinatoka Jimbo la Ilala.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Protocol on the Establishment of the East African Community Common Market)*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Protocol on The Establishment of The East African Community Common Market),* kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipelekea kazi Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 31 Machi 2010, Kamati ilikutana Dar es Salaam kupewa maelezo na ufafanuzi kuhusu Itifaki hii inayopendekezwa kuridhiwa na

Bunge, uliotolewa na Mheshimiwa Dkt. Diodorus B. Kamala Mbunge, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Katika kikao hicho, Kamati ilipata muda wa kutosha kupitia na kujadili hoja ya Serikali kuhusu Azimio hili linalozihusisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Kamati kujadili na kuona maudhui na mantiki ya Itifaki hii, tulielezwa madhumuni ya kuanzishwa kwa Soko la Pamoja, ni kupanua na kuimarisha ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya nchi zote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge hili kuwa Kamati iliridhika kwamba, iwapo Itifaki hii itaridhiwa, Watanzania na Taifa kwa jumla watanufaika zaidi na fursa zitokanazo na ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya hii. Moja ya manufaa kwa Tanzania ni upatikanaji wa soko kubwa la bidhaa, huduma na ajira. Aidha, Soko la Pamoja litatoa fursa zaidi za uwekezaji pamoja na ushirikiano katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopitia na kuchambua maudhui ya Itifaki inayopendekezwa kuridhiwa, ilibaini kuwa iwapo Bunge lako Tukufu litaridhia Itifaki hii, nchi yetu itafanikiwa kuongeza uzalishaji na biashara. Aidha, kuwepo kwa uhuru wa ajira ndani ya Jumuiya, Watanzania wengi wataweza kupata fursa za ajira na kuongeza ujuzi na uzoefu kutokana na maingiliano ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutaja faida nyingine za Soko la Pamoja kuwa ni kukua kwa uwekezaji kutokana na sera, sheria na taratibu zinazolenga kukuza na kuendeleza Sekta Binafsi. Hali kadhalika, miundombinu ya kiuchumi na kijamii itaimarika kutokana na utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kikanda na hivyo kuinufaisha nchi yetu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, Wajumbe walihoji masuala mbalimbali yaliyohusu nyanja ya elimu, ajira, umiliki wa ardhi na mahusiano yetu na Nchi za Afrika Mashariki. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu vikwazo ambavyo vimekuwa vikiwekwa na baadhi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya, hasa linapokuja suala linaloihusu Tanzania. Aidha, Kamati ilitaka kujua utaratibu wa matumizi ya Hati ya Kusafiria ndani ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, baada ya kuridhiwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, tunaipongeza sana Serikali yetu kwa kuwa makini kwani yale yote yaliyoshauriwa na Kamati yamezingatiwa katika Itifaki hii. Ushauri huo ulilenga suala la umiliki wa ardhi ndani ya Jumuiya kuendelea kusimamiwa na Sheria za Nchi husika, matumizi ya Hati Halali za Kusafiria miongoni mwa Nchi Wanachama na suala la ukazi wa kudumu litaongozwa na Sheria za Nchi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inaafiki mapendekezo ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Protocol on The Establishment of The East African Community Common Market).* Kamati ilizingatia masuala yote ya msingi baada ya kutafakari maelezo na ufafanuzi wa kina, kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pamoja na maelezo hayo, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ichukue juhudi za makusudi kuwaelimisha wananchi Wilayani, kwa kutumia lugha nyepesi kuhusu Itifaki ya Soko la Pamoja. Lengo ni kuwawezesha Watanzania kutumia kikamilifu fursa mbalimbali zinazojitokeza.

(ii) Mitaala ya Elimu ya Tanzania iboreshwe kwa kuingiza programu mbalimbali kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla, ili kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika Ushirikiano huu.

(iii) Serikali iweke sheria mbalimbali zitakazobainisha na kusimamia uwekezaji katika nyanja ya uchumi kama zilivyo Nchi za Marekani na Ulaya.

(iv) Dhana ya kukuza Diplomasia ya nchi yetu na Nchi za Jumuiya hii iendelee kuimarishwa kuepusha kujitenga kimahusiano na nchi hizo, kwani lengo la Jumuiya hii ni kuleta uhusiano na ushirikiano baina ya Nchi Wanachama.

(v) Kwa kuwa itifaki hii ni mtambuka, mchakato wa utekelezaji wake uzihusishe kikamilifu Wizara zote, Sekta na Taasisi Binafsi, kwa kuandaa mikakati maalum ya kuhakikisha utekelezaji huu unawezekana kwa ufanisi na uwazi na si kuliacha jukumu hili kwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki pekee. Hali kadhalika, Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta zisimamie utekelezaji wa Itifaki hii katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati yangu. Aidha, namshukuru kwa dhati Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala; Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed A. Mohamed na Wataalam wa Wizara, kwa ufafanuzi wa kina wa hoja zilizojitokeza na hatimaye Kamati kukubali pendekezo la Serikali kuhusu kuridhiwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mjumbe;

Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mjumbe; Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mjumbe; Mheshimiwa William J. Kusila, Mjumbe; Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mjumbe; Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mjumbe; Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mstaafu Feteh S. Mgeni; Mjumbe; Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mjumbe; Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mjumbe; Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stella Mlambo, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashillilah, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuwasilisha maoni ya Kamati hiyo. Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba Kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Azimio la Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu wetu kwa kutuweka wazima na wenye afya, lakini pia kwa kuniwezesha kusimama hapa kwa ajili ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Azimio hili la Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Pili, napenda niwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Mgogoni kwa kuwa pamoja na mimi na naamini kuwa bado wataendelea kuniamini na kuwa pamoja nami kwa wakati wote. Kwa upande wangu nawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana kwa ajili ya kujenga Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameshaweka saini yake pamoja na wakuu wa nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki tokea tarehe 20/11/1009, kwa ajili ya kukubali itifaki hii. Linalotakiwa sasa ni kwa Bunge hili Tukufu kuridhia itifaki hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 55 ya Itifaki ya Soko la pamoja na vile vile Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki inasisitiza uundwaji wa soko hilo kwa hatua na pia kuweka maeneo muhimu ya soko hilo katika nyanja kama vile za soko huru la biashara *(free movement of goods)* uhuru wa raia kusafiri nchi yoyote kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, uhuru wa kufanya kazi, biashara, kuwekeza mitaji na ukaazi; lakini zote kwa mujibu wa sheria na utaratibu uliokubaliwa. Maeneo haya ni kwa mujibu wa Ibara ya 76(1) na 104(2) za Mkataba wa Jumuiya ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kwamba suala hili ni muhimu na zuri kwa Taifa letu. Lakini tuna wasiwasi mkubwa sana kwa ukosaji wa uratibu *(co-ordination)* kwa Wizara zetu za Tanzania. Ubovu huu ndio unatusababishia kuwa nyuma kwa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, mifano mizuri ni kuwa, sisi tulianza nyimbo za kuimarisha bandari zetu kwa ajili ya soko la bara (*interland*) kama vile Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Malawi na Zambia. Wakenya walipoona tumelegea katika suala hili sasa wanajenga bandari kubwa sana hapo Lamu. Kwa misingi hiyo hiyo, sasa pia wanajenga Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa hapo Taveta, Kenya kwa lengo la kuua kiwanja chetu cha Kilimanjaro. Je, soko hili kwa misingi hii kweli tunaweza kufaidika sana?

Tutazame pia jinsi gani viwanda vyetu vimekufa kama vile *General Tyres* wakati wenzetu wanazidi kuimarisha viwanda vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inaonyesha dhahiri kwa mfumo tulionao Tanzania na ikiwa hatukujirekebisha haraka na ukitilia maanani umahiri wa Kenya wa kutokuwa na muhali katika masuala ya biashara, maisha Kenya yatakuwa juu wakati Tanzania yatakuwa yako nyuma. Mifano kadhaa inaweza kutolewa ili kuonyesha ni namna gani Kenya wanavyotusakama. Kwa mfano, Kenya wanapinga uongezaji wa mgao wa kuwinda kwa sababu tu Kenya wao wana msimamo wa kutokuwinda Kenya walipania kukwamishwa kwa utalii Tanzania kutokana na pendekezo lao la kumpandisha daraja simba katika mkutano uliofanyika Bangkok nchini Thailand.

Kupinga kwa Kenya katika Mkutano wa Doha kwamba Tanzania isiruhusiwe kuuza akiba yake ya meno ya tembo nalo ni tatizo lingine. Lakini Kambi ya Upinzani inaona haya ni muhimu kuyazingatia lakini bado hayana uhusiano sana na suala zima la Itifaki hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, urafiki huu au umoja aina hiyo si mzuri hata kidogo. Rafiki wa kweli ni yule anayejali shida zako. Je, kwa sababu hizi na nyingi nyinginezo, tunaweza kukataa tusiridhie Azimio hili au hata kuliahirisha hadi hapo mambo yatapotengemaa? Kambi ya Upinzani inaamini kwamba wenzetu hawa hawana nia njema.

Mheshimiwa Spika, hata ukirudi nyuma mpaka wakati ule wa kuvunjwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977 bado tunahisi sababu hizo za kuvunjika Jumuiya hiyo zipo na bado hazijaondoka. Ni vema tukaziangalia kwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, uingiaji wetu huu wa kuifurahisha siasa tu bila kujali uchumi wa nchi unaweza kutuweka mahali pabaya kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza Serikali kuwa lazima kuwe na ushirikiano mzuri wa Wizara kwa Wizara na kuondoa kabisa urasimu uliojengeka ndani ya Wizara zetu na kuhakikisha kuwa Uzalendo wa kujenga nchi yetu uwepo vinginevyo malisho haya kijani yaliyopo Tanzania yataliwa na Kenya bila ya huruma yoyote.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza ni kwamba, je, kada zilizohusishwa katika soko la pamoja kama vile walimu wa vyuo, wahandisi, maafisa ugani na kadhalika ni kuwa zitafunguliwa kwa ajira kwa vipindi mbalimbali kuanzia 2010 – 2015. Suala la kujiuliza ni kwamba, je, kada hizi kwa Tanzania zimezingatiwa ipasavyo? Kwa sababu leo Tanzania utaona katika maeneo mengi kama vile hoteli, maduka na kadhalika ina wafanyakazi wa Kenya, Watanzania wanaweza kujiuliza, je, muda wa kada hizo kufunguliwa ni tayari.

Mbona maeneo yote hayo yamejaa Wakenya wakati sisi Watanzania bado hatujapata nafasi hizo? Jibu ni la. Lakini ni kutokana na kulegea kwetu na kutokujali Uzalendo na ushirikiano wa pamoja ndio uliotufikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, hadithi hizo zote zinatuvunja moyo na kuona kwamba hakuna haja ya kuridhia Azimio hili. Lakini je, kufanya hivi ndio kweli tutatua tatizo lililopo?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya maelezo niliyoyaeleza hapo juu mwanzoni kabisa, basi ufumbuzi ni kuwa tuliridhie Azmio hilo lakini Tanzania tuwe mahiri zaidi katika kulinda haki za wananchi wetu. Ni lazima pia Bunge hili Tukufu likemee kwa nguvu zote kuhusu vitendo vya kijangili vinavyofanywa na wenzetu kama vile wa Kenya. Kwa misingi hiyo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono juu ya hoja ya Bunge hili Tukufu kuridhia Ttifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini pia Bunge hili lione haja ya kukemea masuala haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono Azimio hilo la kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki la Mwaka 2009 (*Protocol on the Establishment of the East African Community Common Market 2009)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakar kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Sasa nilikwishatamka wachangiaji wale watatu wa mwanzo ambao ni

Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Raynald Mrope. Sasa namwita Mheshimiwa Anne Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimeweza kuwa hapa siku ya leo na kuweza kuchangia Azimio hili ambalo ni Azimio muhimu sana. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukweli, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Kamala kwa jinsi ambavyo anafanya kazi yake vizuri. Maana yake tuseme ukweli wakati mwingine mnyonge mnyongeni lakini ni vema umpe haki yake kwanza. Mheshimiwa Kamala naomba upokee pongezi zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikiano wa kikanda kwa lugha ya kitaalam *Regional integration* kama hiyo ya kwetu sasa hivi Jumuiya ya Afrika Mashariki. inazo hatua ambazo zinafahamika kitaalam. Kwa lugha ya kigeni tunaanza na *customs Union* ambayo inahusu kushirikiana katika masuala ya forodha. Hatua ya pili ni hii ambayo leo tunaizungumzia ya *common market* ambayo ni soko la pamoja. Hatua ya tatu ni *economic union* ambayo itatufanya turuhusu kuwa na sarafu moja. Hatua ya mwisho kubwa kuliko zote itakuwa ni ya *political union* ambayo itaturuhusu tuwe na kiongozi mmoja wa kisiasa au tuwe na Rais mmoja. Lakini sasa nirudi kwenye Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Itifaki ambayo ndiyo iko mbele yetu tunayotakiwa kuiridhia sisi Bunge ili sasa iweze kuanza kazi rasmi kisheria.

Mheshimiwa Spika, hii hatua ya pili, hatua ya Soko la Pamoja *(Common Market)* ni hatua nzito sana. Ni hatua ambayo inaweza ikatufanya sisi Watanzania tukafaidi, tukaendelea kiuchumi lakini pia tusipokuwa makini inaweza ikatufanya tukatumiwa na wenzetu kujijenga kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba niguse uhuru wa Raia wa Afrika Mashariki kufanya kazi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*free movement of workers).* Hapa nitapaongea kidogo na ningeomba Serikali hapa mnione kwamba niko makini. Siku zote kwenye mpira, timu mbili zikiingia kwenye mpira zinaweza zikaanza kwa mbwembwe mbwembwe kwa kufanya mazoezi, kwa kuzunguka zunguka, lakini hakishaingia refa, akipiga kipenga timu zile zinasimama mstari, zinajipanga, zinakaguliwa ndio zinapoanza mpira sasa, ndio zinapoanza mchezo, sasa kipenga ni leo.

Mheshimiwa Spika, kipenga ni leo ndio tunapokuja kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja, ndio tunatakiwa tujipange mstari, tukaguliwe, mchezo ndio uanze kwa wale ambao tunaangalia mpira. Lakini naiomba Serikali iwahakikishie Watanzania kwamba kipenga ni leo na baada ya leo ndio tutaanza kucheza mpira. Kwa nini nasema hivyo, mpira huu ulishaanza kuchezwa na wenzetu siku nyingi sana kabla hatujapiga kipenga. Hili jambo tusipoliangalia tutaumia sisi.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mahoteli yote ya kitalii, anayekuletea chai, anayekuletea soda, hata anayekutandikia kitanda lafudhi yake si ya Kitanzania. Kwa hiyo, mpira ulianza kuchezwa kabla ya kipenga. Ukienda kwenye hoteli za kitalii za

Wazanzibari ziko nyingi sana, ah! Mbona wanavyoongea sio sauti ya Kizanzibar hii? Kwa hiyo, mpira kwenye hoteli zetu za Kizanzibari ulichezwa kabla ya kipenga. Sasa Serikali kipenga ni leo, turudi tujipange, tukaguliwe ndio tuanze kucheza mpira. Hili ni angalizo kwa Serikali na nitaomba Serikali wakati Waziri anapotoa majumuisho awaelekeze Watanzania kwamba hili litasahihishwaje?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Sheria ndio inaanza leo tukiridhia sisi, tuna tatizo. Watanzania tusikubali kuwa warahisi, tuna tatizo. Watoto wetu hawaajiriwi! Ndio, tutakuwa tuna Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania; sasa basi, huu mchezo uchezwe sawasawa kwamba kijana wa Kitanzania akiwa na *qualification,* akienda Kenya aajiriwe, Uganda aajiriwe, Rwanda aajiriwe.

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo kwa Serikali, isije ikawa mpira unachezewa kwetu tu, kwa sababu ya kitu ambacho mimi nakikataa eti ooh! Watanzania hawajui Kiingereza, sio kweli.

Vijana wetu Watanzania wanajua Kiingereza sana, tena Kiingereza cha Watanzania hawa vijana wetu wa sasa hutajua ni Mpare, hutajua ni Mgogo, wanaongea Kiingereza cha *oxford,* Kiingereza cha *Cambridge,* lakini unaambiwa ooh, hapana, hawajui Kiingereza. Mimi naomba Serikali iliangalie hili vizuri. Vijana wa Kitanzania wanajua Kiingereza vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la ajira, *free movement of labour,* jamani Watanzania Serikali tusipokuwa makini vijana wetu wanao-*graduate* kwenye vyuo vikuu vyetu watakosa kazi kwa sababu sisi tutakuwa tunaajiri wenzetu. Hapa itakuwa ni kazi, tutarudi kwenye Bunge hili hili tutaanza tena kushikana mashati na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke kwenye hili la ajira. Hata kama ardhi haizungumzwi sana, naomba nizungumzie ardhi ya nchi. Ardhi ya nchi ndio nchi, ardhi yetu ndio mali yetu na niseme ukweli maana yake hakuna haja ya kusema uongo au kuzungukazunguka katika nchi tano za Afrika Mashariki; Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya, Tanzania, wenzetu wote wanne wana matatizo ya ardhi, kama ni watu wasio na matatizo ya ardhi ni Tanzania, naisihi sana Serikali, ardhi ya Tanzania ni ya Watanzania. Sasa hivi naiomba Serikali, leo tukipiga kipenga hapa iende ikatusaidie na ije itujibu, ikafanye sensa mipakani.

Mheshimiwa Spika, Serikali iende ikafanye sensa Mikoa ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Arusha, Kilimanjaro,Tanga. Kama kuna ardhi yetu ilishanunuliwa tunaomba irudishwe, maana yake najua wenzetu wamenunua ardhi kinyemela, mmeshanielewa, ardhi imenunuliwa kinyemela tunaomba kipenga ni leo, mtufanyie sensa mtujibu.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye vivutio, hizi nchi tano zote zina vivutio, nimekwenda Rwanda kuona vivutio vyao tena vizuri, nimekwenda Burundi kuona

vivutio vyao, nimekwenda Uganda kuona vivutio vingi. Nimekwenda Kenya wana vivutio vingi sana na sisi Tanzania tuna vya kwetu, kila nchi ibaki na vivutio vyake, kila nchi ijinadi nje na vivutio vyake, iwe ni marufuku kwa hizi nchi tano kujinadi nje kwa vivutio vya mwenziwe na Mheshimiwa Waziri katika hili ukawe mkali kwa wenzio. Hakuna jambo linalowaudhi Watanzania kama nchi nyingine inapouzungumza Mlima Kilimanjaro nje kama ni wake.

Mheshimiwa Spika, nyumba yangu iko jirani na ya kwako, lakini siwezi kusema kwa sababu nikiwa nimesimama dirishani kwenye nyumba yangu naiona nyumba yako wewe niseme nyumba ya Spika ni ya kwangu, hapana. Mlima Kilimanjaro nasema kupitia Bunge hili ulimwengu mzima ujue Mlima Kilimanjaro upo Tanzania, Mlima Kilimanjaro ni wa Watanzania, wenye stahili ya kujinadi kwa Mlima Kilimanjaro ni Watanzania, yeyote atakayefanya hivyo ambaye sio Mtanzania atakuwa hatutendei haki na hapo ndio itakuwa mwanzo wa chokochoko.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro uko Mkoa wa Kilimanjaro ambako na Jimbo la Same Mashariki lipo. Ninaomba sisi watano tutaridhia itifaki hii, lakini Serikali iwe makini sana, namwomba Mheshimiwa Waziri nimemsifu kwa sababu kweli anafanya kazi, nenda kafanye kazi kwa Uzalendo maana yake maana ya shirikisho ni kuhakikisha na sisi tunaboreka kiuchumi. Hii kitaalam inaitwa ni *Regional Economic Integration,* kwamba kila mtu aweze kujenga nchi yake kiuchumi, lakini Watanzania tusingependa tutumiwe na wenzetu. Tucheze huu mpira sawa, lakini kabla sijamalizia kwa msisitizo kwa Serikali narudi kwenye ajira, leo ndio tunaridhia Itifaki hii na leo baada ya hapa ndio turudi kwenye mstari, kama kuna watu waliajiriwa kinyemela warudi kwao, tuanze upya. Kwa sababu hatuwezi kuridhia kitu kumbe kuna watu wana miaka mitano kwenye kazi, hapana.

Mheshimiwa Spika, mpira unachezwa baada ya kipenga, kipenga ni leo, naomba niseme naunga mkono hoja, lakini mpira unaanza leo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Namwita sasa Mheshimiwa Kabwe Zitto atafuatiwa na Mheshimiwa Raynald Mrope wakati huo Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge ajiandae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii na pia kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii ambayo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya kikatiba ya kuweza kuridhia Itifaki ya soko la pamoja ya Afrika Mashariki, Waheshimiwa Wabunge tutakumbuka kwamba Bunge la nane liliridhia itifaki ya Umoja wa Forodha na sasa hivi tuko kwenye mwaka wa tano wa utekelezaji wa Itifaki wa Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, masuala ya umoja katika Bara la Afrika sio mambo mapya, ni mambo ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu na mtakumbuka kwamba kulikuwa kuna ugomvi mkubwa kati ya Mwalimu Nyerere na Rais Nkhurumah katika mkutano wa *Cairo* wa kuanzishwa kwa *Organisation of African Unit* kwa sababu kulikuwa kuna makundi,

kuna kundi ambalo lilikuwa linamuunga Rais Nkhurumah kwa kutaka umoja utangazwe mara moja kwa haraka, kuna kundi lilikuwa linamuunga Mwalimu Nyerere na wenzake ambao walikuwa wanataka tuanze na Mikoa kwanza ya kikanda na baadaye tuweze kwenda kwenye umoja wa Bara la Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini matokeo yake bado mpaka leo Bara la Afrika lina *struggle* kwa ajili ya umoja, kuna *The African Union* lakini bado haijaweza kufikia yale matakwa ambayo waasisi wetu wa Bara la Afrika waliyataka na sasa hivi tuko kwenye hatua hii ya kuanza kuungana kiuchumi. Siku moja nilisoma kwenye makala moja ya magazeti yetu hapa, mwandishi mmoja maarufu sana Jenerali Ulimwengu aliandika wakati wa mjadala kuhusu Serikali ya Tanganyika katika Bunge la mwaka 2003. Kundi la Wabunge hamsini na tano waliokuwa wanataka Serikali ya Tanganyika walikwenda nyumbani kwa Mwalimu Nyerere kuweza kutaka awaunge mkono na moja ya hoja waliyotumia ni kwamba hawa wenzetu Wazanzibari kwanza hata tamaduni zetu ni tofauti, Mwalimu akamuuliza aliyekuwa kiongozi wa msafara huo wakati huo Mbunge wa Karatu Ndugu Quorro, kwamba kati ya watu wa Tanga na Pemba na watu wa Manyara, Arusha na Tanga ni wapi ambao wana mahusiano ya karibu zaidi ya kitamaduni, lile kundi likashindwa kujibu kwa sababu ni dhahiri kabisa kwamba kati ya Tanga na Pemba wana mahusiano zaidi kuliko Arusha na Tanga.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo mipaka tunayoizungumza sasa ni mipaka *artificial*. Ni mipaka ambayo haikutengenezwa na sisi Waafrika, ni mipaka ambayo imetengenezwa na wageni, wakoloni kwa ajili ya kutawala, kwa hiyo, hatua ambazo tunazichukua sasa hivi, tuna-*correct historical mistakes* ambazo zilitokea na ndio maana kwa njia hii naunga mkono hatua yeyote ile ambayo itatufanya tuwe karibu zaidi, ambayo itatufanya tushirikiane zaidi, ambayo itatufanya tuweze kuwa na umoja imara zaidi ndani ya Bara letu la Afrika na ndani ya eneo la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tofauti lazima ziendelee kuwepo, tofauti za kimaendeleo lazima ziendelee kuwepo, leo Kigoma haipo sawa kimaendeleo na Kilimanjaro na ni nchi moja, tumepata uhuru pamoja, tunakaa pamoja humu Bungeni, lazima tofauti ziendelee kuwepo. Wenzetu nchi zingine walichukua *route* tofauti na sisi, lakini kuna nchi ambazo ziliingia kwenye matatizo mara baada ya uhuru wao. Waganda walipinduana wakapata *dictator* mbaya sana Iddi Amini, tukapigana nao vita, tukawashinda vita, wakaenda kupigana msituni, mwaka 1986 wakati Rais Museveni anachukua Uganda chini ya NRM, Uganda ilikuwa imekwisha kabisa. Leo Uganda ya mwaka 1986 sio Uganda ya sasa, leo Uganda wanatoa wasomi zaidi ya vyuo vikuu kuliko Tanzania, sasa kutokujiandaa kwetu, kutokujipanga kwetu kusiwe sababu ya kuchelewesha ushirikiano zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni lazima kuchukua tahadhari, ni lazima kujipanga zaidi lakini ni lazima tuhakikishe kwamba sisi ndio tunaochukua *a leading role*. Siku moja hapa wakati Waziri Mkuu anajibu maswali ya papo kwa papo, alionesha masikitiko yake ya kwa nini nchi kubwa kama Tanzania, nchi tajiri kama Tanzania inalinganishwa na vinchi vidogo vidogo kama Namibia, Botswana na kadhalika na inasikitisha zaidi. Nchi kubwa kama Tanzania, nchi tajiri kama Tanzania ambayo ndio ilikuwa inaongoza katika diplomasia ya Kimataifa sasa hivi tunaongoza kwa woga, tunawaogopa jirani zetu kupita

kiasi, kiasi kwamba inafikia hata wakati unaogopa Rwanda, Burundi kuingia kwenye Afrika Mashariki, tunasema kwamba hawa watu watatuambukiza vita, hatufikirii kwamba tutawaambukiza amani, tunafikiria kwamba wao watatuambukiza vita, ni hivyo hivyo katika masuala ya ajira, mzungumzaji aliyepita amezungumza vizuri sana. Lakini ni lazima tufikirie ni jinsi gani ambavyo sisi tutachukua ajira zaidi kwa wenzetu kuliko kufikiria tutakavyonyanganywa ajira zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni suala la kukaa na kufikiria na kuwa kama Taifa. Juzi kwenye semina nilizungumza tuwe makini, tusijikute tunakuwa ni Uingereza ndani ya Jumuiya ya Ulaya. Nafasi yetu sisi kwenye Afrika Mashariki tunapaswa kuwa ni Ujerumani na Ufaransa ndani ya Jumuiya ya Ulaya, kwamba sisi ndio tutoe *leadership* kwenye *region* na sio sisi tuwafuate wenzetu kwenye *region*, ndio hali ambayo ipo sasa hivi. Kutokana na mazungumzo ya Viongozi, sisi wanasiasa na *opinion makers* mbalimbali kwa sababu sasa hivi kwenye masuala ya Afrika Mashariki huwezi kutofautisha lugha ya mwanasiasa na lugha ya mwananchi wa kawaida Kariakoo; wote tunaongea lugha moja tu kuwaogopa Wakenya, wote.

Mheshimiwa Spika, hakuna ambaye anawaonesha wenzake, hapana twende hivi na moja ya jukumu kubwa la kiongozi, jukumu kubwa sana ni kiongozi kuwaonesha wananchi kwamba huku huku ndiko tunakotaka kufika hata kama wale wananchi hawako tayari kufika kule.

Kiongozi naye anatakiwa kuwaonyesha huku ndiko tunakotaka kufika. Sio kiongozi awafuate wale wananchi wanakotaka kwenda. Sasa hii ni lazima tuwe makini sana, hata lugha ambazo tunazitoa. Hata jinsi ambavyo tunavyoona kwamba labda tunaweza ku-*loose* katika soko hili la pamoja, lazima tuwe makini sana kama Viongozi katika lugha tunazozitumia.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano. Mwaka 2005 baada ya kuridhia itifaki ya Umoja wa Forodha (*customs union*), Tanzania ilikuwa na urari hasi wa biashara na nchi zingine, mwaka 2005, urari wetu wa biashara kati ya Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki ulikuwa ni *negative thirty-four billion shillings*, fedha za Kitanzania. Bilioni thelathini na nne hasi, mwaka 2005. Wenzetu wakaenda waka-*negotiate* vizuri tu, tukakubaliana jinsi gani ambavyo sisi tutauza bidhaa zetu bila kodi, wao watauza kwa kodi huku kwetu. Miaka mitatu baadaye mwaka 2008, urari wa biashara wa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki umefikia 70.3 *billion Tanzanian shillings*, tumetoka kwenye *negative thirty-four* tukaiziba ile *negative thirty-four*, halafu tukaongeza *seventy* zaidi mbele.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kwamba tukiamua na pakiwa na *incentives* tunaweza. Sisi kwa kweli tunaweza kuliko wenzetu. Sisi tumepigana vita tukashinda. Tumempiga Iddi Amini. Sisi tumeshiriki kwenye ukombozi wa Kusini mwa Afrika tukawapiga Wareno, tukawapiga Makaburu, sisi *in the region* ndiyo tunapaswa kama nilivyosema hapo awali kutoa *leadership,* haya mambo ya viongozi kunung’unikanung’unika, kulalamika, tunaihamisha kwa wananchi na wananchi

wenyewe wanajiona wanyonge. Wananchi na wenyewe wanajiona kwamba hatuwezi wakati tunaweza. Lazima tubadilike.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tubadilike, masuala ya tofauti zetu nimetoa mfano wa maendeleo, kwa mfano, Mkoa wangu ninaotoka na Mkoa wa Kilimanjaro. Lakini naweza nikatoa mfano, ajira za utalii Zanzibar, leo tunalalamika kwamba Wakenya kwenye mahoteli yetu, ni kweli kabisa. Ni kweli waliandaa mapema, walikuwa na chuo cha utalii, sisi ndiyo kwanza tunaanzisha chuo cha utalii na naamini kama tukiwafundisha vijana wetu vizuri zaidi na sisi tutaweza kushiriki zaidi kwa sababu Watanzania wanajifunza kwa haraka sana. Lakini leo ukienda ukiwauliza Wazanzibar, watu wanaofanya kazi kwenye mahoteli Zanzibar, kati ya Wazanzibar na Watanzania Bara, Watanzania Bara ni wengi. Hizi ni tofauti za kawaida kabisa kwenye uchumi. Ni kujiandaa jinsi gani ambavyo tunaweza tukazi-*correct.*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la jinsi gani ambavyo Kamisheni ile ambayo sasa hivi ni Sekretarieti ya Afrika Mashariki inapaswa kuimarishwa. Mfumo tunaoingia sasa majukumu ya Sekretarieti yatakuwa ni makubwa sana. Kwa sababu mfumo ambao tumetoka ni wa uhuru wa bidhaa tu ku-*cross boarders.* Mfumo ambao tunakwenda watu wata-*cross boarders.* Kwenye Sheria, Mkataba wa Afrika Mashariki kuna Kanuni ya kupinga ubaguzi *non-discrimination principle* kwamba Mkenya na Mtanzania ndani ya Kenya lazima wawe na fursa sawa za ajira kutokana na zile *schedule* za makubaliano miongoni mwa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ya Kenya haitaweza kumnyima ajira Mtanzania kwa vigezo vya kwamba huyu ni Mtanzania na kuna kesi nyingi sana kwa wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya ambazo zimetokea, kuna njia nyingi sana ambazo watu walikuwa wanajaribu kufanya *discrimination* miongoni mwa makampuni na kadhalika na Mahakama ya Jumuiya ya Ulaya *European on Court of Justice* ikawa imetengua yale maamuzi ya zile Serikali katika ku-*discriminate* watu.

Sasa katika hali kama hii Mahakama ya Afrika Mashariki itakuwa na kesi nyingi sana hivi sasa. Kwa sababu kwa vyovyote vile lazima kutakuwa na mwingiliano mkubwa sana wa kibiashara. Bunge la Afrika Mashariki litatunga Sheria nyingi sana. Kwa kupitisha Itifaki hii kuna majukumu ya kiutungaji Sheria ambayo sasa tunayahamisha, tunapeleka Arusha. Tunayaondoa Dodoma, kama jinsi tulivyofanya wakati wa Umoja wa Forodha, majukumu yote ya kikodi za forodha tuliyaondoa. Sasa hivi kuna baadhi ya majukumu ya kiajira, kuna baadhi ya majukumu ya *movement of capital.* Kuna baadhi ya majukumu ya *right of establishment* kwa makampuni tunayapeleka Arusha. Kwa hiyo kuna sheria mbalimbali ambazo itabidi tuzirekebishe, kwa maana hii ni lazima kuimarisha Sekretarieti pale Arusha.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu tujaribu kuangalia, kuna mifano mingi, lakini tunaweza kuangalia jinsi ambavyo tunaweza kuwa na Kamisheni sasa. Na tukachukua Watanzania *bright, the cream* ya nchi tukawapeleka ku-*serve* pale Arusha. Kwa sababu nako kuna tatizo, haya malakamiko ya ajira na kadhalika, pale Sekretarieti wanaajiriwa mpaka wafagiaji ni Wakenya na kadhalika, ni malalamiko ambayo yapo na

*real* ambayo ni lazima kuyafanyia kazi. Nafahamu kwamba tunaye Katibu Mkuu hivi sasa ambaye anafanya kazi yake vizuri sana, lakini ni muhimu sana kuhakikisha kwamba pamoja na Maofisa wengine wa Jumuiya, tunapeleka Watanzania ambao wana uwezo sana. Tusiingie mkumbo wa nchi zingine, kwamba unawapeleka watu ambao umegombana nao kisiasa nchini, ndiyo unawapeleka kwenye Jumuiya za Kimataifa. Ni lazima tuchukue watu ambao ni *bright*, tuwa-*train* vizuri, waielewe nchi, wapate dozi ya uzalendo, tuwapeleke kule kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maamuzi yoyote yanayofanyika pale, yanazingatia maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkuu wa Upinzani ameongea mambo yote ya ki-*principle* ambayo sisi watu Kambi ya Upinzani tumekubaliana na tayari yameunga mkono Azimio hili na pia napenda kuunga mkono Azimio hili, twende mbele tujiandae, tujipange, tuwe *the lead* ndani ya *region.* Tusiwe nyuma, tusiwe walalamishi, tusiwe wanung'unikaji, tu-*provide leadership* kama jinsi Tanzania ilivyokuwa miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa mchango wako huo. Namwita sasa Mheshimiwa Raynald Mrope, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Benelith Mahenge. Baada ya hapo ajiandae Mheshimiwa James Lembeli.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia japo kidogo hili Azimio lililo mbele yetu. Kwanza nazidi kuendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Masasi kwa kuniunga mkono na kwa kila njia wananifanya niwe najiona kabisa nazungumza kwa niaba yao na hivyo naomba siku za usoni tuendelee kushirikiana ili tuweze kukamilisha yale tunayotaka kuyatekeleza katika Jimbo letu. Naomba sasa nimpe pongezi za dhati ndugu yangu Waziri Mheshimiwa Kamala pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed kwa kulileta Azimio hili au Itifaki hii mbele yetu ili tuweze kuridhia.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli nakubaliana na wenzangu hawa ndugu zetu tuliowapeleka kule wametufanyia kazi nzuri sana na sasa hivi mwelekeo unaendelea kuwa nzuri na wenzetu katika Afrika Mashariki wanazidi kutuelewa. Toka mwanzo nataka kusema kwamba naiunga mkono hoja hii na hasa kwa sababu imeletwa na Serikali ya CCM, Chama ambacho naamini kabisa kinaendesha nchi hii kwa utaratibu mzuri na sisi wote tuna imani nacho.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kuunga kwangu mkono naunga zaidi mkono kwa heshima ya Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ndiye ametia sahihi kwamba Jumuiya izidi kuendelea katika hatua mbalimbali na hasa katika mambo haya yanayofuata maazimio ya Itifaki nayo tuweze kuyajadili na kuona jinsi gani Tanzania itanufaika.

Mheshimiwa Spika, lakini ni haki yetu sisi wananchi na hasa sisi wawakilishi wa wananchi, ni haki yetu kusema pale tunapoona mambo hayaendi vizuri. Mpaka sasa hivi katika kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeona wapi tulikotoka na huko tulikotoka sisi Watanzania tuliumia na katika kuumia leo hii hata tukiona mvua tunafikiri ni nyoka. Wote mnakumbuka mwaka 77 yaliyotokea, ilipovunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kulikuwa na shughuli kubwa ya uanzishaji wa CCM kwa mara ya kwanza kabisa pale Arusha. Ghafla Jumuiya ilikufa, wageni wetu wanaotoka nje walikwama, Nairobi hawakuweza kufika Arusha na kukawa na sokomoko. Shughuli zote za usafiri zilikuwa ngumu sana sana kwa Tanzania. Hiyo ni *experience* yetu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, wengi tulifjifunza kutoka pale kwamba aah! Kuna baadhi ya mambo kama tukiyanyamazia, basi mwisho wake tutakuja kulia. Tulikuwa na Shirika letu la Afrika ya Mashariki la Ndege lilikuwa linafanya kazi vizuri sana lakini lilikufa wakati ule na hasa lilikufa wakati mbaya kwetu sisi Watanzania wakati ambapo dunia nzima ilikuwa inatazama jinsi gani hawa wataungana. Ile dosari kwa bahati mbaya, iliwekwa zaidi na wenzetu wa Kenya, hilo hatuwezi kusahau na tunavyozidi kuendelea siyo kwamba tunalalamika lakini tunakumbushana haya mambo ili yasirudie. Yasije yakarudia, kwa sababu tunataka wote tuwe na maslahi safi kabisa, tuendelee vizuri katika nchi zetu, katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuna vitendo vingi vinavyodhoofisha, hivyo nilivyovitaja vilikuwa vya kisiasa zaidi. Lakini kwenye upande wa uchumi nako tusipoangalia hatua hii ya Itifaki itakuja kutuumiza zaidi Watanzania. Kuna mambo mengi tu, nitatoa mifano michache, suala la utalii, ambalo tayari wenzangu wameshalizungumzia kwamba, kwa namna moja au nyingine wenzetu wanalichukulia vibaya na ubaya huo unakuja kuiumiza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rasilimali zetu, nyote mnajua leo hii *Tanzanite* huko ulimwenguni, huko majuu wanafikiri inatoka Kenya. Kwa nini? Kwa sababu wenzetu wametuzidi ujanja, wanachukua mali yetu na inaonekana ni mali yao na wanapata faida kubwa kwa kufanya biashara na ile mali yetu. Sisi wenyewe tumekaa kimya. Lakini kwa ujirani mwema kilichotakiwa kufanyika wenzetu wa Kenya nao angalau wangesema na kuwaambia watu wao, ndiyo ingawa ni biashara, lakini si halali kwenda kumwibia jirani yako.

Hivi Serikali ya Kenya ilikuwa na sababu gani kusema kwamba kama ni *Tanzanite* basi haiwezi kwenda nchi za nje kupitia Kenya. Wao wenzetu kama Kiserikali wangepiga marufuku. Unafikiri magendo haya yangeendelea? Lakini hii inatuonyesha kwamba hawa wenzetu ni wajanja, lakini pia wanatiwa nguvu na Serikali yao. Kwa hiyo, ni lazima tuseme kwamba mambo haya hayafai kwa siku za usoni wakati tunapofungua mipaka yetu. Haya ni mambo ambayo tusipoangalia yatakuja kuvunja huo umoja wetu hata baadaye tukawa na sokomoko bila sababu.

Wakati huo huo ndio tunaweza kwenda tukawa tunatoa mifano mbalimbali na kwa mfano huu wa juzi wa Doha, ni mfano mbaya ambapo wenzetu wa Kenya kwa

makusudi kabisa walipiga kampeni sehemu mbalimbali kwamba Tanzania isiuze pembe zake za ndovu. Sasa wakati tukitoka katika Jumuiya moja, badala ya wenzetu kutuunga mkono, wenzetu hawa wakawa wanatupiga vita. Ndiyo tunaweza kusema kwamba makosa yalikuwa yetu, labda hatukupiga kampeni ya kutosha. Lakini pale unavyoona jirani yako kwa makusudi kabisa, hata hagumii kwamba bwana kuna mwizi, nyumbani kwako ananyemelea, jamani, umoja huu utakuwa ni umoja wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima tuwaseme, tuwaseme kwamba vitendo vya namna hii kwa vyovyote vile vitakuja kuvunja huu umoja wetu. Tumeona ni kitu gani kilitokea hapo awali, lakini kwa sasa hivi tunawajibika kuwaambia kwamba isifike mahali ambapo Tanzania nayo itawajibika nayo kujibu mapigo. Tukijibu sisi mapigo, naamini kabisa wenzetu wa Kenya ndiyo watakaoumia zaidi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tukijibu mapigo kwenye mambo ya utalii, utalii wa Kenya utakufa. Kwa sababu wanategemea zaidi Tanzania. Sasa ni lazima Bunge linavyoona vitendo vya namna hii ambavyo hatimaye vinaweza kuvunja ile nia yetu ya kuungana ni lazima tuviseme wala tusiogope, kwa sababu wanaofanya vile ni viongozi. Wananchi wao wana nia nzuri kama walivyo wananchi wetu. Wananchi wetu wanaposononeka kwa nini Kenya inatufanyia hivyo, sisi ni juu yetu kuwaambia wenzetu namna hii haifai na kwa kweli tuwaambie kwa sauti kubwa kwamba hii ni mara ya mwisho kuona vitendo vibaya namna hii dhidi ya nchi yetu. Siku zijazo na sisi tutachukua hatua ambayo itawaumiza wao wenzetu. Hili naona nilieleze vizuri kabisa, maana yake ujirani wowote ni kufaana.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema kufa ni kufaana. Sasa kama unaona jirani yako hakufai, kwa nini uwe naye. Ndiyo ujumbe wangu kwamba, jamani wenzetu waelewe sisi wenzao tunapokasirishwa tunakasirishwa kwa ajili ya msingi hasa na kwamba tunawaambia wasirudie mambo hayo ili tuweze kuwa wamoja zaidi. Nakubaliana na wenzangu kwamba nchi yetu ijitahidi fursa sasa ndiyo zinazidi kupanuka, ijitahidi kwa wepesi katika kuchangamkia biashara hizi mbalimbali. Najua kutakuwa na ugumu kwa sababu ya miundombinu yetu sisi haijakamilika lakini twende hivyo hivyo. Lakini sisi kama viongozi wa wananchi wetu ni lazima kila wakati tuhakikishe kwamba tunawasaidia wananchi wetu ili nao waweze kunufaika katika hii Jumuiya kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema toka mwanzo kwamba naiunga hoja hii mkono na hasa zaidi kwa sababu Serikali yetu imeifanyia kazi, tunasema tuiunge mkono lakini tahadhari yangu ni ile tu kwamba wakati wowote vinapotokea vitendo ambavyo vitadhoofisha na hasa vitendo hivyo vitakavyoumiza nchi yetu, tusisitize kuwaeleza wenzetu jinsi tunavyosikitishwa na vitendo hivyo na wenzetu watuelewe ili wakibadilika au wakijisahihisha basi huo ndiyo utakuwa umoja wetu katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mwenyekiti kwa kunisikiliza na wananchi pia kwa kunisikiliza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Raynald Mrope. Ni zamu sasa ya Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. Atafuatiwa na Mheshimiwa James Lembeli, wakati huo Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu ajiandae.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ili nami niwe mmoja wa wachangiaji katika hii hoja muhimu ya soko la pamoja la Afrika ya Mashariki. Kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kuleta Itifaki hii na niwakumbushe wenzangu na Watanzania wengine kwamba ni sisi wenyewe Watanzania tulikubali kuanzishwa kwa Afrika Mashariki. Ni sisi wenyewe tulishuhudia kitendo cha Marais wa nchi hizi tano, tarehe 20 Novemba 2009 wakisaini Itifaki hii na leo ni kazi yetu sisi kuweza kuridhia. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba hatuwezi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, ombi langu hatuwezi kurudi nyuma, kinachotakiwa ni kusonga mbele. Kinachotakiwa ni kuangalia mikakati ya kusonga mbele na mikakati ya namna ya kushiriki kikamilifu katika fursa ambazo zinaelezwa kwenye itifaki hii ya soko la pamoja la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Spika, kuna kitu cha pekee ambacho kinafanyika ambacho tunafanya kama historia, unaporuhusu wananchi wa nchi hizi tano kutoka nchi kwenda nchi kwenda kufanya kazi, kufanya biashara, kutoa huduma mbalimbali, kufanya uwekezaji, kimsingi unaleta historia kwa sababu ni kama unafuta ile mipaka iliyokuwa imewekwa na wakoloni. Hii ni kukua sana kwa demokrasia kwa nchi zetu hizi tano ambazo leo zinaleta hii itifaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Tanzania tunatakiwa tuchukulie hii itifaki kwamba ni changamoto kwa nchi yetu, ni changamoto kwa Serikali, ni changamoto hasa kwa wajasiriamali wetu ambao wamekuwa wakizalisha bidhaa mbalimbali ili kuweza kukidhi fursa ambazo zimo kwenye Soko hili la Pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa, ni kuyataja baadhi ya mambo ambayo inabidi tujiandae kama Watanzania, tujiandae kwa ajili ya kuyakabili; la kwanza ukisharuhusu bidhaa mbalimbali kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine, ukisharuhusu uwekezaji mbalimbali kutoka nchi moja kwenda nyingine, ni wazi kwamba biashara zetu, baadhi ya makampuni na hasa hizi kampuni za wajasiriamali, iko hatari ya kufungwa. Kwa sababu ya ubora wa bidhaa ambao wanatoa kama ukiwa chini, basi bidhaa za kutoka nchi za jirani, zikiwa bora basi zitachukua soko la Tanzania. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wajasiriamali wetu, wanatoa vitu vyenye viwango ambavyo vitakidhi Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ili viweze kutumika ndani na viweze kwenda katika nchi hizo za karibu.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ni la hatari linaweza likatokea tusipokuwa waangalifu kujiandaa, ni suala la ajira kama walivyoongea wenzangu na hasa ajira kwa vijana. Ukisharuhusu *a movement* ya watu kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine kufanya kazi, ni wazi kwamba vijana wetu wanatakiwa kuwa na *competence* ambazo zitakwenda kwenye soko la ushindani na wanaweza wakashinda kupata hizo nafasi za kazi. Kama hatutaweza kuwaandaa vizuri, hatutaweza kuwaweka vizuri, ndio sisi tutaonekana kwamba tayari ni soko la ajira kwa nchi nyingine kama inavyojitokeza sasa

hivi kwenye sekta ya utalii ambayo sehemu kubwa ni wenzetu majirani ndio wamevamia soko hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu ni kwamba tunajua kwamba nchi kama Kenya wamewekeza Tanzania kwa kiwango cha bilioni 160, kwa taarifa za hivi karibuni. Ni wazi kwamba uwekezaji wa nchi hizi za karibu, unaweza ukaanza kushuka kwa sababu wawekezaji hawa wataona hamna sababu ya kuja kuwekeza Tanzania, kwa sababu akizalisha kwenye nchi yake anakuta kwamba anaweza akazisambaza zile bidhaa kwenye nchi za jirani. Kwa hiyo, pengine na hii tuanze kuingalia kuhusu uwekezaji na tuwe na mikakati mingine ya kutafuta wawekezaji wengine, sio katika nchi hizi tano bali na nchi nyingine za nje. Kwa sababu upo uwezekano kwamba hawa wawekezaji wakawa na *interest* ya kuzalisha nchini kwao halafu wakasambaza bidhaa kwa sababu zile *tariffs* zote tumeziondoa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni changamoto kubwa ambayo inajitokeza ni suala la kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu, kwa sababu kutakuwa na bidhaa zinatoka nchi za jirani, ni wazi kwamba hizo bidhaa baadhi zinaweza kuwa hazikidhi viwango. Kwa sababu kutakuwa na wafanyakazi wanaotoka nchi moja kwenda nyingine, ni wazi kwamba kutakuwa na watu ambao pengine hata taarifa zao zinatakiwa kuangaliwa vizuri. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na usimamizi wa karibu sana kuangalia kama vitendo hivi vinadhibitiwa. Lakini vilevile kwa sababu itakuwa kutoka nchi kwenda nchi inaruhusiwa, basi ni wazi kwamba kutakuwa na makundi mengi ya wizi yatajitokeza kama kuiba magari na vitu vingine ambavyo yanaweza yakapeleka katika nchi nyingine. Kwa hiyo, tunaamini kwamba Mheshimiwa Waziri, atatupatia taarifa baadaye jinsi walivyojiandaa kudhibiti na kusimamia vitendo vya uhalifu ambavyo vinaweza vikatokea wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufahamu kwamba itakuwa ni vigumu sana kuitekeleza itifaki hii mahali ambapo hapana amani na usalama. Kwa hiyo, amani na usalama ni kitu cha msingi ili kiweze kuwepo.

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka kusema kwamba ni muhimu tukaunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Habari asubuhi ya kukuza matumizi ya Kiswahili. Tuhakikishe kwamba katika sehemu zote za kazi, hasa kwenye Mikoa, kwenye Wilaya na hasa kwenye sekta za watu binafsi kwamba matumizi ya Kiswahili kwenye zile kazi yanakuwa ni makubwa zaidi ili kulinda ajira za vijana wetu kwamba eneo kubwa watumie Kiswahili kutoa nafasi kwa Watanzania kuajiriwa kwa sababu wanakuwa wanaijua lugha yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa mapendekezo yafutayo:-

Pendekezo la kwanza ni namna gani Serikali inaweza ikaweka mkakati wa kuingia kwenye soko hili la pamoja. La kwanza kabisa ambalo ni mkakati, ni lazima tusonge mbele na ili tusonge mbele ni lazima tuwekeze kwenye elimu, ni lazima tuwekeze kwenye sayansi na teknolojia ili tuweze kushindana vizuri. Kwa sababu leo hii unakuta tayari tumeruhusu fani kama uhandisi, udaktari, upimaji ramani kwamba ni

mojawapo ya fani ambazo wenzetu wanaweza wakaja wakaomba kazi huku Tanzania. Lakini nadhani tukijiandaa vizuri, tunaweza kuwaandaa vijana wetu wakaajiriwa ndani ya nchi yetu, lakini wakawa na zile *skills* za kwenda kuajiriwa katika nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani hili ni la msingi na kama pengine Serikali sasa iwe na mfuko wa kuhakikisha kwamba inawa-*coach* vijana na tuna-*hear mark* nafasi mbalimbali za Afrika Mashariki ambazo tunadhani kwamba vijana wetu wanaweza wakazichukua ama ni Uganda ama ni Kenya ama ni Rwanda ama ni Burundi. Kwa hiyo, tunawa-*coach* namna ya kwenda kuzichukua zile nafasi, tunakwenda kwa pamoja na tusiwaachie vijana peke yao. Kwa hiyo, mfuko huu ungeweza kutumika kuwaandaa na kuwa-*train* ili waweze kuchukua zile nafasi kubwa ambazo ziko katika nchi nyingine. Tukiwaachia peke yao watakuwa wanashindwa, na tutakuwa tunasema kwamba hawajui Kiingereza kumbe hatukuwaandaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ninapendekeza ni kuwa tujenge uwezo wa Shirika la Viwango la Taifa (*Tanzania Bureau of Standards(TBS)* na Mashirika mengine ambayo yanaangalia ubora wa bidhaa zinazoingia nchini ili waweze kudhibiti uharibifu utakaojitokeza kwa maana ya kwamba baadhi ya nchi zitaleta bidhaa ambazo ni mbovu. Lakini vilevile ukiwajengea uwezo *TBS* watasaidia kutoa elimu kwa wajasiriamali za kutoa bidhaa ambazo ni bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu ni kwamba imeonesha wazi ilipokuja hii itifaki Wabunge wengi walikuwa hawana taarifa za kutosha. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwa unyeti wa suala la Afrika Mashariki, kwa unyeti wa masuala yote yanayojadiliwa kwenye Afrika Mashariki, ni vizuri Wizara husika ikawa inatoa taarifa kwenye Bunge, ikiwezekana kila tunapokutana na kama haiwezi kufanya vile, basi ipitie kwenye Kamati ya Bunge inayohusika kwenye hiyo Wizara, ili kuwa-*update* Wabunge, mambo yanayotokea kwenye suala zima la Afrika Mashariki na wao waweze kuchangia na kutoa maoni kabla halijafikia mahala ambapo linaleta mabishano makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ninadhani ni la msingi sana na ninaungana na Serikali, ni msimamo kuhusu suala la ardhi. Tunafahamu wote kuwa sisi tuna ardhi kubwa, wenzetu ardhi yao ni ndogo, kwa hiyo, ni lazima tufanye kila mbinu kuhakikisha kwamba huu uhusiano wetu haugusi kabisa masuala ya ardhi na kwa sababu hata wananchi wetu wengi bado hawajui taratibu za kumiliki ardhi yao vizuri, kwa hiyo, tunaweza tukajikuta kwamba ardhi imeanza kutumika na wageni na baadaye wananchi wanakuwa ni watu wa kuhama hama na watu wa kuomba omba kwenye nchi yao wakati wao wana kila kitu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuunga mkono itifaki hii, na kwa kweli inahitajika sana kwa Watanzania. Kikubwa tusiogope, tuseme kwamba tunaweza, tusiseme kwamba hatuwezi; na tukisema tunaweza basi tuangalie ni namna gani ya kusonga mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Itifaki hii ni hatua mojawapo ya kuelekea katika Shirikisho la Afrika Mashariki. Ni hatua muhimu ambayo Bunge na wananchi wa Tanzania wanatakiwa kuitafakari kwa kina.

Mheshimiwa Spika, kufanya kosa sio kosa, kurudia kosa ni kosa baya sana. Wote tunafahamu Jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki ilivunjika mwaka 1977 kwa sababu ambazo tunazifahamu, hapakuwepo na kuaminiana na ndoa yoyote ambayo wanandoa hawaaminiani, haidumu, hata ukifanya nini, hauwezi kuamua kwenda kuoa kwa sababu unawajibu wa kuoa. Ni lazima mwenyewe ujiridhishe kwamba *partner* niliyempata ni mwaminifu na tunaweza kuishi naye milele. *(Makofi)*

Mimi nina wasiwasi na ndoa hii ambayo tunaelekea kuifunga. Siamini kwamba kwa dhati kabisa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaaminiana, zinapendana kwa dhati, wakati wa shida na wakati wa raha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa ni mfupi sana na sio kwamba mimi ni muoga kuongoza, lakini kuwa kiongozi sio basi tu wewe uongoze uwapeleke tu watu hata kama unawapeleka motoni. Sasa nafikiri kiongozi aliye imara na aliyechaguliwa na wananchi ni lazima apime anakowapeleka wananchi wake ni kwema au anawapeleka motoni?

Mheshimiwa Spika, zipo Jumuiya nyingi duniani kama hii ya kwetu ya Afrika Mashariki; wapo *EU, ECOWAS* na *SADC,* lakini wasiwasi wangu mimi unatokana na yale ambayo nimeyaona pale Doha. Tanzania kama nchi, ilikuwa na haki ya kupeleka hoja yake ya ku-*downlist* tembo kutoka *Appendix II* kwenda *Appendix I* na pia kuuza meno ya tembo ambayo yapo hapo Dar es Salaam na yanaigharimu Serikali zaidi ya shilingi 200,000,000 kila mwaka kuyahifadhi na yamekuwepo pale kwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Spika, ndugu yetu, jirani yetu, ametembea dunia nzima kuueleza ulimwengu kwamba hawa Watanzania wasiuze hayo meno yao ya tembo. Ndugu yetu Kenya, ame-*mobilise* nchi za Kiafrika hasa za Afrika ya Magharibi ambako yeye sio mwananchama kupinga hoja ya Tanzania ya kuuza meno ya tembo na baadhi ya nchi ambazo zilitupinga, tena kwa kejeli ni zile ambazo hazina hata tembo mmoja, wamemaliza tembo wao; Sieraleone, Liberia, Mali na hata ndugu zetu wa Rwanda, ambao hawana tembo lakini wana meno ya tembo kwenye maghala yao. Kwa hakika meno yale yanatoka Tanzania. Mimi ninajiuliza wakati tunaridhia Itifaki hii, tumezingatia kwa kiwango gani hulka na tabia kama hizi za nchi wanachama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeunga mkono moja kwa moja kama Serikali ingeshakemea kitendo hiki. Lakini tangu tumerudi, Serikali inafahamu na ilipeleka ujumbe mzito, Mawaziri watano mpaka Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alikuwepo pale ameona kilichotokea. Moja ya sababu ambayo wenzetu hawa walikuwa wanawaambia wajumbe kwamba hawa wakiuza hizo pembe za ndovu, pesa hizo watazitumia kwenye uchaguzi, mwaka huu wana uchaguzi; ni kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitasita kuunga mkono hii hoja na kama nitaiunga mkono basi nitaiunga kwa shingo upande. Kwa sababu hizi, kama hilo linaweza kutokea tena nje ya nchi, nje ya Afrika Mashariki, je, *within the Community?* Hivi kuna *mechanism* gani itakayowa-*control* hawa jamaa kutuma vijana wao kuja Tanzania kuchukua kazi za Watanzania? Tuna Chuo Kikuu hapa Dodoma, wanafunzi 40,000 tutawapeleka wapi? Wameshajaa sasa katika sekta ya utalii na katika maelezo ya Waziri hapa anasema nchi mwanachama kama kuna mwananchi anataka ku-*invest* katika *tourism* nje ya hifadhi, hoteli ya nyota tatu, ndani ya hifadhi hoteli ya nyota nne na kuendelea, wao wamejiandaa.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia kuanzia mwaka ujao mahoteli yote katika miji mikuu ya Tanzania yatakuwa ni ya Wakenya, kwa sababu Serikali yao imeshawaandaa na itawapa mikopo. Sisi hapa ni wimbo, hakuna utaratibu wa kuwawezesha Watanzania, sasa watashindana vipi katika soko hili la Afrika Mashariki, mimi naona kiza mbele ya safari. Na hii ndoa haitadumu kama haya mambo tutayachukua kisiasa siasa tu. Nimesikia ndugu yangu anasema tusiwe Uingereza ndani ya Afrika Mashariki, mimi nawapongeza Waingereza; ni wazalendo wanaipenda nchi yao. Huwezi kwenda mkumbo mkumbo tu, Uingereza ina historia. Sasa wa-*sacrifice pound* yao kwa sababu ya nini? Na sio Uingereza tu, Norway pia hawakusaini mkataba wa sarafu moja. Sasa na sisi Watanzania kila linalokuja tunaweka mkono, lakini ni mabingwa wa kusema jamani jambo hili tulifanye, haiwezekani, tufike mahali tukatae pale tunaapoona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kilichotokea Doha, Serikali ilitakiwa kukemea moja kwa moja haraka iwezekanavyo. Kwa sababu ni kitendo ambacho kilimdhalilisha hata Rais wa nchi yetu. Dakika za mwisho, ametuma ujumbe mzito, Mawaziri wanne, nendeni mkaweke nguvu. Waziri wa Kenya alikuwepo pale na ujumbe wa Tanzania ulimuona na kumueleza *concern* ya Rais, bado ameingia ndani ya ukumbi, anasema sera za Tanzania za uhifadhi ni mbovu. Sasa mimi najiuliza, ni nani mwenye sera mbovu, Kenya au Tanzania? Idadi ya tembo wa Tanzania imeongezeka kutoka 55,000 mpaka karibu 126,000 Kenya idadi ya tembo inazidi kwenda chini. Sasa ni yupi mwenye sera nzuri? Na sisi Watanzania tunakubali matusi ya rejareja kama hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilipenda niseme tu kwamba pamoja na kwamba Rais alitia saini makubaliano haya, bado Bunge hili lina haki kwa niaba ya wananchi. Mama yangu Kilango pale amesema asubuhi kwamba kipenga kimelia leo, kazi inaanza leo jino au kesho. Kwa sababu hawa jamaa hawajali cha kipenga, walishaanza siku nyingi na sisi tuko hapa hapa tunaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa shingo upande nitaiunga mkono hoja hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mtakuwa mmebaini kwamba orodha yangu inakwenda inabadilika, tunafuata mpangilio wa kujali makundi yote yaliyomo humu ndani, ndio sababu. Sasa namuita Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, sidhani kama

kutakuwa na muda aingie Mheshimiwa Pindi Chana, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, lakini tutaona. Mheshimiwa Ismail Jussa.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuwa mmoja katika wachangiaji wa hoja hii ya Azimio la Serikali la kutaka kuidhinisha Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mimi naomba nianze kwa kuungana na wenzangu kwa kusema kwamba tunapojadili mambo makubwa kama haya, kuchukua tahadhari au mkabala wa tahadhari *(cautious approach),* sio udhaifu. Kwa sababu tunatazama ni jinsi gani tutalinda maslahi ya nchi yetu na wananchi wetu ambao ndio tumekaa hapa ili kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili ni muhimu sana suala la kuwa na nia ya pamoja na kuhamiana vilevile katika wale ambao mnataka kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, sasa na mimi nataka niungane na wenzangu kusema kwamba tuna tatizo katika Tanzania, tatizo ambalo inawezekana limesababishwa na hoja nyingi nyingine za kihistoria, za hatua mbalimbali za kisiasa ambazo tumezipata na kiuchumi kwamba tunaonekana hatukujiandaa katika mambo mengi. Kwa hiyo, ndiyo matokeo yake tunakuwa tunahofia kuzidiwa nguvu na washirika wenzetu katika suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lakini Mheshimiwa Anne Kilango alivyokuwa anaanza kuchangia alizungumza vizuri zile hatua ambazo tunakusudia kuzipitia, hizi hatua tunazozipita hivi sasa hatimaye ndiyo zitakazotuekeleza katika *politically union.* Kwa sababu tunaambiwa lengo la haya hatimaye ni kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki la kisiasa. Sasa kwa sababu hiyo nilikuwa nadhani ni muhimu sana kuchukua tahadhari, sasa yamezungumzwa mambo naomba tuyazingatie.

Katika historia tunasema kwamba mipaka hii iliyowekwa iliwekwa na wakoloni kwa ajili ya kututawala, ni kweli lakini tusisahau kwamba wakati unaanzishwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika mwaka 1963 wakuu wa nchi zote walikubaliana kuheshimu mipaka ya nchi zetu iliyoachwa na wakoloni. Na hata huko tunakozungumzia ambapo kumefikia hatua kubwa sana ya ushirikiano kwa mfano Umoja wa Ulaya bado wanatambua mipaka ya nchi zao. Kwa hiyo, nasema hili tusilifanye kuwa dogo humu ndani tuone kwamba lina umuhimu kwa sababu lina misingi yake ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la kuchukua *consious approach* kwa Tanzania si suala jipya wala haitakuwa aibu tukitoa tahadhari hizi au labda pengine kuonyesha udhaifu. Wakati nchi zetu ndiyo kwanza zinapata uhuru Mwalimu Julius Nyerere ambaye tunamtumia mara kama ndiyo rejea yetu alitofautiana na Rais Kwame Nkhurumah ambaye alitaka kwenda katika *super state, running state of Africa* yeye aka-*propose* kwenda katika *gradually* na *conscious approach* kwa sababu hiyo hiyo ya kuzifanya kwanza nchi ziwe zimejiimarisha na zimejiweka vizuri kwa mambo kama hayo. Kwa hiyo, tunasema hilo halina ubaya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba hapa tunazugumzia hizi hatua zote hizi tunazungumzia masuala ya *solvate* (mamlaka ya nchi) na kila hatua moja ya *integration* maana yake tunapunguza *solvate* yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zitto alizungumza hapa kwamba tunahamisha mamlaka katika haya kutoka Dodoma kwenda Arusha na popote pale ambapo jumuiya hii itakuwa na Makao Makuu itaendelea kuwa Arusha au mahali pengine, sasa nasema kwa hiyo, ni vizuri sana kutizama hisia za wananchi wetu ni kweli *roll* au nafasi ya viongozi ni kuongoza na mara nyingine ambapo viongozi tunaona kwamba kuna maslahi kwa wananchi basi hata kama wananchi watakuwa na wasiwasi sisi tuwasaidie kuwajengea imani ya kuwaongoza. *(Makofi)*

Lakini si kila wakati vilevile katika kuongoza tunapaswa kudharau hisia au Afrika na wananchi wetu, tulikuwa hapa na mchakato wa kutaka maoni ya wananchi kuhusu suala la uharakishaji wa kuundwa kwa *East African Federation*. Wakati ule tukiwasoma vizuri Watanzania tena wote wa Bara na wa Zanzibar sio tu walizugumzia kukataa hoja ya *first tracking* lakini mjadala mzima ulikwenda kuonyesha wasiwasi mkubwa katika mambo haya haya ambayo leo yanazugumzwa na Wabunge katika Bunge hili ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni muhimu sana kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wanapoyazugumza haya kuzingatia hizi hisia za wananchi. Na kama ulivyosema kubwa lililokuwa limetajwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba tumesema hapa udhaifu mkubwa unaonekana ni kutokuweza kujiandaa kwamba kutokuwa tayari katika kujiandaa. Kama ni hivyo tunapaswa kujiandaa lakini hatuwezi kujiandaa kama ndani ya Serikali kwenyewe hakuna *coordination* baina ya zile tofauti kwa sababu haya masuala yanayozungumzwa hayahusu Wizara ya Afrika Mashariki peke yake.

Mheshimiwa Spika, humu katika itifaki hii tutazame kuna masuala ya biashara, kuna masuala ya ajira, masuala ya uchumi haya yanasimamiwa na Wizara tofauti ndani ya nchi. Sasa kama hakuna *coordination* kuna masuala ambayo yanazungumzia watu wetu kutokuwa tayari katika maana ya viwango vya elimu panazungumzwa Wizara ya Elimu. Kama hakuna *coordination* ndani ya Serikali maana yake ni kwamba tutaishia kila siku kupitishia maazimio ya kisiasa lakini hatujiweki tayari ndani na hilo ni jukumu la Serikali upande wake kuona kwamba kuna *coordination* ili kuandaa utaratibu.

Kwa hiyo, nadhani moja katika changamoto tuone kitu ambacho tunahitaji kukabiliana nacho na pengine Serikali itakapotujibu ni kiasi gani tunarekebisha mambo yetu ya ndani katika kufanya suala hili la *coordination*.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kujifunza kwa wenzetu ambao wameshapitia katika hatua kama hizo, imetajwa hapa Uingereza na tumeonywa kwamba tusiwe Uingereza katika Afrika Mashariki. Lakini Uingereza ilipofanya maamuzi yake wakati ule ilizingatia, Uingereza haijakaa kuwemo katika *European* ni mwanachama lakini ili *opt out* katika suala la *single parents* kuwa na sarafu moja ya Ulaya na ndiyo maana mpaka leo wanaendelea na *pound* ya Kiingereza na walifanya vile wakati ule wa mjadala

ukisikiliza ilikuwa ku-*preserve* au kuhifadhi nafasi ya Uingereza na hasa jiji la London kama ndiyo kituo kikuu cha fedha cha dunia achilia mbali cha Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuwa na hatua za tahadhari katika kujihami nafasi fulani ambayo nchi itakuwa nayo siyo suala la udhaifu lakini suala zima na kuangalia maslahi ya nchi na kile ambacho Waingereza waliki-*question* wakati ule kimedhihirika. Wiki tatu zilizopita ukiangalia jarida la *The Economist* walitoa *survey* ya uchumi wa nchi za Ulaya na ile *survey* pale kwenye *cover* ya lile jarida ilikuwa inatosheleza kukuonyesha vipi Ujerumani uchumi wake umehodhi uchumi wa Ulaya ukifuatiwa na uchumi wa Ufaransa. Ni ile kwamba msipochukua tahadhari katika baadhi ya mambo mengine mtakuta siku zote hakuna uwiano, hakuna usalama katika kutunza zile fursa zenu lakini wote kufaidika kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nasema haya yanatokezea kule yanaweza yakatokezea katika Afrika Mashariki. Kwa hiyo, nasema ni muhimu sana katika sisi kulitazama hilo la ku-*preserve* baadhi ya mambo ambayo tunadhani na tunajiona hatuko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kwa kuzungumzia suala lingine la nini nafasi ya Zanzibar katika masuala haya, ukisikiliza mdahalo hapa ni mjadala unaovutia kwamba tunazungumzia jinsi gani ya kuhami maslahi ya Tanzania katika jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo hatimaye tunaambiwa itatupeleka katika shirikisho la kisiasa. Kwa hiyo, na ndani ya Muungano nadhani si aibu ikiwa na Zanzibar nayo ikitaka kujua nafasi yake katika hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa makubaliano ya Muungano na hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano inapotafsiri sehemu ya makubaliano hayo kifungu au Ibara ya 102 inasema; "kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia orodha ya mambo ya Muungano katika nyongeza ya kwanza suala la pili ni Mambo ya Nchi za Nje, Ushirikiano wa Kimataifa halijatajwa kama ni suala la Muungano na hadi hivi leo ushirikiano wa kimataifa si suala la Muungano haidhuru tuna Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa lakini haya sio suala moja tusingekuwa na Wizara ambayo ilikuwa inapaswa kuitwa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Na ndiyo maana kwa muda mrefu sana Zanzibar ilikuwa ina idara yake katika Wizara tofauti wakati fulani katika Wizara ya Mipango wakati mwingine ilikuwa katika Wizara ya Fedha ilikuwa ikisimamia masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hofu yangu na hofu ya Wazanzibar naamini nawasemea ni kwamba wakati hatua hizi zinachukuliwa ni kiasi gani Zanzibar inashirikishwa na sio kushirikishwa kwa maana ya kushauriwa lakini hata katika *levels* hizi za kuidhinisha Mikataba ya Kimataifa. Nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar tunaipa kiasi gani kwa yale mambo ambayo siyo ya Muungano ambayo Mkataba wa Muungano na Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatambua kwamba Zanzibar ina mamlaka yake kamili *(Exclusive Judicially over all non union matters)* na hasa tunapozingatia kwamba

unapotazama mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki unapokwenda katika yale mambo ya jumuiya yapo 17 katika yale kumi na tatu si mambo ya Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano ni manne tu ambayo ndiyo yanasimamiwa na Jamhuri ya Muungano. Sasa Zanzibar inasemewa na nani maslahi yake yanalindwa na nani, tukiambiwa inalindwa na Serikali ya Muungano haina mamlaka juu ya mambo haya. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kiasi gani masuala haya yanazingatia nafasi ya Zanzibar na hata ukitazama nilikuwa naupitia hapa ukitazama haya maelezo ambayo imetupa muhtasari wa hili Azimio. Utakuta mambo yote yaliyotajwa kwa mfano natoa mfano mmoja tu katika ukurasa wa saba pale, sekta ya huduma ya biashara, sekta ya huduma za mawasiliano, sekta ya huduma ya ugavi, sekta ya huduma za uwakala, sekta ya huduma za elimu, sekta ya huduma za kifedha, sekta ya huduma ya utalii, sekta ya huduma za usafirishaji, yote haya ukiyatazama si mambo ya Muungano, sasa maslahi ya Zanzibar katika mambo haya yanalindwa na nani?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana naomba nimalizie kwa kudhani kwamba wakati umefika wa kulizingatia hili katika muundo wetu wa Jamhuri ya Muungano linafanyika kwa wenzetu ukienda kwa mfano Finland wana Muungano fulani wa kisiasa na visiwa vya Holland lakini vimeipa nafasi fulani ya kukubali kuridhia na kukataa baadhi ya mambo, ukienda Denmark, Greenland iko hivyo hivyo. Sasa nafasi gani ya Zanzibar katika masuala na ndiyo nasema kwa sababu hiyo nadhani Wizara yetu hii ingetuambia ni hatua gani zinazofanywa ili kutufikisha mahali Rais wa Zanzibar ambaye ndiye anayesimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwa na mamlaka kamili juu ya mambo yote haya yasiyokuwa mambo ya Muungano naye ashirikishwe katika vikao vya *summit* ili kuisimamia Zanzibar kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya mawazo hayo naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kama ilivyosema na msimamo wa Kambi ya Upinzani lakini kama nilivyosema naomba tupate majibu ya masuala haya niliyoyaeleza, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA**: Nimepokea na kuikubali rai ya Mheshimiwa Dk. Charles Mlingwa ambaye ameomba dakika kumi tu ambazo ndiyo muda uliosalia. *(Makofi)*

**MHE. DK. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niongee kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini kwa kifupi tu kwa sababu mambo mengine mengi yamekwisha kuzungumzwa. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa sana waliyofanya kwa utafiti wangu ni dhahiri kabisa hatua hii tuliyofikia ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni matokeo ya kazi kubwa sana waliyofanya wenzetu, Mheshimiwa Waziri akiwa kiongozi wa Wizara hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza sana katika hilo na nawatakia kila la heri muendelee na msimamo huo ili kuhakikisha kuwa chochote kinachokuja katika maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania inakuwa mstari wa mbele kuonyesha njia. Kwa sababu

umedhihirisha wazi jinsi mlivyosimamia suala la ardhi isijumuishwe katika itifaki hii lakini pia masuala ya uhamiaji, kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ni aina ya kujenga umoja wa hizi nchi wachama ambazo sasa ni tano, na naamini siku moja tutakuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki mimi naunga mkono sana kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Kwa hiyo, mimi natamani siku moja tunapokuwa nje ya Afrika Mashariki tuweze kusema mtu akikuuliza wewe unatoka wapi unamwambia natoka Afrika Mashariki, badala ya kusema natoka Uganda au Tanzania, basi akipenda kuelewa zaidi unasema sehemu gani ya Afrika Mashariki unamwambia Tanzania. Kwa sababu naamini katika umoja kuliko vinginevyo lakini kwa vyovyote vile hapawezi kukosa matatizo ndani ya harakati za kujenga umoja na ndiyo maana mchango wangu mkubwa ni ushauri kwa wenzetu ni dhahiri kuna baadhi ya nchi wanachama ambao kwa kweli unahitaji uvumilivu wa hali ya juu sana kuweza kukaa nao kwa sababu mambo ya msingi kabisa wanaweza kuyapindisha wewe wakakupa taabu sana.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Mheshimiwa James Lembeli amezungumzia suala la Doha, mimi pia naelewa na nilishawahi kushiriki mwaka 2002 na 2004, mwaka 2002 Santiago - Chile na mwaka 2004 Bankok, Thailand na kuhusu masuala haya ya *sights.* Wenzetu hawa wanakuja na hoja ziko wazi zikijaribu kuipiga vita Tanzania inachukiza kweli kweli kwa sababu zinatumika njia za aina mbalimbali kuhakikisha kuwa unashindwa na zingine kusema kweli zinakasirisha nasema zinakasirisha kwa kweli kwa sababu mimi nilishawahi kushiriki kwa hiyo, lazima tuseme ukweli na ni bahati tu ni wenzetu hawa wa Kenya. *(Makofi)*

Sasa yawezekana wamewaambukiza na wengine ambao ni wanachama wa siku za karibuni kiasi kwamba inasikitisha kuona kuwa hata Rwanda na Burundi zinatupinga, wanawashawishi watu wa Afrika Magharibi na nchi zingine Afrika ya Kati kupinga mambo ya Tanzania. Tanzania mimi natolea mfano wa Tanzania mimi natolea mfano suala la uhifadhi wa wanyamapori kwa Afrika Mashariki, Tanzania inaongoza kwa kuwa na sera na sheria nzuri katika mambo ya uhifadhi wa wanyamapori. *(Makofi)*

Mimi ni mtafiti na nimewahi kuwa kiongozi wa taasisi ya wanyamapori kwa hiyo, nafahamu nchi zote za Afrika Mashariki. Tanzania ukichukua hata Afrika labda tunafanana kiasi fulani na Afrika ya Kusini lakini wao wana mfumo tofauti kidogo kwa hiyo, Tanzania ni namba moja Afrika naweza kusema hivyo na ni miongoni mwa nchi zilizofaulu sana duniani na watu wengine wanajifunza kutoka kwetu lakini unapigwa vita kama vile sio jirani. Sasa huu ujirani wa kupiga vita namna hii na sio ujirani tu ni ndugu mnatoka kwenye nyumba moja nyumba yetu ni ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lakini badala ya kuongea akakueleza kasoro zako mkakubaliana ndani halafu mkitoka nje kule mnaondoka na makubaliano yenu kule kiasi kuwa hata mnapotofautiana mnaondoka mmekubaliana hivi, sasa kwa sababu tumetofautiana huko nje tutafanya hivi na ndiyo maana kwa wakati mwingine kwa watu

waliozoea kuwapiga akina mama, mama anaweza akaanza kulia, lakini akibisha hodi mgeni mama anafuta machozi mgeni akiingia mama yuko anafurahi wapo wanaume wachache nadhani wanaopigwa pia lakini wachache sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachosema hapa ushauri wangu kwa Wizara hii yaliyotokea Doha, na haya ya huko nyuma yanatufanya tupeleke ujumbe wa kusema jamani eeh, katika kujenga nyumba yetu ni muhimu tukubaliane namna ya kufanya huko nje ya Afrika Mashariki kwa yale tunayokubaliana na yale tusiyokubaliana ili kusudi tusiwe kama watu ambao Tanzania inatoka bara lingine, Kenya inatoka bara lingine haikubaliki, huwezi ukajenga nyumba kwa mtindo wa kupigana namna hii, haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika hili nimesema nimempongeza Waziri kwa niaba ya Serikali kwa kuchukua nafasi ya kuhakikisha kuwa mafanikio haya yaliyopatikana katika Afrika Mashariki, Tanzania imekuwa mstari wa mbele. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa dhati kabisa lakini naomba Tanzania iendelee kuchukua kiti chake cha mbele kama kiongozi katika kuona kuwa tunajenga Afrika Mashariki imara yenye uchumi uliokomaa, wenye usawa na haki kwa wananchi wote. Kazi yetu sisi ni kuhakikisha tu kuwa tunazo sera za kutosha ili kuhakikisha kuwa tunakuwa ni wachezaji kamilifu nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, mwanasayansi lakini pia umetusaidia sana kwa kuwa umetimiza ahadi, umefuata ule muda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, hebu niwataje wachangiaji wanne watakaoanzia saa 11.00 jioni ambao ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Halima Mdee na tutamaliza na Mheshimiwa Oscar Mukasa. Baada ya hapo, nakusudia leo hii hii Muswada unaofuata kwa marekebisho ya sheria mbalimbali *Written Law Miscellaneous Amendment* uanze kusomwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi awaandae wahusika ili twende hivyo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo basi nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha Shughuli za Bunge pale saa saba mchana niliwatangazia kwamba ninao wachangiaji wanne kama ifuatavyo, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Oscar Mukasa. Kwa hiyo, nitaifuata orodha kama ilivyo na kwa sasa namwita Mheshimiwa Pindi Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kupata nafasi hii na sambamba na hiyo nianze kwa ku-*declare* kwamba ninaunga mkono hoja hii ya kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote pia niunge mkono sana Serikali ya awamu ya nne ikiongozwa na Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu kwa kuisaidia sana nchi yetu ya Tanzania kuwepo katika ushirikiano huu wa kikanda yaani *Regional Integration* ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kulitafakari jambo hili na kwa bahati nzuri niliwahi kushiriki katika ukusanyaji wa kura za maoni kuhusiana na ushiriki wa sisi Tanzania katika ushikiano wa Afrika Mashariki kisiasa, wanasema *East Africa Political Federation*. *(Makofi)*

Katika ukusanyaji wa maoni yale, Watanzania sisi tukasema kwamba ushirikiano wa kisiasa kati ya nchi tatu bado ni mapema lakini ushirikiano wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na masuala ya masoko ni jambo ambalo ni muhimu na ni jambo ambalo linafaa sana kwa Tanzania na hata kwa nchi hizi tatu. Kwa hiyo, naungana kabisa na Wizara husika ya Afrika Mashariki kutuletea jambo hili muhimu hususan kwa wakati huu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa ina idadi ya watu milioni 40, lakini tutakaporidhia itifaki hii ya soko la pamoja maana yake tutakuwa na idadi ya watu katika *region* na kwa idhini yako naomba kusema kuwa nitakuwa natumia maneno ya Kiingereza katika baadhi ya maeneo kutafsiri kwa haraka inakuwa ni ngumu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutakuwa na *regional* yenye idadi ya watu milioni 90 wakati Tanzania peke yake ina watu milioni 39 hadi 40, maana yake kwa wale wazalishaji wazuri katika nchi yetu na wazalishaji wadogo kama mwanzo tulikuwa na tatizo la soko, sasa tutakuwa na uhakika wa ku-*supply* bidhaa zetu katika idadi ya watu milioni 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumesema tuwe na masuala ya kilimo kwanza, kilimo kwanza maana yake tunazalisha bidhaa mbalimbali, sisi watu wa Iringa ni wataalamu sana wa kuzalisha Mahindi katika Ukanda Kusini, viazi na chai maeneo ya Mufindi, ngano maeneo ya Makete na wazalishaji hawa 51% ni wanawake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni imani yangu kabisa kwamba baada ya kuridhia na utaratibu utakapokuwa umewekwa, masoko yetu ya kilimo kwanza ni ya hakika. Masuala kama korosho, pamba, kahawa na hata chai tuna soko lenye idadi ya watu milioni 90.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ipo haja sasa ya ku-*harmonise* utekelezaji kwa mfano ku-*harmonise* masuala ya *micro economic policies* na hata masuala ya *currency* kwa sababu itakuwa ngumu sana kwa mfano mtu utoke Tanzania ubadilishe pesa ya Kenya au utoke Kenya ubadilishe hela ya Uganda ndiyo maana katika *East Africa Treaty* wamesema *eventually* tutakuwa na *monetary union* kama *European Union,* wao wana *Euro* katika Muungano wao wa *Europe.* Kwa hiyo, huko mbele na sisi inabidi tutafakari hizi *transaction* itakuwaje.

Lakini ukilitazama jambo hili vizuri unapofanya *analysis* maana yake hata benki zetu zita-*transact* sana, sasa hapo ni muhimu sana Wizara ikaangalia suala la *central* kwa mfano *Tanzania* tuna *Bank of Tanzania* kila nchi ina *central bank*. Hizi *Central Banks* zetu wakati wa ku-*harmonise micro economic policy* zisipoteze *sovereignty* ya nchi hizi kwani kila nchi ina utaratibu wake lakini yapo maeneo ambayo tutaendelea kuungana. Kwa hiyo, suala la *sovereignty* ya nchi moja moja ni jambo ambalo lazima liheshimike. Kwa hiyo, pia ipo haja ya kutafakari masuala ya *identity card,* yaani tutatumia vitambulisho gani unapotaka kufanya biashara kati ya Tanzania na Kenya, je, kutakuwa na vitambulisho maalum vya *East Africa* kama vilivyokuwepo mwanzo au tutatumia *passport* ili shughuli zetu ziende haraka? Haya pia ni mambo muhimu sana kuyatafakari. Lakini sambamba na hilo tunapokuwa na soko la pamoja kati ya Tanzania, Kenya na Uganda ni hakika kabisa kwamba wapo wazalishaji iwe ni wa viwanda au wa malighafi mbalimbali au masuala ya kilimo kwanza, wao wenyewe kwa wenyewe watakuwa wanashindana yaani wazalishaji. Wazalishaji wanaposhindana maana yake bei inashuka na bei inaposhuka wale *producers* lazima waweke *quality* inayoeleweka yaani *quality* nzuri ili wale walaji waweze kunufaika. Kwa hiyo, ni jambo ambalo litasaidia sana *competition* na hata bidhaa mbalimbali ziwe ni za viwandani au za aina mbalimbali zitashuka tunapokuwa na hili soko la pamoja.

Sasa pamoja na fursa hizi ipo haja ya sisi kuchangamkia hizi fursa, tunaposema kuchangamkia fursa maana una soko la watu 90 unazalisha mazao *let say* kwa kutumia programu ya kilimo kwanza, lazima tuwe *sharp* kupata maeneo ya ku-*supply*. Kwa mfano, wenzetu katika hizi nchi nyingine wana *air line, Kenya Airline,* Rwanda wanayo, Uganda wanayo sisi Tanzania kidogo inasuasua nadhani kwa maelezo haya basi Wizara husika ijaribu kutafakari *Air Tanzania* itaanza kufanya kazi lini. Sasa haya mashirika ambayo yanafanya kazi hivi inakuwaje tunashindwa ku-*supply* hata chai, kahawa au hata maji katika *airline* hizi ambazo zinakuja Tanzania zinachukua watu wetu lakini unakuta inapo-*pack* au ndege inapo *land* Tanzania watu wetu wanaingia wanasafisha tu ndege na kuondoka, hatu-*supply* kitu chochote. Sasa *common market* ni fursa na fursa haziwezi kutufuata nyumbani ni lazima tuzichangamkie, hata chai Mufindi kuna chai bora, kuna *tea bags* za aina mbalimbali kama *lemon tea, hibiscus tea,* kilimo kwanza.

Sasa hizi fursa ambazo zipo tunasema idadi ya watu milioni 90 ni lazima sana tuzishughulikie, tuziwahiwahi *otherwise* tutakuwa tunaendelea kusema wenzetu wanafanya hiki na hiki na sisi hatuchangamki. Kwa hiyo, ipo haja ya kuhakikisha kwamba fursa zilizopo za ku-*identify.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kupitia mchango wangu huu naomba Wizara ya Afrika Mashariki iweke kitengo maalum pale kinachohusiana na masuala ya *common market*, kitengo hicho maalum kitakuta kina *deal* na *statistics* kila siku. Leo katika soko la *common market Tanzania* tume *supply agriculture products* kiasi gani, tume *supply* madini ya *Tanzanite* kiasi gani yaani kama vile *stock exchange* wanavyoangalia, au kama vile watu wanao *control foreign exchange* yaani soko la hisa na masuala ya dola wanavyojua kwamba *rate* sasa hivi imepanda au imeshuka. Kwa hiyo, tunahitaji watu *very qualified* katika Wizara ya Afrika Mashariki kuangalia kwamba soko letu la *common market* sasa hatu-*produce* zaidi au hatupeleki bidhaa zaidi tatizo ni hili na hili sasa tuongeze nguvu lakini *otherwise* tukiacha bila kuwa-*coordinated properly* italeta kusuasua kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, ipo haja ya kutafakari maeneo haya na lingine ambalo ni masuala ya *coordination* kati ya viwanda mbalimbali ipo haja ya kutafakari mambo hayo ili tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia *common market* lazima tuwe na *priority areas,* soko la pamoja linahitaji shughuli mbalimbali za kuliwezesha hilo soko la pamoja kwa mfano masuala ya miundombinu, tunayo barabara kwa mfano inayotika Iringa kuja Dodoma, ile ni barabara ambayo ni *Cape Town to Cairo*, sasa hizi bidhaa ambazo tumekubaliana tuwe na soko la pamoja ni lazima zisafirishwe kwa sababu miundombinu yetu tusipoiboresha italeta shida, tuboreshe njia za treni na barabara ili soko hili la pamoja tuweze kunufaika na kupeleka nchi za jirani.

Kwa mfano, tunapozungumzia kilimo kwanza mikoa ya Kusini wanazalisha mahindi na viazi, ingewezekana kabisa bidhaa hizo zinatoka mikoa ya Iringa unakuja moja kwa moja Dodoma unaunganisha mpaka Nairobi kuliko kuzunguka. Kwa hiyo, sambamba na hilo masuala ya miundombinu hususani ya barabarani muhimu sana tukayatafakari na kuyafanyia kazi tena kwa mapema ili tuweze kunufaika na suala zima la soko la pamoja.

Mheshimiwa Spika, siku zote umoja ni nguvu kwa hiyo kati ya hizi nchi tatu tunapokuwa na umoja itatusaidia sana kuwa na sauti, tutakuwa na sauti katika region yetu ya *East Africa* lakini wakati mwingine hata kujadiliana na *region* nyingine. Kwa mfano, tunapojadiliana na *region* ya *SADC* tutakuwa na nguvu sana na *region* nyingine ambazo zipo ndani ya Afrika na hata nje ya Afrika, *European Union* tukitaka kuongea nao itakuwa ni rahisi sana kuliko unapojadiliana na *region* nyingine unapokuwa nchi moja. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo nilidhani ni muhimu sana tukayazingatia na kuyatafakari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa soko la pamoja litasaidia kuwa na wawekezaji wakubwa ambao watakuwa na uhakika wa maeneo ya ku-*supply* changamoto nyingine ni jinsi ya kuvilinda viwanda vidogo vidogo, hiyo itakuwa ni changamoto kubwa sana baadhi ya maeneo bado teknolojia tunayoitumia ni ya kawaida sana. Kwa hiyo, yale maeneo ambayo teknolojia yetu ni kawaida tunavyo viwanda vyeti vya kujitosheleza kwa shughuli za humu ndani ya nchi kwa mfano *SIDO,* haya maeneo ni muhimu sana viwanda hivi vidogo vidogo tukavilinda ili viwanda hivi vidogo vidogo visije vikamezwa na viwanda vikubwa.

Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo ni lazima tujaribu kuyatafakari na kuyapa kipaumbele, tuyape mitaji, tuyasaidie ili yaweze kuzalisha shughuli ndogo ndogo isije ikawa soko hili la pamoja tunazalisha tu vitu vikubwa, wawekezaji wakubwa ndiyo wanakuja, kampuni kubwa kubwa na wale wazalishaiji wadogo tukawasahau.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naunga mkono hoja hii ya kuwepo kwa soko hili la pamoja na nina hakika naiona Tanzania yenye neema tele, naiona Tanzania yenye viwanda, Tanzania ambayo ukizalisha hata kitu kidogo kinahitajika kama siyo Tanzania kitahitajika Kenya na kama siyo Kenya basi Uganda. Wakati mwingine mtu unaweza ukashangaa kwamba huku maeneo ya vijijini masuala ya kilimo kwanza hivi hii biashara nitanufaikaje, lakini kwa maeneo ya pembezoni ni kwmba itakuwa ni rahisi kwa wale wafanyabiashara wakati wanakuja kununua kwa wafanyabiashara wadogo na wazalishaji wadogo na hatimaye wao ku-*supply* maeneo mbalimbali.  Kwa hiyo, naunga mkono nikiamini kwamba hata akinamama ambao ni 51% ya *population* yetu jambo hili la soko la pamoja litawasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ninaendelea kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana kwa ufafanuzi huo na sasa ninamuita Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na wakati huo huo Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii niwashukuru sana wapigakura wangu katika Jimbo la Lulindi kwa ushirikiano wao wanaonipa katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nawashukuru  sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kusema hivi sisi tuliokuwa hapa katika Bunge hili hakuna hata mmoja atakayesimama akapinga hoja hii, hata kidogo! Nasema hivyo kwa sababu za msingi kabisa, ninasema hivyo kwa sababu hakuna asiyejua kwamba Watanzania wanapenda umoja sana, wanapenda sana ushirikiano na wanawapenda majirani zao na wanapenda Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza hapa ni historia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, tusije tukafika mahali tukadhani kwamba hiki tunachokizungumza hakijawahi kutokea huko nyuma hata kidogo, ma-*champion* wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 waliokuwa wamesimama mstari wa mbele katika kuiunda mwaka 1967 ni Tanzania ikiongozwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. Ni Watanzania ambao walikuwa wa mwisho kabisa kukubali kuvunjika kwa Jumuiya iliyopita mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao walikuwa bado hawajazaliwa ama walikuwa wadogo nataka kuwaambia kwamba tulikubali kwa shingo upande kuivunja Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata tulipofika mahali tukaanza kugawana mali ilitusumbua sana, tulijiuliza hivi ni kweli tunavunja Jumuiya ya Afrika Mashariki? Nendeni katika vitabu mtaona. Kwa hiyo, tusije tukadhani hapa kwamba leo hii Watanzania hatutaki Afrika Mashariki hata kidogo tunachosema sisi tumeunda Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki, Chuo chetu Kikuu ni Jumuiya iliyopita iliyovunjika mwaka 1977. Lazima tujifunze huko kwani ni *reference* kubwa kabisa ili tusifanye makosa mengine tena, tusiwe tunaanza kila siku hatutaeleweka hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipovunja Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 mimi kipindi kile nilikuwa mtangazaji, tulifika mahali tulifunga mipaka yetu tukitaka kwenda Nairobi tunapitia Addis Ababa, Ethiopia, tulikuwa na kipindi tunaitana majina ya ajabu ajabu tu…

**WABUNGE FULANI:** Manyang'au!

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mmenisaidia! Majina ya chuki chuki tu, ilikuwa ni aibu! Aibu kubwa kabisa, watu ambao mnakaa nyumba moja mnachukiana, mnaonyeshana migongo, sasa haya ndiyo mambo ambayo tunataka kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi ulisema hapa kwamba tusizungumze zungumze masuala ya Doha, lakini hatupendi kuyazungumza hata kidogo, tunakumbushana kwamba kitendo kile tunamuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake yote watakapokwenda kupeleka *document* rasmi ya kuridhia hoja hii wawaambie wenzetu kwamba Watanzania wanasema tusirudie tena kitu kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kama hatujajiandaa kiasi hicho tungefika mahali tukajifungia katika mahoteli ya Kimataifa tukasema imekuwaje, ilikuwa hivi, ilikuwa hivi tukitoka pale tunakwenda kuteteana. Leo hii meno yetu ya ndovu yangekuwa yameshauzwa na hata wenzetu wangefaidika pia.

Mimi wakati mwingine nashindwa kuelewa hivi hawa ni Wakenya kweli ama kuna jambo gani. Hawa ambao wapo mstari wa mbele kutaka Soko la Pamoja, hela ya pamoja, *political federation* hivi ni Wakenya kweli ama kuna nini hapa? Wanasahau tulikotoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayazungumza haya kwa uchungu mkubwa kabisa. Tunayazungumza haya tusije tukafika mahali tukaingia kwenye vitabu vyeusi, eti Watanzania walikuwa hawapendi ushirikiano hata kidogo. Katika *article* namba 4, *objectives of the common market* inasema hivi naomba kunukuu kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika. Katika kipengele kidogo cha (b); "Strengthen, coordinate and regulate the economic and trade relations among the partner states in order to promote accelerated harmonious and balanced development within the community."

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki ni muhimu sana. Wenzetu wajue kwamba na sisi Watanzania tunapenda maendeleo ya pamoja, tunapenda tuishi vizuri kama wanavyopenda wao. Kwa maana hiyo basi wasije wakafika mahali wakafikiri kwamba ujanja ujanja, *shortcut shortcut* itawasaidia sana hata kidogo, wasije wakahatarisha jumuiya hii. Kama nilivyosema hapo mwanzo huko tulikotoka hivi ndivyo tulivyokuwa. Tuna majina hapa tunayafahamu waliosimama mstari wa mbele kuivunja Jumuiya hii. Naomba nisiyaseme kwa kutaka kuweka uhusiano mzuri kati yetu na majirani zetu. Kwa nini tufanye hivyo, kwa nini tufike huko, inatia simanzi sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawakaribisha, tumesikia sasa hivi wameshajaa kwenye mahoteli yetu, nasema hivi sio narudia kwamba sina cha kuzungumza ninasisitiza hii peke yake inaonyesha jinsi gani Watanzania tunavyowapenda ndugu zetu wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Nina hakika tena kwa asilimia kubwa kama hali hii ingetokea kwa majirani zetu katika nchi zingine leo tungesikia kule Watanzania wanarudishwa tena kwa nguvu kubwa kabisa. Lakini leo hii wenzetu wametulia tuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda katika mahoteli ya Zanzibar wanafanya kazi bila woga wala matatizo. Hatuwanyanyasi hata kidogo, wanajisikia wako nyumbani na hata kwetu Bara huku wapo. Hii ni dalili tosha kuonyesha kwamba Watanzania hatuna matatizo. Lakini hiyo isiwafikishe mahali wakadhani kwamba Watanzania ni sawa sawa na godoro, ukililalia linakwenda chini tu hata kidogo. Tunawaomba sana ndugu zetu na namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yako utakapokwenda kulipeleka ukawaambie kuwa Watanzania wale wa miaka iliyopita si hawa wa sasa. Tulichobaki nacho ni kupenda umoja, ushirikiano lakini hatubabaishwi tena tumeelewa, tumesoma sana, tuko wengi sana sisi arobaini milioni, tungesema kwamba tunatosha lakini hatuwezi kusema hivyo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokwenda Arusha ukalisisitize hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kumalizia kwa kusema haya, moja, bado Watanzania tunapenda ushirikiano, mbili, bado Watanzania tunakumbuka jinsi ilivyovunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977 na tatu, Watanzania tunahitaji maisha bora kama wenzetu wanavyohitaji. Na kwa maana hiyo mwisho Watanzania tunahitaji ushirikiano utakaonufaisha watu wote wa Afrika Mashariki ili huko mbele tunakokwenda kwa pamoja tunauondoa umaskini wa wananchi wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake na kwa jinsi anavyofanya kazi. Kwa kweli kama alivyosema Mama Anne Kilango, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Kwa hiyo, nakupongeza kwa dhati kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapitisha Itifaki ya Kuridhia Soko la Pamoja wakati huo huo tuna taarifa ambayo imeandikwa na gazeti la *East African* inayoonyesha kwamba

nchi za Afrika Mashariki kwa ujumla wake ukitoa Rwanda na Burundi katika kipindi cha miongo minne imepoteza kiasi cha dola zaidi ya bilioni 22 kutokana na rushwa kubwa kubwa Serikalini, kutokana na usafirishaji wa fedha haramu, kutokana na biashara chafu chafu. Sasa nadhani hii taarifa inaweza ikawa imekuja kwa wakati muafaka kwa sababu Jumuiya yetu inaingia kwenye Muungano mpana ambavyo vitu kama hivi tusipovirekebisha kama Serikali, tunaweza tukajikuta tunapeleka *East Africa* katika mikono mibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi ni kwamba Tanzania katika miongo hiyo minne miaka 40 ya utawala wa chama chetu ndiyo imekuwa inaongoza. Kwa hiyo, hii ni changamoto kuweza kuangalia ni kwa namna gani tunasuluhisha haya matatizo ili basi kama ambavyo ripoti imeonyesha tuweze kulipa madeni ya nje. Hizi bilioni ama dola bilioni zaidi ya 22 zingetosheleza kabisa kulipa madeni ya nje ya nchi zote tatu za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunatengeneza mfumo wa kiutawala ambao utaziba mianya ya upotevu wa fedha kama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kabisa kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuungana. Dunia ya sasa hivi sio dunia ya mwaka 1977. Dunia ya sasa hivi huwezi kusimama peke yako ukaendelea. Kama Jumuiya za Ulaya ama nchi za wenzetu za Ulaya ambazo zimeendelea zinaona umuhimu wa kuungana ili kuweza kuboresha biashara baina yao na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi wao. Nchi maskini kama Tanzania hatuwezi kuepuka suala kama hilo. Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuingia lakini tunaingiaje, tumejiandaa kimkakati. Kwa sababu sisi ni wazuri sana wa maandishi lakini lazima tufahamu tunapoingia kwenye hili soko la watu milioni 130 napenda kumsahihisha kidogo Mwanasheria mwenzangu pale alisema milioni 90. Milioni 90 ni Kenya, Tanzania na Uganda ukijumlisha Rwanda pamoja na Burundi ni karibu watu milioni 130. Sasa tunapopanua soko la watu milioni 130 ni kwa kiasi gani kama nchi tumejiandaa ndani. Ni wazi kabisa kwamba hapa mwanzoni kutakuwa kuna changamoto, lakini tunaamini vilevile changamoto hizi haziwezi kuzuia yale mafanikio mapana ambayo tunayatarajia mbele. Lakini Tanzania kama nchi tumejiandaa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa sababu tutakapofungua hii mianya kama tunavyotaka kufungua na mimi naunga mkono ni wazi kabisa kutakuwa kuna upungufu ama tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu wa Kitanzania, hilo halina ubishi. Ni wazi hii mipaka tukiifungua wafanyabiashara wadogo wadogo na wafanyabiashara wa kati wanaweza wakajikuta biashara zao zinafungwa ama zinakufa kwa sababu tulikuwa hatujajiandaa kwa kuwasaidia wao kimkakati kuweza kuendana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na ushindani wa kibiashara kwa sababu hakuna ubishi. Kenya wao ni nchi ya Kibepari, kwao wao suala la ushindani, suala la *confrontational* huwa ni kitu cha kawaida. Lakini sisi na ujamaa wetu tumekuwa wapole wapole. Sasa lazima tuwaandalie hawa watu wetu mazingira ya kuweza ku-*deal* na haya mabadiliko. Ndiyo maana tunaona Wabunge wengi wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, naungana mkono na Mheshimiwa Kabwe Zitto alivyokuwa akizungumza leo asubuhi. Tusilalamike, tuonyeshe njia, tena sisi tuna bahati kwa sababu tumepata fursa ya kusoma hizi Itifaki, kupata semina mbalimbali, sasa tujiulize yule

Mtanzania mmachinga wa kawaida kule Kariakoo. Kwa sababu Itifaki hii maana yake ni nini sio kwamba ni wafanyakazi tu wa kawaida watakaokuwa wana-*move* na watu ambao wanafanyabiashara za kujiajiri. Kwa hiyo, kama watu wetu hatutakuwa tumewaandaa maana yake ni nini? Kama ambavyo wamachinga wa Uchina wamejaa mjini Dar es Salaam watakuja wamachinga wa Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi, sisi tutabakia kulalamika. Hatuwaandai watu wetu, wenzetu wako *busy* kule wanaandaa watu wao. Kwa hiyo, tuna changamoto ya kuhakikisha kwamba tunaandaa mazingira muafaka ya kuweza kuwasaidia watu wetu. Hakuna ubishi kwamba kufunuka ama hii Itifaki tukiipitisha leo hii ongezeko la uhalifu lazima hatutalikwepa. Kuna uwezekano mkubwa sana wa uhalifu kuongezeka ndani ya Afrika Mashariki, tumejiandaaje kuli-*tackled* hili?

Mheshimiwa Mudhihir samahani kwa kuwaita wamachinga, umesema wanaitwaje? Wafanyabiashara wadogo wadogo. Samahani Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Kwa hiyo, ni muhimu tujiandae. Miaka 10 imepita tokea *custom union* ifanyike. Kuna *progress* kubwa sana imefanyika kutokana na kuondolewa huu ushuru wa forodha. Lakini bado viongozi tunalalamika. Kwa maana yake kuna tatizo la msingi inawezekana hata sisi wenyewe hatujaelewa kabisa umuhimu wa Jumuiya, inawezekana. Sasa kwa wale watu wetu kule chini inakuwaje. Mimi nasisitiza hapo kwa sababu tusije tukajikuta baadaye tunaanza kulia na kulalamika. Katika mazingira ya kawaida usitegemee kuonewa huruma. Usitegemee leo tuingie Jumuiya ya Afrika Mashariki Kenya kama nchi isijitangaze kwa sababu hapa kuna Tanzania, hakuna kitu kama hicho. Tutaingia katika Jumuiya, Kenya itaendelea kuwa kama alivyo kama ambavyo ana-*behave* sasa hivi, Rwanda itaendelea hivyo hivyo, Uganda itaendelea hivyo hivyo na sisi Tanzania tunatakiwa tuwe na huo utamaduni wa kushindana ama kuwa ngangari kama wenzetu wa *CUF* wanavyoutumia ule msemo. Bila hivyo tutapigwa bao la kisigino, hapo hakuna ubishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia *article 10* ya Itifaki. Ukiangalia katika *article 10* pamoja na mambo mengine inazungumzia hatua mbalimbali ambazo nchi imeamua kupitia katika kufungua hiyo milango. Sasa wakati napitia nikakutana na masuala ambayo kwangu naona ni ya msingi lakini naona Waheshimiwa wameyaona au wameona wayasogeze mbele. Kwa mfano ukiangalia kuruhusu Maafisa Ugani katika sekta ya kilimo wamesema kwamba tunaanza mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kila siku tunaambiwa kwamba kilimo kwanza. Sasa kilimo kwanza inaendana na nini? Kilimo kwanza lazima iendane na kuwa na wataalamu ambao watawawezesha hawa wakulima wetu maskini kule chini kuweza kulima kilimo kinachoendana na matakwa ya sasa ya hivi ili ndugu zetu hawa inawezekana kabisa Waziri wa Afrika Mashariki kwa kuwa anahangaika mwenyewe ushirikiano na hizi Wizara nyingine ambazo kimsingi zinatakiwa zimsaidie kuangalia kama nchi tunaendaje ni mdogo. Unaposema Maafisa Ugani katika sekta ya kilimo ni mwaka 2015 wakati mkakati wa Kitaifa kama nchi ni kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa kwanza na ndiyo kinategemewa na asilimia 80 ya Watanzania. Lakini wakati huo huo ripoti za Serikali zinaonyesha katika Maafisa Ugani 15,000 wanaohitajika tunao Maafisa Ugani 3,000 tu kuna upungufu wa Maafisa Ugani 11,700. Lakini tumeliona hili halina maana tumelipeleka mwaka 2015. *(Makofi)*

Sasa sijui ni vigezo gani ambavyo vilikuwa vinatumika. Eneo ambalo anatoka Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Stephen Wasira kulikuwa kuna njaa juzi, kuna upungufu wa Maafisa Ugani 40, lakini hili halionekani kama ni moja ya vipaumbele ambavyo vinatakiwa wakati tunafungua hii mipaka yetu ama njia zetu za kibiashara za Afrika Mashariki. Hii inashangaza. Ukija kwa Wahandisi wa Madini mwaka 2011 lakini madini katika kumwondolea maskini wa kawaida Mtanzania, *linkage* inakuwepo mbali kidogo kwa sababu ajira inatoa kwa watu wachache wenye taaluma. Ukija kwenye sekta ya ualimu unasema walimu katika shule za sekondari katika fani ya hisabati, fizikia, baiolojia na lugha ya kigeni kuanzia mwaka 2015. Leo hii tunajivunia kabisa, tumejenga shule za kata safi ilikuwa ilani ya *CUF* ikachukuliwa na CCM lakini bora liende tunashukuru Mungu. *(Makofi)*

Tumejenga shule za kata ni vizuri lakini kwa mwanasiasa yoyote anayezunguka nchi hii anagundua kwamba kuna tatizo kubwa sana la walimu katika nchi hii. Kama mnazunguka inawezekana wengine mnakaa tu kwenye majimbo yenu Mheshimiwa Makamba ndiyo anakwenda. Lakini kama mnazunguka nchi hii mtajua kuna tatizo kubwa sana la walimu. Ukienda shule ya kata walimu ni watatu, mwalimu mmoja wanafunzi 800, yaani hiyo kata ikiwa ina bahati sana labda walimu nane au kumi hizo ndiyo shule zetu. Lakini tunakuja hapa tunaambiwa mwaka 2015 tatizo ni nini? Ni kwamba hatujui vipaumbele vyetu au ndiyo hivyo tunatengeneza mfumo kule wajinga wabakie wajinga sisi tuendelee kutawala? Tusitengeneza mambo kama haya jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia masuala ya wahudumu katika sekta ya afya mwaka 2015, wote tunajua ni kwa namna gani akinamama wanafariki kutokana na maradhi ya ujauzito. Katika kila siku moja inayopita katika saa 24 mwanamke mmoja anafariki, lakini haya masuala kwetu sisi sio vipaumbele, lakini wenzetu Rwanda wajanja. *(Makofi)*

Sisi wakati tunaweka vikwazo ama tuna-*demand permit* kwenye sekta hizi nyeti, Rwanda wao wamesema kabisa kwamba sisi tunafungua milango wazi anayetaka kuja aje kwa sababu wanajua wao kutokana na vita iliyowakumba wanahitaji watu wa kujenga uchumi wao na kweli uchumi unajengwa vizuri, Watanzania wenye taaluma watakwenda kule kwa sababu lazima kutakuwa na *incentives* za maana, sisi tunabaki kulalamika.

Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba hatua zozote tunazozichukua ziendane na mikakati yetu ya kitaifa. Hamuwezi kutuambia kuna Kilimo Kwanza wakati Maafisa Ugani wanaohitajika ni 15,000 lakini tulionao ni Maafisa Ugani 3,000. Kuna upungufu wa 12,000 halafu mnasema Maafisa Ugani watakuja mwaka 2015; ili iweje? Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na dhamira za dhati na kuna haja vilevile kwa Waheshimiwa Mawaziri wengine wamsaidie Mheshimiwa Kamala, wakusaidie ili uweze kuja na taarifa sahihi au wao watuambie hivi vitu ambavyo vimewekwa 2015, kwao wao sio *priority?* Sasa kama hivi vitu vya msingi sio *priority,* hiki kitu tunachosema, “Maisha Bora kwa kila Mtanzania”, maana yake ni nini? Maana yake tunapiga ngonjera, inapokuja fursa kwa ajili ya utekelezaji, hatufanyi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Lakini pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yeye na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya, kwa kweli ni moja ya Wizara ambazo mwelekeo wake unauona kabisa. Nampongeza sana na timu yake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sasa nikija kwenye azimio letu la sisi kuingia kwenye soko la pamoja la Afrika Mashariki, sababu za kuingia kwenye soko la pamoja tunazo, tumesikia kutoka kwa wengi na sihitaji kuzirudia. Lakini nia ya kuingia kwenye soko la pamoja tunayo, ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameweka mkono wake pale kwa ngazi yake. Lakini pia tumesikia Mheshimiwa Kumchaya pale, ametueleza vizuri historia, lakini napenda tujiulize swali la tatu: Uwezo wa kuingia kwenye soko la pamoja tunao? Kama tunao, tunao kwa kiwango gani? Hayo mapungufu yaliyopo ni namna gani tutayafanyia kazi ili huko mbele tunakokwenda na sisi kama Watanzania tushiriki kwa namna ambayo inaleta manufaa kwetu sote?

Mheshimiwa Spika, nikisoma hii taarifa kwa ufupi Itifaki hii, sitakwenda kwenye lile kabrasha kubwa, utaona kwamba yaliyoelezwa pale ukurasa wa pili kuanzia kipengele (a) mpaka mwisho ni malengo ambayo sisi kama wanachama wa Jumuiya hii, nchi zote tano, kwa ngazi ya Jumuiya yamewekwa, tunataka kufanya nini na kufika wapi. Lakini tuna kazi ya ziada sisi kama Watanzania na tuna kazi ya kuhakikisha kwamba tunaweka mkakati ya Taifa kabla hatujafika kwenye ule uwanja wa kushauriana na wenzetu ni namna gani tunatimiza malengo haya, tujue sisi kama nchi tunataka nini?

Mchana huu nilikuwa nasikiliza kipindi kimoja cha *TBC1*, wako wenzetu wale wasanii wanaitwa, nimesahau kidogo, wanaongea wanasema chakula kilichoshindikana kuiva jikoni kitawezaje kuiva kwenye jua? Ukanifurahisha sana msemo ule kwamba sisi, kama nchi hatuwezi kukaa ndani tukahakikisha tuna mkakati ambao kwa dhati na kwa uhakika tunakwenda kwenye Jumuiya tukijua kwamba hii itatusaidia, sio rahisi sana kuzipata faida ambazo zimelengwa na haya tunayoyaona hapa kwa ngazi ya Jumuiya tukiwa tumefika kule. Tuangalie kwa nyanja zote kiuchumi, mahusiano ya biashara na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, mifano mingi imetolewa hapa, tumesikia ndugu zetu Wakenya sasa hivi kuna mkakati mkubwa kabisa unaendelea wa kujenga uwanja wa ndege ambao kwa namna ulivyokaa unakuja kufanya ushindani wa kibiashara na uwanja wetu wa Kilimanjaro. Huo ni Mkakati ambao wenzetu walishaona tunakwenda wapi kama Jumuiya, walishasoma mazingira ya nje, lakini pia wameshafanya *economic intelligence*, wameona kabisa tukifanya hivi hawa wenzetu tutawafunga goli kwa namna hii. Kwa ngazi yao ni sawa na sisi kazi yetu sio kulalamika. Kazi yetu iwe namna gani na sisi tunasoma mazingira ya nje katika kuingia kwetu kwenye soko la pamoja, lakini pia, ni kwa namna gani tunafanya *economic intelligence* kwenye nchi zote zinazotuzunguka kwenye Jumuiya kuona ni wapi ziko fursa ambazo tunaweza kuzitumia kama tutakuwa tumejipanga vizuri?

Nashukuru sana kwa mchakato unaoendelea wa Ujenzi wa Reli itakayounganisha bandari kavu ya Isaka kwenda Rwanda. Ule ni mkakati mzuri, lakini tuongeze umakini pale tuone ni namna gani tutakwenda kwa mapana zaidi. Unavyoongelea Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na manufaa na ushiriki ambao sisi kama Watanzania tunashiriki kwa ujumla, lakini iko Mikoa ambayo kwa kiwango kikubwa itashiriki zaidi kwa niaba ya Watanzania wengine. Kwa mfano, ushirikiano wa kibiashara wa Tanzania na Rwanda ni wazi wenzetu wa Ngara, Biharamulo, Bukombe na Kibondo wana nafasi zaidi ya kushiriki kwa nguvu zaidi kwa niaba ya Watanzania wengine.

Sasa ni kwa kiwango gani tumeangalia fursa zilizopo nchi za jirani za Rwanda na Burundi kwa maana ya bidhaa za kilimo, kwa maana ya kuweka mkakati utakaowezesha bidhaa za kilimo ambazo tunaweza kuzizalisha kwenye maeneo hayo? zinaweza zikapata kuongezewa thamani ili ziweze kukidhi haja ya ukuaji wa sekta ya viwanda kwenye nchi ya Rwanda.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Rwanda sasa hivi kama alivyosema mzungumzaji aliyetangulia, kuna mwelekeo mzuri kabisa wa mapinduzi ya viwanda ila wanafanya kwa manufaa yao, lakini unapokuja ngazi ya ushirikiano wa Afrika Mashariki ile sisi kwetu ni fursa. Ni namna gani tunaiona mapema? Ni namna gani tunaifanyia kazi mapema? Ni namna gani tunaanza kuchukua fursa hizo kabla wengine hawajashtuka?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Rwanda miezi michache iliyopita, kuna Mtanzania mwenzetu mfanyabiashara maarufu hapa anawekeza kiwanda kikubwa cha kutengeneza *juice*, ameshapata eneo sasa na kazi inakwenda kwa kasi kabisa. Lakini nikajiuliza kwa maelezo niliyoyapata kutoka kwa wenzetu wanaomkaribisha wanasema Mtanzania huyu atategemea matunda kutoka Tanga kwa ajili ya kiwanda chake Rwanda. Lakini ziko aina za matunda ambazo atazihitaji pale ambazo *potentially* zinalimwa kwenye Wilaya ya Ngara, Biharamulo, Bukombe na maeneo kama hayo.

Sasa kama tunakwenda karibu pale, tunakuwa wajanja tunawekeza mapema, ni wazi tunaweza kujibu haja ya soko la kiwanda hicho, lakini tutaweza kujibu haja ya nafasi ya kushiriki kwenye uchumi za Watanzania walioko maeneo ya karibu zaidi na pale na itakuwa na manufaa sio kwetu tu, hata kwa wenzetu wa Rwanda kwa sababu itapunguza gharama za uzalishaji kwa sababu malighafi haitakuwa inatoka mbali sana, kwa hiyo gharama zitashuka.

Mheshimiwa Spika, nije suala la ajira. Mchana huu baada ya wewe kutangaza watakaochangia jioni, Watanzania wanaotutazama walikwenda kwa kasi kabisa. Yupo mmoja amenipigia simu ananieleza namna yeye anavyosoma kwenye Tawi la Chuo Kikuu kimoja cha Uganda ambacho kina Tawi jijini Dar es Salaam. Anasema, Walimu walioko pale, asilimia 60 kwa maelezo yake, ni watu kutoka nchi zetu za jirani na asilimia zaidi ya 50 ya hao wanaingia nchini kwetu bila *work permit*. Anasema amefanya utafiti zaidi. Sasa hili tutahitaji kuthibitisha zaidi kama tuna haja. Wenzetu wanasema wanapenda zaidi kuchukua walimu kutoka kwao kwenye nchi hizo kwa sababu wanahofia sana kwamba sisi Watanzania tumekuzwa kwenye ile siasa ya ujamaa na

kujitegemea, kwa hiyo, wana wasiwasi tutakuwa *aggressive* kwenye kufanya kazi. Ni *concern* ambayo unaweza ukaikataa, lakini pia ni vizuri kuitafakari.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunapozungumza jambo la namna ile, unasikia kauli mara nyingine kutoka hata kwa viongozi ambapo wanarudisha kazi hiyo kwa Mtanzania mmoja mmoja kwamba Watanzania badilikeni. Lakini tunasahau kwamba pamoja na wajibu wa Mtanzania mmoja mmoja katika kubadilisha hali hiyo, Serikali ina wajibu pia. Vinginevyo hili jambo litakuwa limetawanyika na huwezi kulifanyia kazi kwa namna ambayo italeta tija. Tunayo mifano, tatizo la ugonjwa wa UKIMWI, ni tatizo ambalo ili liondoke ni lazima lishughulikiwe kwa ngazi zote. Kuna wajibu wa mtu mmoja mmoja kwamba yeye asipofanya wajibu wake, hata kama kuna jitihada za Serikali hatafanikiwa, ataingia kwenye tatizo hilo. Lakini pamoja na wajibu wa mtu mmoja mmoja, kuna wajibu wa taasisi zisizo za kiserikali na kuna wajibu wa Serikali kuangalia jambo hili lote kwa ujumla.

Kwa hiyo, ninaomba kama moja ya mikakati ya sisi kuingia kwenye soko la pamoja, tutazame ni namna gani tutaweza kuingia kwenye kubadilisha *mind set* za Watanzania. Tumpe wajibu Mtanzania mmoja mmoja kwa kuwakumbusha kwamba wana wajibu, lakini na Serikali ichukue nafasi yake. Ipo mifumo inayoweza kutusaidia. Wizara ya Elimu pale tuna nafasi, wale ambao ni wadogo tunaweza kuingiza elimu ya ujasiriamali tukabidilisha mawazo ya watu.

Mheshimiwa Spika, mchana huu nilifika kwenye duka fulani kununua dawa ya *cofta*. Nafika namwuliza mwuzaji kuna *cofta?* Ananiambia *cofta* zipo lakini anageuka anaangalia Televisheni. Nikamwambia dada yangu unafanya biashara? Ananiambia mimi nimeshakujibu kama hutaki nenda kwenye duka lingine. Unaweza ukamlaumu, lakini hiyo ni ishara moja ya mfumo mzima uko vipi, kwamba kuna *skills* tunazikosa pale tunapokuwa kwenye mifumo ya chini inayotukuza. Turudi tutumie fursa zilizopo, Wizara ya Elimu twende tuone namna gani tunaingia kwa hawa watoto ambao bado tuna nafasi ya kuwabadilisha, ni namna gani tunaingia kufanya mabadiliko ambayo ni ya taratibu lakini kwa muda mrefu yatazaa matunda kwa sababu kila mmoja atakuwa ameguswa. Lakini tusiache wajibu huo kwa mtu mmoja mmoja peke yake. Serikali ichukue nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningeomba kwa dhati kabisa Wizara yetu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, natambua kwamba uko utaratibu kwamba Wizara inaandaa mikakati itakayotumika kwa Watanzania kuingia kwenye soko la pamoja. Lakini pamoja na mikakati, kwa sababu kwenye itifaki hii kipo kifungu kinachoturuhusu kwamba wakati tutakuwa tumeshaingia na kuangalia kwamba tunakwenda vizuri na pale tunapoona hatuendi vizuri tuna nafasi ya kuondoka na kujipanga tena. Tujipange na kwa maana ya kuwa na *monitoring and evaluation framework.*

Mfumo wa kufanya tathimini, kwamba Wizara ya Afrika Mashariki ishirikiane na Wizara nyingine kuhakikisha zinatengeneza ile *platform* ya kushiriki kwetu, lakini kabla ya kuingia, tuhakikishe tuna mfumo wa kufanya tathmini ili siku ikifika, sisi Watanzania

na hasa Wabunge kwa niaba ya Watanzania wengine, tukiona kuna haja ya kupitia tena uamuzi wetu tuwe na namna ambapo kuna kioo ambacho kinatuonesha kabisa kwamba tulisema tutafanya hiki; tumefanikiwa? Ndiyo. Tulisema tutafanya hiki; hatujafanikiwa. Mwisho wa siku tunafanya uamuzi, tunasema tunadhani hatuendi vizuri. Kwa sababu haina maana kuingia tu kwenye itifaki za namna hii kwa sababu tu ya kukidhi haja kama hazileti tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, lakini naweka hiyo changamoto kwa Wizara, tufanye kazi ya kujipanga kuweka mikakati, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Oscar Mukasa. Sasa Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mtoa hoja naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii ili aweze kutoa machache na kwa kiasi kikubwa atakuwa anasaidia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuja mbele ya Bunge lako Tukufu hili. Aidha, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ya ushauri na maoni yao waliotupa katika kuleta au kuridhia azimio hili la soko la pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru sana Waziri wangu kwa ukakamavu na kujiamini katika kutenda kazi zake hasa kutokana ushindani mkubwa katika majadiliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, nawashukuru sana na kuwapongeza Watendaji wote wa Wazira yetu kwa namna wanavyofanya kazi zao vizuri. Napenda pia nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa namna ambavyo wanashirikiana na Wizara yetu kufanya kazi sambamba na Wizara yetu wakati wote, hususan Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote. Nawashukuru sana kwa msaada mkubwa mnaotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, leo wamezungumzia sana namna ya kuchukua tahadhari katika majadiliano yetu katika mchakato mzima wa mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tahadhari yenu na maoni yenu kwetu sisi tunayachukua na siku zote ndiyo inakuwa dira yetu katika utendaji wetu wa kazi na vile vile katika mazungumzo mbalimbali katika shughuli za Jumuiya. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa maoni haya. Nataka niwaambie kwamba tuko makini sana, tutaendelea kuwa makini, tulikuwa na tahadhari na tutaendelea kuwa na tahadhari zaidi kama ambavyo mmetuambia tufanye.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, haya yaliyojitokeza huko Doha na kwingine tunaomba tuyachukue na tukayafanyie kazi na naamini kutokana na ushauri huu mliotupa nina hakika tutafikia pazuri na mambo kama haya naamini kwa sasa hayataweza kujitokeza tena kwa sababu tutajitahidi kuimarisha Diplomasia na ushikiano na wenzetu ili kuhakikisha mambo madogo madogo ya namna hii hayajitokezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi, itifaki iliyoko mbele yetu, kwa kiwango kikubwa ni ile ambayo maoni na ushauri wa Wabunge na Bunge lako Tukufu waliotupa na tukayatekeleza kwa vitendo na matokeo yake itifaki hii kwa asilimia kubwa sana ni ushauri na mwongozo wenu. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba ni itifaki ya Watanzania na ninahakikisha kwamba itakidhi malengo na haja ya Watanzania na itasaidia sana katika kuimarisha uchumi, biashara na uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba uniruhusu nisitaje Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja kwa sababu Waziri wangu atafanya kazi hiyo kwa kuonesha kwa kila kifungu na kila Mbunge aliyechangia katika eneo hili. Lakini napenda niendelee kwa ujumla tu.

Kwanza nianze kwa ushauri tuliopewa kuhusu ushiriki wa Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Napenda niwashukuru sana Wabunge waliozungumzia jambo hili. Kwanza niseme tu kwamba ushauri tunaupokea, tutaufanyia kazi na pale inapohitajika kuwasilishwa katika ngazi husika. Tutafanya hivyo ili ushiriki uwe bora zaidi kwa ajili ya maendeleo ya Muungano wetu na maslahi ya Zanzibar na kwa ajili ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tunao utaratibu wa kushirikiana katika suala zima hili tunaposhiriki katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla ya kwenda katika mikutano hii, huwa tuna msimamo wa kinchi na kukutana na wenzetu wa Zanzibar. Zanzibar huwa inashirikishwa kuanzia ngazi ya watalaam, Makatibu Wakuu na hata ngazi ya Mawaziri na kila linalofanyika, tunalifanya kwa pamoja kwa maslahi ya pande mbili za Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ilizungumziwa hapa kwamba ilionekana sana miradi mingi iko kwa upande wa Tanzania Bara. Lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba na upande wa Zanzibar iko miradi yake kutokana na mazingira yake kama Kisiwa na miradi hiyo inasimamiwa kwa pamoja na Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Iko miradi mingi ikiwemo miradi ya kuendeleza viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba, miradi ya umeme kwa kutumia upepo, miradi ya *Roll On – Roll Off (RORO)*, miradi ya kilimo na uvuvi na mradi wa Bandari ya Magubi. Kwa hiyo, kwa hakika kila sekta tunashirikiana vizuri na naamini kwamba mambo yatakwenda vizuri kwa ushirikiano ambao tunakwenda nao.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia sana ni suala la biashara na uwekezaji. Wakati tunasaini Umoja wa Forodha, wasi wasi mkubwa wa Watanzania kwa kusaini Umoja ule wa Forodha ilikuwa ni kushuka kwa biashara na kushuka kwa uwekezaji nchini. Lakini kwa sababu ya umakini wa Serikali yetu na hatua zilizochukuliwa na kwa kushirikiana na wadau wote hasa sekta binafsi mambo yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa biashara, mwaka 2005 ambapo tulikuwa tunasaini Umoja wa Forodha, mauzo ya Tanzania katika nchi za Afrika Mashariki yalikuwa ni dola milioni 142 za Kimarekani. Tulichoagiza wakati ule ama manunuzi

yalikuwa ni dola milioni 176 fedha za Kimarekani. Lakini, mwaka 2008 Tanzania iliuza, kabla ya kuziuzia Burundi na Rwanda tuliuza dola milioni 272. Lakini baada ya kujumuisha Burundi na Rwanda katika mwaka 2008, mauzo ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifikia Dola za Kimarekani milioni 353 na tulichoagiza ilikuwa ni dola milioni 202. Kwa hiyo, ukitizama hapa kuna mafanikio makubwa kwenye suala zima la biashara.

Mheshimiwa Spika, na hata kwenye suala la uwekezaji; Katika uwekezaji unaotoka nje ya Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo inachukua *lion's share*, kwa asilimia 70 ya uwekezaji wote unaoingia Afrika Mashariki unakuja Tanzania. Kwa hiyo, pia ule wasiwasi kwenye sekta ya uwekezaji nao pia umepungua na hali inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye makusanyo yetu ya ndani, wakati tunasaini Umoja wa Forodha mwaka 2005, mapato ya ndani, makusanyo yetu kwa mwezi yalikuwa ni bilioni 160. Lakini, leo hii tunazidi bilioni 400 kwa mwezi. Kwa hiyo, kuna mafanikio makubwa katika maeneo ya makusanyo, maeneo ya uwekezaji na maeneo ya biashara.

Mheshimiwa Spika, msingi hapa ni kwamba hatuna haja ya kuwa na wasiwasi. Cha msingi ni kukubali mabadiliko, kama mlivyotuambia suala la kujipanga vizuri ili tuweze kufikia lengo letu. Juu ya hatua hizi, tunahitajika kufanya jitihada zaidi ili tupige hatua mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, limezungumziwa hapa suala la uratibu. Kwanza nataka kusema kwamba, tunapokea ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini, nataka niwahakikishie kwamba na sisi suala la uratibu na ushirikiano baina ya Wizara tunalipa kipaumbele sana na kwenye hili tumepiga hatua kubwa. Tunao ushirikiano mkubwa baina yetu na Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba kazi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuratibu zaidi na Wizara zenye sekta zao ndizo zinazohusika kuongoza mazungumzo katika mikutano husika. Kwa msingi huo ni kwamba Wizara zinafanya kila wajibu wake bila kuingiliwa na Wizara yetu, isipokuwa Wizara yetu inaratibu yale ambayo Wizara imeyakubali na kuyapitisha na pia kupitishwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, suala hili kama mlivyotushauri tutalizidisha na kuliendeleza.

Mimi nataka niwahakikishie kwamba, sasa hivi uko ushirikiano mkubwa na tutazidi kuuimarisha siku hadi siku. Ni lazima tukubali katika maisha ya kila siku, changamoto za hapa na pale zinatokea. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba pale ambapo unatokea upungufu, tutachukua hatua za kuondoa upungufu huo.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, changamoto nyingine ambayo imezungumzwa sana hapa ilikuwa ni suala la ardhi hasa ardhi yetu kuuzwa kinyemela. Nataka niseme wazi kwamba wale ambao wananunua ardhi kinyemela bila kufuata taratibu zilizopo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa, maana ardhi hiyo sio mali yao. Ardhi zina taratibu zake na lazima uipate kwa taratibu zilizowekwa. Tutakapopitisha

Azimio hili leo, tukaipa nguvu itifaki hii, tunazidisha uwezo wa kuweza kusimamia vizuri masuala yetu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba itifaki hii itafaa sana katika kusimamia masuala mazima ya ardhi na kuepusha haya mambo ambayo yanatokea. Lakini, eneo hili ndilo lilokuwa eneo nyeti sana kwenye mazungumzo na lilichukua muda mrefu sana kufikia hatua iliyonayo.

Lakini nataka niwapongeze sana watalaam wetu, Mheshimiwa Waziri na hasa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa hatua alizochukua ili kuhakikisha naye anawashawishi vya kutosha Wakuu wa Nchi Wanachama na kukubaliana na msimamo wa Tanzania kwenye masuala ya umiliki wa ardhi kwa sababu suala la ardhi linaongozwa na sheria na sera za nchi wanachama. Wenzetu mwanzo walitaka sana kuingiza jambo hili kwenye mazungumzo ya Soko la Pamoja, lakini kutokana na umahiri wa majadiliano ya upande wa Tanzania, jambo hili liliweza kufanyika vizuri na sasa masuala yote ya ardhi yanaratibiwa na sera ya sheria za nchi husika. Hivyo basi, masuala mazima ya tatizo la ardhi naamini sasa yataondoka na tutaendelea kuimarisha uwekezaji wetu na biashara zetu vizuri bila ardhi yetu kuingiliwa wala kuchukuliwa na mtu mwingine kinyume na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, suala lingine ambalo limzungumzwa sana sana na Waheshimiwa Wabunge lilikuwa linahusu masuala ya ajira ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Limezungumziwa sana suala la ajira za kiholela.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninaloweza kusema, kwanza kabisa, tunazingatia kwa umakini mkubwa kabisa ushauri wenu wote mliotoa kwenye eneo hili. Naamini utakuwa mwongozo mzuri zaidi na kuboresha zaidi jitihada zinazochukuliwa na Serikali kwenye masuala mazima ya ajira.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tutakwenda hatua kwa hatua katika kufungua milango ya ajira na tutafungua milango ya ajira kwenye yale maeneo yanayohitaji utalaam kwa kuanzia. Lakini, hii ratiba tuliyonayo sio msahafu, pale sekta husika itakapoona kuna umuhimu wa kurekebisha na mahitaji mengine, wakati wowote inaweza kufanya vile. Ile tuliweka kama tahadhari ili tusije tukajivuruga kwenye suala zima la ajira kutokana na umuhimu wa kukuza ajira zetu za ndani.

Kwa hiyo, hatua zilizochukuliwa na Wizara pamoja na Serikali ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata kwanza ajira na pale penye upungufu ndipo pale tunahitaji kutoka nje ya Tanzania. Kwa hiyo, yote yaliyofanywa yalifanywa kwa nia njema na kwa nia ya kuangalia na kulinda maslahi ya nchi yetu. Kwa hiyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili la ajira halina maana kuwa tumefunga moja kwa moja, pale ambapo patahitajika kufunguliwa mlango, sekta husika itakuwa na mahitaji hayo, basi hilo litafanywa ili kuhakikisha kwamba yale manufaa kwa njia hii yanapatikana kama ambavyo tunaona inafaa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, jambo la msingi hapa ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha elimu yetu. Hatua mbalimbali zimechukuliwa na

Serikali katika kuimarisha elimu. Ni ukweli kwamba tumepiga hatua kubwa kwenye eneo la elimu. Hivi karibuni wakati imefanywa *vetting* ya kutazama Vyuo Vikuu bora katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Chuo Kikuu cha Dar es salaam ndiyo kilitokea namba moja. Hii inaonyesha wazi ubora wa elimu yetu hapa Tanzania. Chuo cha Mzumbe kimepata namba tatu. Kwa hiyo, jitihada zinachukuliwa kuimarisha elimu na hata hivi karibuni mlisikia nchi ya Marekani ikipongeza sana hatua zinazofanywa katika kuimarisha elimu ya Tanzania.

Lakini, ushauri mliotupa kwenye eneo hili, tutawasiliana na Wizara husika ili yale yote ambayo yatazidisha *speed* ya kuongeza uelewa nchini, kuongeza utalaam nchini kwa ajili ya maslahi ya Watanzania, kazi hiyo kama mlivyoshauri Waheshimiwa Wabunge, tutaifanya na bila ya kusita. Nataka niwahakikishie kwamba yale yote mazuri mliyotuambia, tutayafanyia kazi ili mabadiliko katika nchi yetu yaonekane.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi hususan ya kimiundombinu ambapo nchi yetu imechukua hatua. Tumezungumza hapa, tukazungumzia nchi jirani wanafanya mambo mbalimbali ya kuimarisha miundombinu. Lakini, nataka niwahakikishie kwamba shughuli kama hizo na upande wa Tanzania zinafanyika sana kuanzia kuimarisha miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli, miundombinu ya bandari, miundombinu ya viwanja vya ndege, miundombinu ya vianzio vya umeme (kuimarisha umeme nchini) na kadhalika. Kwa hiyo, hatua mbalimbali zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waheshimiwa Wabunge tuone na jitihada zinazofanywa na Serikali zetu na hatua ambazo zimefikia. Lazima tufike wakati tujipongeze wenyewe kwa kazi nzuri inayoendelea. Haifai kujivunja moyo wakati uwezo wa kufanya hivyo tunao na uwezo wa kushindana na nchi nyingine tunao mzuri sana.

Kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tuelewe na upande wetu jitihada zinaendelea na hatua tuliyofikia tunahitaji kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, tutazidi kushirikiana ili tufanye vizuri kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walizungumzia suala moja kubwa sana la kuhusu kutoa elimu kwa umma. Kwa kushirikina na Wizara ya TAMISEMI tunaendelea kujipanga vizuri tuweze kutoa elimu kwa umma. Hivi sasa tumeanza kazi hiyo kupitia televisheni, vipeperushi na mijadala mbalimbali katika Vyuo Vikuu na vyuo vingine hapa nchini.

Aidha, watalaam wetu, Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na watendaji wengine tumekuwa tukifanya ziara mbalimbali katika Mikoa, katika taasisi mbalimbali, katika jumuiya za sekta binafsi na kadhalika. Kwa nia ya kutoa elimu kwa umma. Lakini, inaonekana bado eneo hili lina uhitaji mkubwa, sasa tunapanga mkakati mzuri zaidi kwa kushirikiana na TAMISEMI ili tuhakikishe kwamba basi elimu kwa umma inawafikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na ili nisipigiwe kengele ya pili, naomba na mimi nitamke wazi kuunga mkono Azimio hili la Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Aboud, Naibu Waziri wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Sasa tumefika wakati ambapo namwita Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili aweze kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali ziliozotolewa. Ana dakika zisizopungua 45.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa jinsi ambavyo umekuwa ukisimamia shughuli za Bunge kwa umakini mkubwa, lakini, nikushukuru kwa jinsi wakati wote Wizara yangu ilipoomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge, kukutana na Kamati, ulitupa fursa ya kufanya hivyo ili tuweze kuwaeleza yale yanayoendelea kuhusiana na mtangamano wa Afrika Mashariki ikiwemo masuala ya majadiliano ya Soko la Pamoja. Kwa niaba ya ya Wizara, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vile vile kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje na Bunge zima, lakini vile vile kushukuru wote waliochangia kwa maandishi na kwa mdomo. Nasema kwamba michango yao yote itatusaidia katika utekelezaji wa shughuli zetu katika Wizara kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Wilson Masilingi kwa jinsi ambavyo ameendelea kuongoza Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Namshukuru Mheshimiwa Azzan Zungu kwa jinsi ambavyo leo hii amewasilisha Taarifa ya Kamati kwa umakini mkubwa na tunaishukuru Kamati kwa kutuunga mkono. Namshukuru Msemaji wa Upinzani kuhusiana masula ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa jinsi ambavyo amewasilisha vile vile Taarifa ya Kambi ya Upinzani na naishukuru Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono Azimio hili. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Watendaji wa Wizara, Katibu Mkuu Dr. Tax pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi tunavyoshirikiana kutekeleza wajibu wetu. Lakini, nitakuwa sijatenda haki kama sitazishukuru Kamati mbili ambazo mnaweza nyie msizijue kwa kazi nzuri walizofanya. Tulikuwa na Kamati moja pale Wizarani ambayo iliitwa *High Level Task Force*. Kamati hii iliongozwa na Mheshimiwa Uledi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu ambayo ndiyo ilikuwa inaongoza Kamati ya Watalaam ya Mazungumzo ya Soko la Pamoja. Kamati hii ilifanya kazi nzuri sana.

Mazungumzo yalipoanza wenzetu wa nchi jirani walifikiri labda Watanzania hawajajiandaa vizuri, lakini kadri siku zilivyokwenda wakagundua wao ndio walikuwa hawajajiandaa na walikuwa hawaelewi vizuri hata Soko la Pamoja ni nini. Kwa hiyo, wakati mazungumzo yanaendelea, nchi nyingine ziliomba zipate mapumziko ili waweze kurudi kwenye *drawing board* kujifunza ili na wao wafananefanane na Watanzania katika mazungumzo hayo. Tanzania kama kawaida yetu hatukuwa na tatizo la kuzuia hilo, tuliwaruhusu wakarudi tena kwenye *drawing board*, baadaye wakarudi tena kwenye

mazungumzo wakaendelea. Lakini hatimaye hoja za Tanzania zote ambazo tulitaka ziwemo kwenye Itifaki ya Soko la Pamoja hivi leo nawathibitishia zote zilizingatiwa na ziko kwenye Itifaki ya Soko la Pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halitakuwa jambo la busara kuwasahau wapigakura na ukizingatia hasa huu ni mwaka muhimu sana kwa mwanasiasa yeyote yule, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa ushirikiano ambao wamenipa. Natambua maeneo mbalimbali ambapo nimekuwa nikipita wamekuwa wakiniuliza Mheshimiwa mbona hujatangaza? Naomba niseme, kipindi changu bado kinaendelea, bado naendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Lakini, nawaahidi wakati ukifika nitafanya kazi nzuri ya muda mfupi, yenye majeruhi wachache. Eeh, maana ukitangaza mapema, kampeni huwa zinatoa majeruhi wengi. Sasa ni vizuri ukatangaza kipindi kifupi kuepuka kuwa na majeruhi wengi kwa sababu na wengine wanaogombea na wewe wanakuwa ni wapiga kura wako. Sasa ukijeruhi watu unaweza ukapoteza kura nyingi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kabla ya kujibu nitambue wote waliochangia nikianza na wale ambao wamechangia kwa maandishi. Kwanza ni Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Abubakar Khamis, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Abubakar S. Faki, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Pascal D. Nakei, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale na Mheshimiwa Raphael Ligallama.

Mheshimiwa Spika, wapo waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Azan Zungu, Mheshimiwa Abubakar Khamis, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Raymond Alfons Mrope, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Suleiman Omari Kumchaya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mohamed Aboud.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba nashukuru sana kwa ushauri wa Kamati kama ambavyo umetolewa. Taarifa ya Kamati imebainisha wazi kwamba mambo yote ambayo Kamati ilishauri kuhusiana na ardhi, hati za kusafiria, kuhusiana na ukaazi wa kudumu tulizingatia katika Itifaki ya soko la Pamoja. Naomba niihakikishie Kamati kwa jinsi ambavyo mlitushauri tutayazingatia, mwendelee kutushauri na tutaendelea kuyazingatia yale yote mtakayokuwa mkitushauri.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati, vilevile walieleza umuhimu wa kuendelea kuelimisha Watanzania. Kuhusu eneo hili, Mawaziri wa Afrika ya Mashariki kikao chetu tulichokaa Arusha mwezi uliopita tumeagiza Sekretarieti kuandaa mkakati wa kutoa elimu ya masuala ya mtangamano kwa wa Afrika Mashariki. Lakini vilevile tumeiagiza Sekretarieti kuandaa *strategy* ya mawasiliano. Hivyo hivyo tumefanya katika Sekretarieti na katika ngazi ya Wizara, tayari tumeshakamilisha mpango wa kutoa elimu kwa umma ambao tumeanza kuutekeleza na mpango huu tumesema utakwenda na hautaishia ngazi ya Wilaya au Mkoa, bali utakwenda mpaka kushirikisha Serikali za Mitaa. Kwa kuanza, tumeanza kutoa elimu kwa kukutana na Wakurugenzi ambao watatusaidia sana katika kuendesha elimu hii.

Mheshimiwa Spika, kila Kurugenzi ilipo na kila Halmashauri tutakuwa *focal point* ambayo tutakuwa tunaitumia kuendelea kutoa elimu kuhusiana na mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ziko hoja nyingi ambazo zimetolewa, lakini kwa kweli sitaweza kuzijibu zote zile ambazo sitazijibu kwa kina, ninawaahidi kwamba na wataalamu wangu wamenihakikishia kwamba tutaandaa taarifa inayojibu hoja zote zilizojitokeza kwa kina ili tuweze kuwaletea Waheshimiwa Wabunge waweze kuzitumia siku zijazo hata kwa kutoa elimu au kurejea kile ambacho tutakuwa tumekieleza.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ambayo imetolewa kuwa ni vizuri Serikali ikashirikiana. Naomba nilihakikishie Bunge hili kuwa katika masuala ya Soko la Pamoja tunashirikiana Wizara yangu imekwishawasiliana na Wizara zote ili kila Wizara iangalie Itifaki ya Soko la Pamoja na kuweza kuona kila Wizara inatakiwa kufanya nini linaloangukia kwenye Wizara husika, lakini vilevile hivi sasa tunaandaa mkakati wa jinsi ya utekelezaji wa Soko la Pamoja utakaowezesha Tanzania kunufaika. Mkakati huo utapitishwa na Baraza la Mawaziri na kwa maana hiyo, mkakati huo ukiwa tayari utakuwa na baraka za Serikali nzima na utatekelezwa na Serikali nzima kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abubakar Khamis - Msemaji wa Kambi ya Upinzani ametoa hoja ambayo na mimi nakubaliana naye kwa asilimia mia moja kwamba ni vizuri tuendelee kuwa makini kulinda maslahi ya nchi yetu. Nakubaliana na ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi ya Upinzani imeshauri kwamba ni vizuri tukajali Uchumi. Jambo ambalo nakubaliana naye na kama alivyosema Naibu Waziri ni kwamba kwasababu tunavyodai masuala ya uchumi ndiyo maana hata katika Sekta ya Umoja wa Forodha ambayo tulipokuwa tunaanza kulikuwa na wasiwasi kwamba labda tusingefanya vizuri, lakini uzoefu umeonyesha kwamba tunafanya vizuri, lakini kilichojitokeza siyo kwamba tunafanya vizuri tu, hata mazao yetu ya biashara tunayouza kwenye soko la Afrika ya Mashariki yamebadilika kutoka kwenye mazao ya kilimo peke yake kwenda kuwa mazao ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, utakuta tulipokuwa tunaanza bidhaa za plastiki zilikuwa zinatoka Kenya zinakuja Tanzania, lakini sasa hali imebadilika, zinatoka Tanzania zinakwenda Kenya na nchi nyinginezo. Lakini siyo tu kwamba hali hiyo imebadilika, baadhi ya viwanda vya plastiki vilivyokuwa kwenye nchi hizo jirani wameanza kung'oa viwanda hivyo kwenye nchi hizo jirani na kuja kuviwekeza Tanzania. Kwa maneno mengine, huo ni ushahidi kwamba Tanzania kama tukiendelea kujipanga vizuri wawekezaji wengi zaidi ndani ya Afrika Mashariki wataweza kuja Tanzania na kuwekeza na ndiyo maana nchi kama Kenya ni mwekezaji namba mbili kwa Tanzania kwa uwekezaji ukilinganisha na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, Wakenya hao wamekuja kuwekeza Tanzania kwa sababu mbalimbali, lakini kikubwa ni mazingira mazuri ambayo tumeyaweka na ambayo tutaendelea kuyaweka. Iko hoja imetolewa na Kambi ya Upinzani kwamba ukiangalia jedwali na jinsi ya kufungua ajira tumeonyesha kuhusu wataalamu wa Ugani na upande wa Walimu kwenye Sekondari zetu kwamba tutaanza hivyo mwaka 2015 na Mheshimiwa Halima Mdee ameeleza kwamba ingekuwa vizuri tukafungua eneo hili kwa sababu ni la haraka.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja hapa. Mnapokuwa kwenye mazungumzo na mara nyingi mojawapo ya mkakati wa kutumia ambao ninaweza kuusema hapa, kwa sababu hata wenzangu wakiusikia kwasababu sitautumia tena kwenye mazungumzo kama haya ndiyo tumemaliza hivyo, kwa hiyo, ninachoweza nikasema kwa sasa ni kwamba mbinu ambayo tulikuwa tukiitumia ni kutoa jambo ambalo ni zito zaidi kiasi kwamba na wao wakizidi kujadiliana wanavyoshuka chini wanajikuta wamerudi kwenye kile unachokihitaji. Kwa hiyo, kwenye ku- *negotiate* unafungua wapi? Kwa maana wao walitaka tufungue kila kitu kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maeneo mengine kwa makusudi mazima tulionyesha kubana. Lakini kama nchi tukifanya utafiti na kujiridhisha kuwa tunapenda kufungua eneo fulani haraka, tunaweza kufanya hivyo na hakuna atakayetufunga mikono. Kwa hiyo, nawashukuru wapinzani kwa ushauri wao, namshukuru Mheshimiwa Mdee, tutaliangalia hili kuhusiana na Wizara zinazohusika, tukiona kuna umuhimu wa kufanya hivyo tutafanya hivyo. Hii ni tofauti na kama tungekuwa tumefungua tayari, tukafika hapa mkatuuliza mbona mmefungua? Ingekuwa ngumu kufunga, kwa sababu tungekuwa tayari tumeshamaliza mazungumzo ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwamba ziko hoja zimetolewa, Mama yangu Anne Kilango ameeleza vizuri sana suala la ajira kwamba mbona akiangalia anaona watu wengine wameshakuja hata kabla utaratibu haujaanza. Lakini niseme tu kwamba Baraza la Mawaziri la Afrika ya Mashariki tayari tulishaagiza nchi wanachama zifanye utafiti wa *manpower* kujua kila nchi ina wataalamu wa aina gani, ina upungufu wa wataalamu kiasi gani na imeajiri watu wa aina gani kutoka nchi jirani za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kama Tanzania, tayari tumekwishaanza kufanya utafiti huu ambao utatusaidia kujua mapungufu yetu ni yapi kwa wataalamu, tunao kiasi gani, tulioajiri kutoka nje ni kiasi gani na kwa kuanzia, tumeanza na Mikoa ambayo imechaguliwa kufanyika kama *Pilot study*. Mikoa ambayo tumeanza nayo kama *pilot study* tumeanza na Dodoma, Kilimanjaro, Mtwara pamoja na Mbeya. Sasa utafiti huu wa awali ambao tunatarijia ukamilike ifikapo Mei mwaka huu itatusaidia kuweza kujua kwa kina ni wataalamu wangapi ambao tayari Tanzania imewaajiri kutoka nje lakini pia itatusaidia kwa kina kujua wapi tuna upungufu na hatua zipi tuchukue kuweza kuziba nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Itifaki inayoanzisha Umoja wa Forodha ni kwamba zimewekwa taratibu na Sheria za jinsi wana-Afrika ya Mashariki wataweza kufanya kazi hapa. Ukija hapa Tanzania ukaomba kazi ukaipata hautaweza kufanya kazi hiyo kama hujapata *working permit* na ukiomba *working permit* siyo lazima tukupe. Tutakupa *working permit* tukiona kwamba: Je, hilo eneo ambalo umepata kazi ni eneo ambalo tumefungua? Je unazo sifa zinazostahili kufanya kazi hiyo? Je, tunakuhitaji ufanye kazi hiyo? Tukishajiridhisha, sasa ndiyo utapewa *working permit.*

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto kubwa tuliyonayo ni kuhakikisha kuwa haya tunayazingatia, lakini kwa kuwa sasa tunataka kuingia kwenye Soko la Pamoja itabidi vilevile tufanye utafiti wa kina kujiridhisha kama: Je, wale waliopo wapo kihalali? Kama hawapo kihalali, kama alivyosema Naibu Waziri, basi Sheria zitachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imejitokeza ya masuala ya ardhi, naomba niseme kwamba tulizingatia. Lakini vilevile kuna hoja Mama Anne Kilango, amesema, ni vizuri haya mambo ya kutangaza vivutio kila mtu atangaze kivyake. Lakini napenda kusisitiza kwamba kuna Muswada binafsi uliwaowasilishwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki ambao ulilenga kuanzisha kitu kinaitwa *Tourism and Wildlife Management Agency* (Chombo cha Afrika ya Mashariki cha kusimamia Masuala ya Utalii). Muswada huu ulipofikishwa katika Bunge hilo, mimi kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri niliwashawishi Mawaziri wenzangu wa kutoka nchi nyingine kwamba nchi wanachama zisiunge mkono Muswada huu kwa sababu mbili.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza ni kwamba, Itifaki ya masuala ya *Tourism and Wildlife Management Protocol* bado haijapata sahihi ya Mawaziri na bado Mabunge ya nchi wananchama Bunge letu kwa mfano halijaridhia kwa sababu Itifaki yenyewe haijawa wazi. Kwa sababu hiyo, niligundua kwamba masuala ya Utalii ni masuala nyeti na wala nchi wanachama zilikuwa hazijakubaliana zishirikiane vipi. Kwa sababu hiyo, nikawashawishi wenzangu kwa pamoja tukakataa Muswada huo kwa maana nchi wanachama zikisema kwamba zikubaliane na Muswada huo hata kama ukiupitisha maana yake Muswada hautapata baraka za Marais na usipopata baraka za Marais, Muswada huo ni sawasawa na kutokuwepo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna hoja ambayo inazungumzwa kwenye masuala ya Utalii na hoja yenyewe ni kama ama tuwe na *Single Tourist Visa* au tuendelee na utaratibu wa sasa. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wenzetu wa Wizara ya Utalii,

walijenga hoja vizuri kwa wenzao na wakakubaliana kwamba jambo hilo lisianze kwanza mpaka utafiti ufanyike. Hebu sasa tusubiri matokeo ya utafiti na matokeo hayo ya utafiti pamoja na uzoefu mwingine tulioupata, pamoja na yote mliyozungumza hapa yatatusaidia kufanya maamuzi kwa kuangalia ni lipi jema kwa Tanzania na lipi siyo jema kwa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza kwa umakini Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa jinsi alivyotoa hoja na akasisitiza kwamba Tanzania hatuwezi kukwepa suala la Ushirikiano na Mheshimiwa Halima Mdee akasisitiza hilo na Mheshimiwa Kumchaya naye akasisitiza. Naomba nikubaliane nao wote kwamba suala la Ushirikiano halikwepeki hivi sasa. Katika nchi zote duniani zaidi ya asilimia 50 ya biashara inafanyika ama kwenye umoja wa Forodha ama kwenye Soko la Pamoja kama hivyo ndivyo ilivyo hatuwezi kuepuka kuingia kwenye soko la pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile majadiliano yanayoendelea *WTO* ambayo yanataka kuondoa vikwazo vya biashara kati ya nchi na nchi, yanaruhusu vikwazo hivyo viweze kuwepo kama nchi hizo ziko kwenye ushirikiano wa Forodha au kwenye *Common Market.* Kwa maana nyingine, wakati tunaendelea na mazungumzo na *WTO,* njia pekee ya kuweza kuendelea kulinda mipaka yetu na kulinda ukanda wetu wa kibiashara ni kuwa kwenye *Reginal Blocks* kama *East African Customs Union* au *East African Common Market* .

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, nchi tajiri duniani na zenyewe zinajitahidi kushirikiana kwa mfano *America* ambayo ni Muungano wa zaidi ya nchi 50 wao vilevile waliona umuhimu wa kuungana na Canada pamoja na *Mexico* wakatengeneza kitu kinaitwa *North Atlantic Free Trade Area.*

Sasa kama Wamarekani pamoja na ukubwa wao na Uchumi wao bado wanaona umuhimu wa kuwa kwenye chombo cha kushirikiana kwa vyovyote vile nchi zetu maskini kama Tanzania lazima na sisi tuone umuhimu huo, lakini kwa nchi kama Marekani pamoja na ukweli kuwa iko mbali sana na nchi za Asia kumeanzishwa Taasisi inaitwa *Asia Pacific Economic Corporation* ambayo Marekani ni mwanachama, sasa unajiuliza pamoja na umbali uliopo kati ya uliopo kati ya nchi za Asia lakini bado Marekani ameona ashirikiane na nchi za Asia kwa kuunda umoja wa *APEC*.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyowafanya wajiunge kule ni kwasababu ya nusu ya *GDP* ya dunia inapatikana kwenye nchi zilizo *APEC*. Kwa sababu hiyo, ukiwa umezungukwa na nchi ambayo ina uchumi mzuri, hiyo ni sababu nzuri ya kushirikiana kwa karibu zaidi kuliko kuachana.

Mheshimiwa Spika, pia uzoefu umeonyesha mtikisiko uliotokea duniani, makampuni ambayo yalikuwa yamefanya biashara katika masoko ya Kimataifa yameyumba zaidi kuliko makampuni ambayo yalikuwa yakifanya biashara kwenye soko la kikanda. Ndiyo maana leo hii ukiwa na *incentive* yoyote unataka kuipa kampuni *incentive* hiyo kama unamwambia kwamba utamwondolea kodi ili auze katika Masoko ya Kimataifa atakwambia hiyo hapana, bora aendelee kulipa kodi, lakini aruhusiwe kuuza

kwenye soko la kanda. Ushahidi huu wa kuyumba kwa uchumi duniani unatukumbusha umuhimu wa sisi kushirikiana zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwasababu hizo nilizozitoa, naungana na Mheshimiwa Kabwe Zitto pamoja na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Kumchaya kwamba Tanzania tunatambua umuhimu wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki na tutaendelea kufanya hivyo. Lakini Mheshimiwa Kabwe Zitto pamoja na Mheshimiwa Dr. Mlingwa walisema, Tanzania lazima tutoe *leadership,* tutoe uongozi.

Naomba niseme kwamba Tanzania tunatoa uongozi katika Afrika ya Mashariki na tunaendelea kutoa uongozi kwa mfano yalikuwepo mawazo kwamba katika kushirikiana ama twende haraka ama twende hatua kwa hatua, maoni yalipokusanywa kwenye nchi zote wanachama, nchi zote nne zilisema kwamba twende haraka haraka, Tanzania ilisema twende hatua kwa hatua, Wakuu wa Nchi walipokaa kwenye Kikao waliibuka na msimamo wa Tanzania kwamba ni vizuri twende hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, Tanzania tulitoa *leadership* katika eneo hili. Naomba kuzidi kuthibitisha kwamba Tanzania hatuanzi kutoa *leadership* leo, tulianza zamani mwaka 1963, Mwalimu Nyerere alizishauri nchi za Afrika ya Mashariki na alizieleza kwamba Tanzania ilikuwa tayari kuchelewesha uhuru wake, lakini akawaambia tukipata Uhuru tu, basi badala ya kila nchi kuwa na Benki Kuu yake, badala ya kila nchi kuwa na sarafu yake, tuwe na sarafu moja ya Afrika ya Mashariki. Ni kwa bahati mbaya na ninasikitika na Watanzania walisikitika nchi zilizotuzunguka hazikuunga mkono wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa tuko katika ushirikiano huu, hatua ya pili ni ya *common market* ambayo tunataka kuingia, hatua ya tatu itakuwa ya sarafu moja. Naomba nizihakikishie nchi zote wanachama wa Afrika ya Mashariki, Tanzania itatoa uongozi katika eneo hili. Ilitoa uongozi mwaka 1963 na sasa itaendelea kutoa uongozi kwa sababu sarafu moja ni muhimu kwa nchi zote wanachama wa Afriaka ya Mashariki. Tanzania haikuishia hapo wakati wa mazungumzo ya soko la pamoja, wengi walifikiri kwamba masuala ya ardhi maana yake ndiyo Soko la Pamoja. Tanzania tulitoa uongozi tukasema hiyo siyo maana yake na mwisho wa siku wakabaini kwamba kweli hakuna sababu ya masuala ya ardhi kuwa kwenye Soko la Pamoja na wote tukakubaliana na katika hilo tukatoa uongozi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Jumuia ya Afrika ya Mashariki toka ianze imekuwa ikiendeshwa bila sera. Imekuwa ikiendeshwa kwa Katiba, lakini Katiba au Mkataba siyo Sera kwa kutumia Mkataba, unatakiwa uangalie ni mambo yapi unayotakiwa kushirikiana muweze kuwa na Sera. Toka Jumuiya hii ilipoanza hadi sasa ilikuwa haijawahi kuwa na Sera imekuwa ikiendeshwa kwa Mkataba na mawazo mbalimbali yaliyokuwa yakiibuka kwenye vikao mwaka huu Tanzania ndiyo tumeshika Uenyekiti wa kuongoza Jumuiya hii kwa kutoa mwongozo tumeshawishi wenzetu umuhimu wa kuwa na sera ya Afrika ya Mashariki na katika kikao cha Mawaziri wa Afrika Mashariki tuliokutana hivi karibuni wamekubaliana na mawazo ya Tanzania. Hivi sasa kwa mara ya

kwanza katika historia ya Afrika ya Mashariki tunaandaa sera ya mtangamano ya Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, tumetoa uongozi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania vilevile tumetoa uongozi katika Afrika ya Mashariki Wakuu wa Nchi walipokutana na niseme siyo kwamba tumetoa uongozi katika Afrika ya Mashariki. Tumetoa uongozi ndani ya Afrika Mashariki na nje ya Afrika Mashariki Wakuu wa Nchi za *SADC*, *COMMESA* na *EAC* walikutana kule Kampala walikuwa na mawazo kwamba uanzishwe ukanda huru wa biashara wa *SADEC, COMMESA* na *EAC.* Mheshimiwa Rais wetu alipopewa nafasi ya kuzungumza, akawaambia ukanda huru wa kibiashara bila kuwa na Umoja wa Forodha ni sawa sawa na kutofanya lolote. Kwa hiyo, akawaambia Marais wenzake wa *SADEC, COMMESA* na *EAC* tuanzishe ukanda huru wa kibiashara kwa nia ya kuelekea kuwa na Umoja wa Forodha wa *SADEC, COMMESA* na *EAC*.

Mheshimiwa Spika, Marais wote wa *SADC*, *COMESA* na *EAC* walikubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Rais wetu, kwa mara nyingine tukatoa uongozi sio tu kwa *EAC* bali kwa nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, naomba kumthibitishia Mheshimiwa Zitto kwamba Tanzania tutaendelea kutoa Uongozi na kushirikiana na wenzetu ili tuweze kujenga Afrika Mashariki iliyo imara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Dr. Mlingwa, Mheshimiwa Mrope pamoja na Mheshimiwa Kumchaya wamesema wanakumbuka yaliyotokea mwaka 1977 na wasingependa Jumuiya hii ivunjike tena. Pia Wabunge wengi walizungumza hapa mambo yaliyotokea DOHA. Naomba nichukue nafasi hii kuzikumbusha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mara kwa mara wawe wanasoma kifungu cha Sita cha Mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki utakaosaidia sana Jumuiya hii iweze kudumu na iweze kuendelea.

Ukisoma kifungu kile kinazitaka nchi wanachama kuendelea kuaminiana, kuheshimiana, kuishi kwa amani pamoja na ujirani mwema, kumaliza migogoro kwa amani, kushirikiana kwa manufaa ya wote na kinazitaka nchi wanachama kila mtu kutojifikiria yeye mwenyewe kabla ya kumfikiria mwenzake.

Mheshimiwa Spika, yote yaliyozungumzwa hapa nimeyasikia kwa kutumia nafasi ya uongozi wangu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nitazikumbusha nchi wanachama kwamba ziendelee kuzingatia hilo ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na ukweli kwamba yote yametolewa kwamba Jumuiya hiyo inaweza ikavunjika, lakini ninaomba niwahakikishie kwamba Jumuiya hii kwa akili za kibinadamu na kwa yote tuliyoyaweka kwenye mkataba wa kuanzisha Jumuiya hii, kwa kweli labda yatokee maajabu mengine ya dunia, Jumuiya hii haiwezi kuvunjika.

Mheshimiwa Spika, sababu moja iliyopelekea Jumuiya ya Afrika Mashariki ivunjike, wakati ule ilikuwa kwa sababu kila nchi ilikuwa na itikadi zake. Wengine

walikuwa Wajamaa, wengine walifuata mfumo wa Kibepari, wengine usingeweza kujua kama ni Wajamaa au ni Wapebari maana walikuwa hawajajua wako wapi. Lakini mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa, unazitaka nchi zote kufuata falsafa ya Soko, kwa sababu hiyo, hatutarajii uwepo tena mgongano wa kuitana fulani ni Mjamaa na fulani ni Mbepari, kwa sababu Mkataba huu unasema ukijiunga na Jumuiya ni lazima uamini katika Sera za Soko.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine kilichopo kwenye mkataba huu ni kitu kinaitwa *Asymmetry Principle*, kwamba katika ushirikiano huu kama kuna nchi inaeleza kwamba yenyewe inafikiria kwamba kwa kufanya jambo fulani itapata matatizo na inaomba ilifanye kwa staili ya mwingine huwezi ukaikatalia. Yeyote akija na hoja akasema anaomba afanye hivi huwezi ukamkatalia na ndiyo maana Januari, 2005 tulipoanza umoja wa forodha, Tanzania na Uganda tulijenga hoja kwamba bidhaa za *category* (b) kutoka Kenya kuja Tanzania na kwenda Uganda ziwe zinatozwa ushuru unaopungua taratibu kwa sababu ya *Asymmetry Principle* ambayo inasaidia sana kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, lingine lililo ndani ya Mkataba ule ni kwamba ushirikiano wetu usiende kwa haraka uende hatua kwa hatua, kwa sababu ukisoma kifungu cha tano sehemu ya pili, kinaeleza kwamba tutaanza na Umoja wa Forodha, baadaye Soko la Pamoja, baadaye sarafu moja na baadaye mambo yakienda vizuri tunaweza kwenda kwenye shirikisho la kisiasa. Sasa hayo tukiyaheshimu na kuyafuata hatuwezi kuingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililopo kwenye mkataba ni kwamba lazima kila kitu twende *progressive* na ndiyo maana Itifaki ambayo leo mtairidhia mambo yote yaliyomo mle hayaanzi rasmi tarehe tarehe 01 Julai, 2010 isipokuwa kila nchi itaanza kutekeleza kadri ilivyosema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililopo kwenye mkataba ule ni kwamba maamuzi yote yanafanyika *by consensus.* Hakuna nchi itakayolazimishwa kukubali jambo isilolitaka na nchi ikikataa jambo fulani kwamba halifai maana yake ni kwamba inabidi mkubaliane kwamba mambo yameishia hapo. Kama tukiendelea kuheshimu hii itasaidia sana umoja wetu kuweza kuendelea kuwepo. Jambo lingine ni suala la *subsidiary,* kushirikisha watu, *people centred,* lakini na miradi iliyo mingi inatekelezwa kwenye nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuyaangalia haya, naomba niwaondolee wasiwasi wale ambao wanafikiri kwamba labda Jumuiya inaweza ikavunjika kinachotakiwa ni kuheshimu misingi tuliyojiwekea, ndiyo itasaidia Jumuiya hii kuweza kuwa imara na kupiga hatua mbele.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Mahenge vile vile alisema kwamba ni vizuri Wajasiriamali watoe bidhaa zenye viwango. Naomba kuchukua nafasi hii kupitia maonesho ya Wajasiriamali na Juakali ambayo yanafanyika kila mwaka ndani ya Afrika Mashariki. Mwaka 2008 Wajasiriamali wa Tanzania waliibuka wakiwa vinara kwa kuonesha bidhaa bora kuliko bidhaa zozote zinazotoka nchi yoyote ile ndani ya Afrika

Mashariki na hii ni matokeo ya kazi nzuri ambayo imefanywa na *SIDO* pamoja na wadau wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilijulishe Bunge lako kwamba mwaka 2006 Bunge la Afrika Mashariki lilitunga sheria inayoangalia masuala ya viwango, masuala ya *Standardisation, Quality Assurance, Testing and Metrology,* sheria hiyo inazisaidia na inaendelea kutuongoza kuweka viwango vinavyofanana ndani ya Afrika Mashariki na hivi karibuni taasisi za viwango za nchi wanachama zimeshaweka viwango 1000 na wataendelea kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, tunashukuru kwa mchango wake, amezungumzia suala la *coordination,* Naibu Waziri wangu amelielezea vizuri, nakushukuru, tutaendelea kulizingatia. Lakini vile vile naomba nisisitize kwamba ushahidi wa kwamba maslahi ya Zanzibar yanaendelea kulindwa ni Itifaki ambayo tunaipitisha leo kwa mfano, inapokuja kwenye suala la ujenzi wa Hoteli za Kitalii, uongozi wa Zanzibar ulieleza kwenye Kamati ya Tanzania kwamba wasingependa kule Zanzibar ujenzi wa hoteli za kitalii kuanzia nyota Tatu, wakasema zianzie nyota nne na ndiyo maana ukisoma Itifaki, inasema tunaruhusu Tanzania isipokuwa kwenye mbuga za Wanyama pamoja na Visiwani, maana yake tulilinda maslahi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Itifaki hii utagundua kwamba inapokuja kwenye Ualimu wa Kiingereza, *English Medium* ambao kwa Tanzania Bara tumesema kwamba kuanzia mwaka 2010 Walimu wanaokuja kufundisha kwenye Shule za Kiingereza wenye digrii wanakaribishwa, lakini Mawaziri kutoka Zanzibar tulipokutana kama Watanzania, walisema wao kwa Zanzibar, hilo hawataki, ndiyo maana ukisoma kule utakuta kwamba Walimu wa Kiingereza wanaruhusiwa isipokuwa Visiwani.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie kwamba maslahi ya Zanzibar yanaendelea kulindwa. Lakini vile vile ukifuatilia vitu ndani ya Afrika Mashariki ni kwamba ukitaka kuagiza mchele kuutoa nje ya Afrika Mashariki ni lazima ulipie asilimia 75.

Kuna kipindi Zanzibar walijenga hoja wakasema kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa mchele hata Bara walikuwa wanashindwa kupata mchele huo. Kwa hiyo, wakataka waruhusiwe kuweza kuingiza mchele bila kulipia asilimia 75 na hilo tulilisimamia kikamilifu na likatekelezwa. Kwa hiyo, hakuna maslahi ya Zanzibar yoyote yale ambayo yameshapotea na wala hakuna ambayo yatapotea kwa sababu tukienda kule tunakwenda kama Tanzania na unaposema Tanzania ni pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wakati wote kama nilivyosema, maslahi ya Zanzibar yatalindwa. Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, ametoa hoja akasema ingekuwa vizuri tuendelee kulinda ajira, nakubaliana naye. Akasema tuendelee kulinda ardhi yetu, pia nakubaliana naye. Mheshimiwa Godfrey Zambi amesema kwamba tuongeze mazao, nami nakubaliana naye kwa sababu ukiangalia Umoja wa Forodha tunasema kwamba mchele kutoka nje ya Afrika Mashariki unalipa asilimia 75, sukari kutoka nje ya Afrika

Mashariki inatakiwa ilipiwe asilimia mia moja, mahindi kutoka nje ya Afrika mashariki asilimia 55.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hayo kwa kulinda soko la wakulima wa Afrika Mashariki, ndiyo maana Tanzania kama mnavyofahamu tumekuja na mpango wa Kilimo Kwanza, tumekuwa tukitekeleza *ASDP* na ndiyo maana jitihada zinafanyika ili kuweza kujenga viwanda vya kuongezea ubora wa mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Janeth Mbene amezungumzia suala la ardhi kwamba ni nyeti, nakubaliana naye na akasema itifaki peke yake haitoshi ni lazima vile vile tuwe na mkakati. Mkakati huu tumeanza kuuandaa na tayari tumeshapata *draft* ya kwanza, utaendelea kuboreshwa na hatimaye utakuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, Dr. Mwakyembe tunamshukuru kwa mchango wake, ameulizia tathmini ya *Customs Union* iko wapi? Kama nilivyosema kwenye semina ni kwamba tayari tumefanya tathmini na inaendelea kuboreshwa na ikiwa tayari tutakuja mbele ya Wabunge kuweza kutoa semina ili kuijadili hiyo tathmini ya *Customs Union*.

Mheshimiwa Spika, niseme hili kwa kumalizia kwamba kwenye *Customs Union* Mheshimiwa Mwakyembe aliuliza miaka mitano ya kujiandaa Tanzania tumefanya nini? Miaka mitano ya kujiandaa kilichofanyika Tanzania ni kwamba, tulipoanza ushirikiano tulikuwa tunapeleka bidhaa za mashambani tu, lakini sasa bidhaa zimebadilika tumeanza kupeleka na bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Spika, leo hii mimi Kamala kama Waziri wa Afrika Mashariki wa Tanzania na Waziri wa Afrika Mashariki wa Kenya, tukienda pamoja London kwenye ziara mtu akaniuliza tunawauzia nini Kenya, nitamwambia Kenya tunawauzia *transformer* na yeye akiulizwa mnawauzia nini Tanzania, atasema tunawauzia *sausage*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yule atakayekuwa anatuuliza ataona kwamba huyu Waziri Kamala ndiye anatoka kwenye nchi yenye uchumi wa kisasa kwa sababu huwezi ukauza *transformer* kama uchumi wako siyo wa kisasa. Ukweli ni huo na tutaendelea kufanya vizuri katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy ametoa hoja hapa pamoja na Mheshimiwa Msolwa na Mheshimiwa Ligallama kwamba ni vizuri tujiandae kielimu. Kwenye elimu tunaendelea kujiandaa. Wote mnafahamu Tanzania ni nchi pekee yenye Shule kila Kata, tunajua kwamba zina matatizo, tulikuwa na matatizo ya maabara, lakini wote mnafahamu tayari tumepata fedha za kujenga maabara za kisasa kwenye shule hizi kwa kushirikiana na *ADB.*

Wote mnafahamu kwamba shule hizi zilikuwa na matatizo ya vifaa, lakini nimemsikia Waziri wa Fedha ambavyo amesema sasa mkakati ni kutenga fedha nyingi zaidi kununua vifaa kwa ajili ya Maabara hizi. Lakini nyote mnafahamu kwamba Tanzania ndiyo nchi pekee yenye *Public Universities* nyingi kuliko nchi yoyote ile Afrika Mashariki. Hata Wabunge kutoka Uganda walipokuja kutembelea *University of* Dodoma,

walipofika pale wakaiangalia, Mbunge mmoja akanipigia simu nikamwuliza uko wapi? Akasema nipo kwenye Mji mmoja ambao upo karibu na Mji wa Dodoma. Nikasema wapi huko? Akasema tumekwenda kutembelea *University* lakini inaonekana huu ni Mji. Nikasema hapana, huo siyo Mji mwingine bali hicho ni Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi, cha ng'ambo ya mto ni kizuri kuliko kile ulichonacho. Kwa hiyo, mara nyingi kwa kuwa *University of Dodoma* iko karibu hatuwezi kuona maajabu haya. Ni vizuri Serikali tukaendelea kuwaleta Waganda wengi zaidi na wengine, waje waone mambo tunayoyafanya watusaidie kutoa ujumbe, ni kitu gani tunafanya katika elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Tanzania ndiyo nchi pekee yenye mfumo mzuri wa *Loan Board*, ambao unatoa mikopo kwa wanafunzi ambao wanasoma kwenye elimu ya juu kuliko nchi zote tulikozunguka, wengine wameanza lakini hawajaweza kufanya vizuri kama sisi. Tunazo changamoto, lakini ni lazima tuendelee kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea na kasi hii ya *University of Dodoma* kwa sababu miaka michache iliyopita wanafunzi wote Tanzania waliokuwa kwenye Vyuo Vikuu walikuwa hawazidi 36,000, lakini *University of Dodoma* peke yake itakuwa na wanafunzi 40,000. Tukifanya hivi tukawa na *University of Dodoma* nyingine na nyingine miaka michache ijayo tatizo litakalokuwa linazungumzwa hapa ni kwamba tuna wasomi wengi wamemaliza kwenye vyuo vikuu lakini hawana kazi.

Mheshimiwa Spika, siku zote maendeleo ni Baba wa matatizo. Ukileta jambo lolote la maendeleo, ujue vile vile unatengeneza tatizo lingine. Kabla ya hapo, tulikuwa tuna tatizo la watu wengi kumaliza kwenye Vyuo vya Ualimu na kukosa kazi, tukaja na sera ya kuhakikisha kwamba watoto wote wanaomaliza Shule ya Msingi wasome na kwa sababu hiyo tukajikuta tuna upungufu wa Walimu. Kwa hiyo, mafanikio ya watoto wote kwenda kwenye Shule ya Msingi yakatuletea tatizo la kuonekana kwamba sasa tuna upungufu wa Walimu.

Lakini vile vile tulipoamua kwamba watoto wengi wanamaliza darasa la saba wanafaulu lakini hawaendi Sekondari, tukaja na sera ya kujenga Sekondari kila Kata. Hilo tukafanikiwa kwa kuwa na Sekondari hizo, lakini kwa kuwa mafanikio ni Baba wa matatizo, hilo likatuletea tatizo la kuwa na upungufu wa Walimu na upungufu wa vifaa. Kwa hiyo, mara nyingi ukisikia mtu anazungumzia upungufu wa Walimu, upungufu wa vifaa, ujue kwamba anazungumzia maendeleo kwa sababu bila maendeleo haya huwezi ukaliona tatizo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siku zote ni lazima tuelewe mafanikio ni Baba wa matatizo, na ndiyo maana hata ukijenga barabara nzuri za lami ujue unatengeneza tatizo lingine la kuongeza ajali kwa magari kwenda kwa kasi. Kwa hiyo, ni lazima uweke matuta kwenye barabara hizo. Mafanikio ni Baba wa matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohamed Missanga na yeye ametoa hoja ambazo nakubaliana naye, lakini na Waheshimiwa wengine ambao wametoa hoja nyingi nimeambiwa kwamba sasa muda unakwisha, ningependa wote niwajibu. Mheshimiwa Pascal Nakei, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Kumchaya, Mheshimiwa Mdee, Mheshimiwa Oscar Mukasa, nawashukuru wote sana kwa hoja zenu mlizozitoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa moyo wa ukunjufu kabisa, nawaomba sana mridhie Itifaki hii kwa sababu mambo yote Tanzania ambayo tuliyahitaji yapo ndani ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na hususan kwa msemo wako kwamba Mafanikio ni Baba wa Matatizo. Lakini mimi nadhani ningependeza zaidi ungesema mafanikio ni Mama wa matatizo, kwa sababu Baba hazai kinachozaa matatizo ni Mama. Basi kila mtu ataichukua anavyopenda. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, lilopo mbele yetu hapa ni ombi au rai ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwamba Bunge hili liridhie Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, hoja ameitoa na imeungwa mkono.

*(Hoja iliamuliwa Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nathibitisha rasmi kwamba Bunge limepitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, ahsante sana tunaomba kazi iendelee sasa, katika mijadala, katika kukabiliana. Tunajua kazi hii ipo katika mikono salama kabisa kutokana na jinsi mlivyojipanga. Tunawashukuru sana.*(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010
***[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010]***

*(Kusomwa kwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hiyo *neck tie* uliyovaa na kitambaa mfukoni vinapendeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye kupitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2, wa mwaka 2010 *[The written laws (Miscellaneous Amendments Act No. 2), 2010]*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema pamoja na maisha. Napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na kupitia kwako kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wao kwangu tangu nilipoteuliwa kushika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ninawapongeza sana kwa kazi nzuri ya kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuishauri tangu Bunge hili la Kumi tangu Uhuru wetu lilipozinduliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema ni Bunge la Kumi ukiacha Bunge la kutunga Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya Mwaka 1962, Bunge la Kutunga Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano Mwaka 1965 na Bunge la Kutunga Katiba ya Jamhuri ya Muungano Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, ingawa sikuwa Mbunge tangu mwanzo, lakini niliyafuatilia majadiliano ndani ya Bunge hili na kusoma sheria zilizotungwa na Bunge lenyewe ambazo zilikuwa na mwelekeo wa uchumi na haki za kijamii. Nilipoteuliwa nilikuta hoja nzito na nyeti zikijadiliwa kwa umahiri mkubwa bila hofu wala hila. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi, ninapenda kuwatakia Waheshimiwa Wabunge wenye nia za kutetea nafasi zao, kila la kheri katika mchakato wa uteuzi na kampeni za uchaguzi. Kwa wale ambao hawana nia ya kutetea nafasi hizo, ninawatakia kila la kheri katika shughuli nyingine watakazokuwa wanazifanya baada ya kulitumikia Bunge na Majimbo yao na kwamba sasa watakuwa Mabalozi wa Bunge la Viwango na Kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Watanzania wengine wenye nia ya kugombea nafasi ya Ubunge, ninapenda kutumia nafasi hii, kuwakumbusha kwamba, kwa mara ya kwanza tangu tupate uhuru katika uchaguzi mkuu, Sheria ya Kusimamia Uchaguzi ndani ya Vyama vya Siasa kuhusiana na Matumizi ya Fedha katika Kampeni kabla na baada ya uteuzi wa wagombea, imetungwa. Masharti ya Sheria hii yasipozingatiwa, uteuzi wenu utaenguliwa kama itathibitika kwamba mmekiuka masharti hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo na kabla ya kuelezea maudhui ya Muswada huu, napenda kutambua mchango mkubwa wa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na ndugu George Masaju, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kazi nzuri wanazofanya ambazo zimeniwezesha kufanya kazi yangu kwa urahisi na ufanisi. *(Makofi)*

Aidha, kwa aina ya pekee, ninamshukuru sana ndugu Kasim Sumba Kihuki, Mwandishi Mkuu wa Sheria na Maafisa Waandishi wote wa Sheria, kwa kuandaa na kupitia Miswada yote ambayo ndiyo imetuwezesha kuwa na kazi za kutosha za Bunge hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana pia ndugu Elieza Mbuki Fereshi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Ndugu Maria Kejo, Mkurugenzi wa Madai na Sheria za Kimataifa, Ndugu Mathew Mwaimu, Mkurugenzi wa Katiba na Haki za Binadamu, Bibi Deodata Makani, Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala, Ndugu Haroub Gasi Kimasi, Mkurugenzi wa Mipango, kwa kazi zao nzuri za kuboresha utendaji kazi katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali wa ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana watumishi wasioonekana lakini ambao bila wao, kazi hizi zisingekuwa na ubora wa kiwango hiki. Hawa ni pamoja na Waendesha Ofisi, Watendaji na Maafisa Wakuu, Madereva na Wahudumu wa ofisi zetu. Nawashukuru sana na ninawasihi waendelee kuwatumikia wananchi kwa unyenyekevu na kwa kujishusha kama inavyotakiwa kwa watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada huu, ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na kupitia kwake Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa ushauri wao wakati wa kuupitia na kuujadili Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninautambua pia mchango mkubwa wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo, waliungana na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, katika kuupitia Muswada huu. Maoni na ushauri wao kwa kiasi kikubwa, umesaidia kuboresha sana Muswada huu. Hii inathibitishwa na marekebisho katika Muswada kama yanavyoonekana katika majedwali yaliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na.2 wa mwaka 2010, unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria mbalimbali 16 zilizotungwa na Bunge. Marekebisho yanayopendekezwa, yanalenga kuondoa upungufu ambao umedhihirika wakati wa utekelezaji wa masharti yaliyomo katika Sheria hizo. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-

- Sheria ya Benki *(The Bank of Tanzania Act)*, Sura ya 197;

- Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha *(The Banking and Financial Institutions Act)*, Sura ya 342;

· Sheria ya Mamlaka ya Masoko ya Hisa na Dhamana *(The Capital Markets and Securities Authority Act),* Sura ya 79;

· Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai *(The Criminal Procedure Act),* Sura ya 20;

· Sheria ya Mikopo ya Rasmali *(The Financial Leasing Act),* Sura ya 417;

· Sheria ya Biashara ya Usafirishaji Baharini *(The Merchant Shipping Act),* Sura 165;

· Sheria ya Magazeti *(The Newspapers Act)*, Sura ya 229;

· Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(The Penal Code Act),* Sura ya 16;

· Sheria ya Makosa ya Mwenendo wa Jinai *(The Civil Procedure Act),* Sura ya 20;

· Sheria ya Mashirika ya Umma *(The Public Cooperation Act),* Sura 257;

· Sheria ya Kuhamisha Mali za Benki ya Taifa ya Biashara *(The National Bank of Commerce Re-organization and Vesting Assets and Liabilities Act),* Sura ya 404;

· Sheria ya Mafao ya Uzeeni ya Watumishi wa Umma *(The Public Service Retirement Benefits Act),* Sura ya 371;

· Sheria ya Takwimu *(The Statistics Act),* Sura ya 352;

· Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(The Tanzania Revenue Authority Act),* Sura ya 148;

· Sheria ya Msajili wa Hazina *(The Treasury Registrar (Powers and Functions) Act,* Sura ya 370; na

· Sheria ya Udhibiti ya Gharama za Uchaguzi (*The Election Expenses Act),* Sheria Na.6 ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Benki Kuu, Sura 197, Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342, Sheria ya Udhibiti wa Masoko na Hisa, Sura ya 79, Sheria ya Mafao ya Uzeeni ya Watumishi wa Umma, Sura ya 371, Sheria ya Takwimu, Sura ya 351 na Sheria ya Mamlaka ya Mapato, Sura ya 396, Sheria hizi zinafanyiwa marekebisho yanayoshabihiana. Lengo la marekebisho hayo, ni kumuondoa Katibu Mkuu Hazina kwenye Wadhifa wa Ujumbe au Uenyekiti wa Bodi wa Mashirika au Taasisi Mbalimbali katika Sheria hizo anazosimamia yeye mwenyewe. Kwa marekebisho haya, Wizara ya Fedha, itawakilishwa katika Bodi hizo na Mwakilishi ambaye ni Afisa asiyekuwa Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Sheria ya Biashara ya Usafirishaji Baharini, Sura ya 165 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, marekebisho yake yanalenga kupanua uwigo wa matumizi ya Sheria hizo katika makosa yanayofanywa na maharamia katika Bahari Kuu (*High Seas)* inayopakana na ukanda wa bahari yetu. Marekebisho haya yanalenga pia kutoa mamlaka kwa Mahakama Kuu ya Tanzania ya kupokea mashtaka yanayohususiana na makosa ya jinai ya uhalifu wa kiharamia unaofanywa kwenye Bahari Kuu, bila kujali kama uharamia huo umefanywa au wamefanyiwa Watanzania na kwamba vifaa vilivyotumika katika uharamia huo vinamilikiwa na Watanzania au vimesajiliwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sheria zinatambua makosa ya kiharamia yanayotendwa baharini kama makosa hayo yametendwa ndani maji ya Tanzania yaani *Territorial Waters* au utendaji wa makosa hayo umeihusisha meli ya Tanzania au iliyosajiliwa Tanzania au kama katika meli husika walikuwemo Watanzania. Kwa kuwa Tanzania imeridhia Mikataba ya Kimataifa ya Kupambana na Uharamia wa Baharini, tunaona ni vyema Sheria zetu ziruhusu Mahakama zetu kushughulikia makosa hayo bila kujali uraia au utaifa wa mkosaji na vyombo vyake.

Mheshimiwa Spika, marekebisho katika Sheria ya Mikopo ya Rasilimali (*The Financial Leasing Act),* Sura ya 417, yanakusudia kuondoa mgongano wa mamlaka ya kutengeneza Kanuni uliopo baina ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha kwa upande mmoja na Sheria ya Mikopo ya Rasilimali *(The Leasing Financial Act),* Sura ya 417 kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mikopo ya Rasilimali, mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazohusiana na usimamiaji wa mikopo ya rasilimali (*The Financial Leasing),* yametolewa kwa Waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha. Kwa upande mwingine, Sheria za Benki na Taasisi za Fedha, inatoa mamlaka kama hayo kwa Gavana wa Benki Kuu. Marekebisho yanayofanyika, yanakusudia kuhamisha mamlaka ya kutunga kanuni chini ya Sheria ya Mikopo ya Rasilimali kutoka kwa Waziri ili mamlaka hayo yabaki kwa Gavana wa Benki Kuu ambaye atashauriana na Waziri kabla ya kutunga kanuni hizo. Marekebisho haya yanalenga katika kusimamia mienendo mema katika vyombo vya fedha (*good practices).*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Magazeti *(The News Papers Act)*, marekebisho yanayokusudiwa, yanalenga kuondoa ulazima wa kuwepo Washauri wa Mahakamani wakati wa kusikiliza mashauri ya kashfa magazetini yaani *defamation* na badala yake Washauri hao wawepo tu pale ambapo Mahakama itakapoona ni lazima ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wakati au pale upande wowote utakapoomba Washauri hao wawepo. Mapendekezo haya yanafuatia malalamiko na kilio cha muda mrefu kutoka kwa wadau kuwa ulazima wa kuwepo kwa Washauri hao, kumekuwa kukichangia kwa kiasi kikubwa katika ucheleweshaji wa kusikiliza mashauri hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mashirika ya Umma *(The Public Corporations Act)*, Sura ya 207, Sheria ya Kuhamisha Mali za Benki ya Taifa ya Biashara *(The National Bank of Commerce Re-organization and Vesting of Assets and*

*Liabilities Act),* Sura ya 404 na Sheria ya Msajili wa Hazina *(The Treasury Registrar Powers and Functions Act),* Sura ya 370, yanafanyika marekebisho yanayoshabihiana. Marekebisho yanakusudia Ofisi ya Msajili wa Hazina, kuwa chombo kinachojitegemea kisheria na kuiwezesha ofisi hiyo kusimamia ufanisi wa Mashirika ya Umma yaliyopo na kwa ujumla. *(Makofi)*

Aidha, inapendekezwa kuyahamisha majukumu yote ambayo awali yalikuwa chini ya *SCOPO* kwenda kwa Msajili wa Hazina. Sheria nyingine inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Gharama ya Uchaguzi (*The Election Expenses Act*), Sheria Na.6 ya 2010. Katika Sheria hii, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9(1) ili kupunguza siku za kuwasilisha taarifa kuhusu gharama ambazo mgombea anatarajia kutumia kutoka siku saba ili kuwa siku tano.

Aidha, katika jedwali la marekebisho, tunapendekeza kukifanyia marekebisho Kifungu cha 7(3) ili kukidhi mapendekezo mapya ambayo Waheshimiwa Wabunge, wametoa na Serikali imeyakubali kutoka na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo maneno nje ya Bunge, kwamba Kifungu hiki kiliingizwa kwenye Muswada huu kinyemela. Nimekwishatoa maelezo kwenye Kamati ya Uongozi chini yako Mheshimiwa Spika na pengine si jambo la tija kurudia yale niliyosema kwenye kikao hicho. Itoshe tu kusema kwamba katika kuzingatia majadiliano ndani ya Bunge na yale maagizo uliyoyatoa kwetu kutafuta maneno yanayotafsiri kile kilichotokea Bungeni kama inavyoonekana katika *Hansard* ya tarehe 11 Februari, 2010, kwa nia njema na kwa kuzingatia Taaluma ya Uandishi, tuliona kwamba kuidhinishwa kwa wajumbe wa timu ya kampeni ilikuwa ni jambo la kuzingatiwa. Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Uongozi na Ushauri wa Kamati mbili zilizoujadili mjadala huu, sasa dhana ya kuidhinishwa kwa timu ya kampeni iondolewe na itoshe tu kwa wagombea kuwasilisha orodha kama inavyoonekana katika Muswada. *(Makofi)*

Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 24(1) kwa kupunguza siku ambazo kila Chama cha Siasa kitatakiwa kukamilisha mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya Vyama kutoka siku 21 hadi siku tano. Lengo ni kuainisha dhana ya siku tano iliyoko katika Kifungu cha 9(1) na maudhui yaliyomo kwenye kifungu cha 24(1), marekebisho haya yanalenga kuainisha siku ambayo Tume ya Uchaguzi, imeiteua kama ndiyo siku ya uteuzi ambayo ilikuwa haijulikani wakati Sheria ilipokuwa inatungwa na kipindi cha kumaliza uhai wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninapenda kuzipongeza sana timu mbili zilizocheza jana na sana Yanga ambao walijitahidi sana lakini pia Simba waliofaulu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua mbili yaani Kusoma Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia marekebisho yote yanayopendekezwa na litakubali marekebisho hayo yawe sehemu ya Sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010*. Kama ilivyo kawaida ya Kanuni zetu, sasa nitamwita Mwenyekiti au Mwakilishi wake wa Kamati husika ambayo ni Katiba, Sheria na Utawala, ili tupate maoni ya Kamati, Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Lubeleje, kwa maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lubeleje, huna haja ya kusema lolote kuhusu aliyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhusu timu yako iliyoshindwa jana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - (MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, baada ya kukamilisha kazi ya kuuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010*, kwa Mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, tarehe 16 Aprili, 2010, Kamati ilikutana katika Ukumbi uliopo Ofisi ya Bunge Dodoma na kupata maelezo ya Serikali kuhusu Muswada huu. Katika Kikao hicho, Kamati iliwaalika Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ili kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa michango ya Waheshimiwa Wabunge walioshiriki katika Kikao cha Kamati, ilisaidia na kurahisisha kazi tuliyokuwa nayo. Nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo na Waheshimiwa Wabunge wengine waliotoa michango yao ya kina na kusaidia kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha pamoja cha Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alieleza maudhui, madhumuni na sababu ya Muswada huu. Katika maelezo yake, mtoa hoja alionyesha kuwa sababu kubwa ya kuleta mapendekezo hayo, ni nia ya Serikali ya kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa. Sababu nyingine iliyoelezwa ni kuimarisha misingi ya utekelezaji wa sera zilizopo. Kutokana na maelezo ya mtoa hoja, kwa ujumla Kamati iliafiki kuwa sababu zilizotolewa ni za msingi.

Mheshimiwa Spika, mbali ya maelezo hayo, mtoa hoja pia alitaja Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa katika Muswada huu. Alizitaja Sheria hizo 17 zikiwemo Sheria za Gharama ya Uchaguzi ya Mwaka 2010 *(The Election Expenses Act, 2010)* na Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta, Na.3 ya Mwaka 2010 *(The Electronic and Postal Communication Act, No. 3 of 2010).*

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja aliieleza Kamati shabaha ya kupendekeza marekebisho hayo. Kwa mfano, maelezo ya Serikali yalionyesha kuwa marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Na.6 ya Mwaka 2010 *(The Election Expenses Act No. 6 of 2010)*, yanakusudia kupunguza siku za kuwasilisha gharama anazotarajia kutumia mgombea kutoka siku saba hadi tano. Aidha, mapendekezo haya yanahusu pia kuondoa ulazima wa mgombea kupata ridhaa ya Msajili, Mkurugenzi au Afisa Mtendaji wa Kata kabla ya matumizi. Maelezo yote haya yaliafikiwa na Kamati kwa kuwa Bunge likipitisha marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii, mazingira ya utekelezi wa Sheria hiyo yataboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Muswada huu, wajumbe na Waheshimiwa Wabunge wengine walipata fursa ya kuhoji na kutaka ufafanuzi wa kina pale walipoona inafaa. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote waliohudhiria kikao hicho, waliruhusiwa kuibua hoja mbalimbali katika kufanya uchambuzi. Upande wa Serikali nao ulipata fursa ya kutoa ufafanuzi ambapo mifano mbalimbali ilitolewa. Jambo moja la kuvutia lililojitokeza ni rejea ya uzoefu na kesi mbalimbali ili kufafanua au kujibu hoja. Vile vile, Waheshimiwa Wabunge na upande wa Serikali, mara kwa mara walirejea Sheria za nchi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Ibara ya 4, Ibara ya 114 na Ibara ya 115 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilirejewa pale lilipojitokeza suala la mamlaka za Mahakama. Mjadala huu uliibuka tulipojadili Ibara ya 18 ya Muswada, ambapo Serikali inapendekeza Marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, *(The Penal Code Act, Cap. 16).*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria yanayolenga kuondoa upungufu uliopo katika utekelezaji wa Sheria na Sera, ni jambo la kuungwa mkono. Suala muhimu la kuzingatiwa ni namna marekebisho hayo yanavyoweza kuondoa upungufu unaolengwa bila ya kuathiri misingi ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maelezo hayo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu Marekebisho ya Sheria mbalimbali kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja, pamoja na maoni yaliyotolewa wakati wa Kikao cha Kamati.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya Muswada huu, naomba kueleza kuwa baada ya majadiliano ya kina wakati wa kuuchambua Muswada huu, Serikali iliondoa mapendekezo yake kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Elektroniki na Posta, Na.3 ya Mwaka 2010 *(The Electronic and Postal Communication Act, 2010).* Uamuzi huu ulikuwa ni uamuzi wa busara uliozingatia mwenendo wa majadiliano ulivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Ibara ya 12 inayohusu mapendekezo ya kurekebisha Kifungu cha 22 kwa kufuta maneno ”*Minister may*” na kuweka maneno ”*Governor of the Bank of Tanzania may after consultation with the Minister*”. Katika Ibara hii, Kamati iliafiki mapendekezo hayo kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja. Hata hivyo, Kamati yangu ina maoni kuwa usimamizi wa Bunge na vyombo vingine katika eneo hili la mamlaka na majukumu ya Gavana wa Benki Kuu ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 16 ya Muswada, inayohusu mapendekezo ya kurekebisha Kifungu cha 57 cha Sheria ya Biashara ya Usafirishaji Baharini, Sura ya 165 (*The Merchant Shipping Act, CAP.165*), Ibara Ndogo ya 3, inayoanza kwa neno ”*lin*” ambalo halina maana yoyote katika mapendekezo. Kamati ilishauri kuwa neno hilo ”*lin*” libadilishwe na kusomeka ”*in*”. Kwa marekebisho hayo, Ibara ya 16 (3) ya Muswada inaanza kwa maneno ”*in deciding*” badala ya ”*lin deciding*”.

Mheshimiwa Spika, tulipochambua Ibara ya 25, suala la uandishi wa Sheria na matumizi ya vifungu vya maneno yanayotumika lilizingatiwa. Ibara hii, inahusu Marekebisho ya Kifungu cha 52 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Watumishi wa Umma (*The Public Service Retirement Benefits Act, CAP. 371*.) Ili Ibara hii iwe na maana nzuri inayozingatia namna bora ya uendeshaji wa mambo ya utawala, Kamati ilishauri kuwa maneno “*upon consultation with the Minister*” katika aya “*a*” inayopendekezwa, yaondolewe na kuacha mamlaka ya Rais kuteua Mwenyekiti yasifungwe na sharti hilo. Nafurahi kusema kuwa ushauri huo ulizingatiwa na Serikali.

Kamati pia iliangalia mtiririko na kubaini makosa ya kiuchapaji. Kama ilivyo ada, Kamati ilishauri kurekebishwa kwa makosa hayo na Serikali ilikubali. Eneo mojawapo ni Ibara ya 34 ya Muswada inayohusu mapendekezo ya kuongeza katika Sheria ya Msajili wa Hazina, Kifungu kinachofafanua uteuzi wa Msajili huyo. Katika mapendekezo ya Serikali, Kifungu cha 3(4) kinarejea Kifungu kidogo cha 3. Hata hivyo, katika Muswada tunaoujadili, mapendekezo yanaonyesha kuwa Kifungu hicho kinarejea Kifungu kidogo cha 4. Kamati iliona kuwa, haya yalikuwa ni makosa ya uchapaji na ilishauri marekebisho. Mtoa hoja aliafiki ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, mbali na matumizi ya maneno na uchapaji, Kamati pia ilizingatia umuhimu wa misingi ya utawala bora na kujenga imani ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa msingi huu, tulipofika Ibara ya 36 inayohusu marekebisho ya Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Msajili wa Hazina, tulishauri Serikali ibadilishe maneno yaliyotumika. Madhumuni ya ushauri huu ni kuboresha marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa sura nzuri ya Sheria na kujenga imani kuhusu maslahi ya umma *(public interest),* Kamati ilishauri kuwa Kifungu cha maneno kilichotumika katika mapendekezo ya Ibara ya 36, kiandikwe upya kwa namna ya kumsaidia Rais katika utekelezaji wa madaraka hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hayo ndiyo maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2010 *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010*. Kama yapo maeneo mengine ambayo sikuyagusia, wajumbe na Waheshimiwa Wabunge wengine watachangia.

Kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2010 *(The written Laws (Miscellaneous Amendments), Bill, 2010).* Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalamu wake, kwa ushirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa George Simbachawene, kwa ushirikiano wao kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wakati wa kuchangia na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru sana na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango yao ya kina wakati wa kuuchambua Muswada huu. Naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Katiba,Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti na Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati hii Ndugu Elihaika Mtui na Ndugu Athuman Hussein, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashillilah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kamati na sasa utafuatiwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fatma Maghimbi.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani za Kambi ya Upinzani, kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuleta marekebisho haya kwa sheria zote ambazo kwa kweli yanaleta umakini na kuongeza ufanisi kiutendaji kwa vyombo husika na sheria hizo. Pongezi hizo ni kwa watendaji wote walioko chini ya ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpa pongezi nyingi Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, kwa umakini wake wa kuendesha Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, ni shukrani kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao wanaonipa katika kutimiza wajibu wangu kama Msemaji Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria zinazofanyiwa marekebisho ni nyingi, hivyo basi, tutazipitia tu ambazo tunaona marekebisho yake yanagusa jamii pamoja na kuimarisha dhana nzima ya utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada huu, inafanya marekebisho katika Sheria ya Benki Kuu. Kwa ujumla, Kambi ya Upinzani, inaona dhana nzima ya kumwondoa Katibu Mkuu kwenye Bodi ya Benki Kuu, ni nzuri, kwani inampa yeye nafasi ya kuweza kusimamia vyema yale yanayoamuliwa au kurekebishwa pia kushauri yale ambayo yana kasoro. Hii inaondoa dhana nzima ya "*conflict of interests*" katika uendeshaji na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Katibu Mkuu wa Hazina anakuwa na majukumu ya usimamizi katika masuala yote ambayo yanahusiana na fedha pamoja na asasi zake na masuala ambayo yalikuwa yanamhusisha katika vyombo vingine vya utungaji wa miongozo kwa asasi ambazo zinatakiwa kuwajibika kwa kiongozi huyo, ni jambo lililokuwa linasababisha udhaifu kiusimamizi. Hivyo, sisi Kambi ya Upinzani, tunampongeza Mwanasheria Mkuu, kwa kuanza sasa kutekeleza ushauri wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na ushauri wa Kambi ya Upinzani, kuwa wale wanaotakiwa kusimamia na kuhoji, wasiwe ni sehemu ya Bodi ambazo zinatakiwa kutoa taarifa kwao.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa marekebisho haya hayataishia hapa, kwani *CAG* amekwisha kupendekeza kuwa Waheshimiwa Wabunge wasiwe sehemu ya Bodi ya Mashirika au Taasisi, hivyo ni imani ya Kambi ya Upinzani, kuwa mapendekezo hayo ya *CAG* pia yatafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili kuleta ufanisi katika utendaji wa Bodi hizo, ikiwa ni pamoja na kuondoa mgongano wa maslahi yaani "*conflict of interest*".

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada, inaweka marekebisho katika Sheria ya Biashara ya Usafirishaji Baharini, kwa kuweka kifungu cha adhabu kwa kosa la uharamia. Dhana ya kubadilisha Sheria hiyo inaenda sambamba na sehemu ya tisa ya Muswada yenye mabadiliko ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, katika Kifungu cha 18 kinachorekebisha Kifungu cha 6 cha Sheria. Kambi ya Upinzani, inaona kuwa, kuongezwa kwa vifungu hivyo, itakuwa ni fundisho zuri kwa wale wote ambao wanafikiria kutenda kosa hilo la uharamia kwa meli na ndege kwa lengo la kudai fedha kwa ajili ya kukomboa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya nane ya Muswada, Kifungu cha 16 kinachofanyia marekebisho Kifungu cha 57 cha Sheria ya Magazeti, Sura ya 229. Kambi ya Upinzani, inaona japokuwa dhana ya kufanya marekebisho ni nzuri, lengo lake linaweza kuwa ni kuhatarisha uhuru wa vyombo vya habari na hivyo kuwanyima Watanzania haki zao za msingi kutoa na kupata habari. Tunasema hivyo kutokana na mwenendo mzima ulivyo pale zinapoandikwa habari za baadhi ya watu na wao kukimbilia Mahakamani na kudai mabilioni ya fedha kama fidia, wakati habari ile ni wao wenyewe ndio wamesababisha iandikwe kwenye magazeti (wao au washirika wao ndio *source ya* habari yenyewe).

Mheshimiwa Spika, Serikali inadai kuwa ma-*assessors* wanachelewesha kesi zinazofunguliwa kutokana na kudhalilishwa na magazeti. Mahakama Kuu wala Mahakama ya Rufaa hazina ma-*assessors* lakini Watanzania wengi wanalalamikia ucheleweshaji kwa kesi zao. Serikali mara zote inasema kuwa itajitahidi kurekebisha. Kambi ya Upinzani inauliza ni jambo gani linaloishinda Serikali kurekebisha pale ma-*assessors* wanapokuwa ndio chanzo cha ucheleweshaji wa kesi?

Mheshimiwa Spika, kuondoa ma-*assessors* ni kuvibana vyombo vya habari na kutaka kuvinyima vyombo hivyo kuwa na mtetezi kutoka miongoni mwao, maana ni wazi miongoni mwa ma-*assessors,* atakuwa mtu mwenye taaluma au anayetoka katika taasisi ya habari. Hivyo basi, uwepo wa ma-*assessors* katika mashauri hayo ni muhimu sana katika mchakato mzima wa utoaji wa maamuzi/hukumu ambazo pande zote mbili zitaridhika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mategemeo ya Kambi ya Upinzani na Watanzania kwa ujumla yalikuwa ni kuletewa Marekebisho ya Sheria yenyewe ya Habari na Haki ya Kupata Habari na siyo badiliko dogo kama hili ambalo tusipokuwa waangalifu litakuwa linalinda zaidi uovu kuliko kulinda mali na rasilimali za jamii. Serikali ina jukumu la kuhakikisha inatunga sheria kulinda maslahi ya Taifa zaidi jambo ambalo halionyeshwi na dhamira ya marekebisho ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na tano ya Muswada huu, kuanzia Kifungu cha 31 hadi 38, vinaifanyia marekebisho Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, kwa kuifanya Ofisi ya Msajili kuwa na mamlaka kamili, kwanza kwa uanzishwaji wake na jinsi Msajili atakavyopatikana pamoja na kuajiri watumishi wake. Kwa ujumla, Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni jambo zuri na kutokana na ukweli kwamba tumekuwa tukikosa kile tulichokuwa tukitegemea kupata kutokana na zoezi zima la ubinafsishaji wa

mashirika yetu na pia hata yale ambayo hayakubinafsishwa yamekuwa yakitoa kazi bila ya kuwa na mtu wa kuangalia mchakato mzima wa mapato na matumizi hasa yale yanahusiana na utawala (marupurupu kwa wajumbe wa bodi na menejimenti za mashirika/makampuni ambayo kwa njia moja au nyingine hayawekwi bayana), aidha, pale ambapo Serikali inamiliki hisa chache kiasi kwamba inakosa hata sauti ya kuwa na chombo cha kuangalia maslahi yake kwenye hisa hizo chache, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa uanzishwaji wa Ofisi hii na kuipa mamlaka sasa tunatarajia upungufu uliokuwepo hapo awali yatarekebishwa na nchi itapata angalau kile kilichotarajiwa na wananchi. Sambamba na hilo, tunamshauri Rais pale anapokuwa anateua Msajili wa Hazina, ni lazima mtu huyo afanyiwe "*vetting*" kali na kuhakikisha mtu huyo hana sura ya ufisadi.

Mheshimiwa Spika, hatimaye, Kambi ya Upinzani imefurahi na hatua ya Serikali ya kurekebisha Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi, kwa kuondoa maneno "*approving authority*", yaani mamlaka ya kuthibitisha Timu ya Kampeni, ambayo hayakuwa yamejadiliwa na Bunge wakati wa Mjadala wa Bunge kama inavyoonyesha *Hansard* ya tarehe 11 Februari, 2010. Kambi ya Upinzani inadhani, kwa kuwa kazi ya kutunga Sheria ni kazi ya Bunge, si vyema kuiachia Serikali, hatimaye kuingiza tafsiri yao tofauti na maamuzi ya Bunge. Hali hii ikiachiwa hivi, inaweza kuhatarisha kabisa mamlaka ya Bunge ya kutunga Sheria na badala yake, kazi yake ikafanywa na Watendaji. Huko nyuma kulikuwa na haja ya kufanya tafsiri ya aina hiyo, kutokana na teknolojia ya wakati ule, lakini kwa teknolojia ya sasa, hakuna sababu kwani maamuzi ya nini kiingie katika Sheria yanafanywa ndani ya ukumbi wakati wa Bunge Zima likikaa kama Kamati na kusiwe na badiliko la aina yoyote, isipokuwa ya uhariri baada ya Bunge kufanya maamuzi yake. Hiyo ndiyo dhana halisi ya Bunge kuwa ni Chombo cha kutunga Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye sekta ya Katiba, Sheria na Utawala. Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia, hautuwezeshi kuanza kuwasikiliza wachangiaji kwa hiyo, nitayasoma tu matangazo machache.

La kwanza, ni kwamba baada ya Muswada huu, ile Miswada miwili ya sekta ya mifugo ndio itafuatia, natamka hivyo ili mjiandae kwa *Order Paper* ya kesho kwa sababu inawezekana tukimaliza saa sita hivi basi nitamwita Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ili tuendelee na hatua aliyofikia yeye na Kamati halafu twende mbele.

Cha pili, Mheshimiwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amewasilisha taarifa ipo katika *volume* tano hizi, kwa hiyo, nakuombeni, bahati mbaya wengi kidogo hawapo lakini usipoweza kupunguza makaratasi, majarida na nakala mbalimbali za nyaraka zilizomo katika kisanduku chako basi itakuwa vigumu sana kwa wahudumu kuweka hizi randama za Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Sasa, nawaombeni mnaotoka hivi sasa basi tuweze kupunguza yaliyomo mle ili hizi nyaraka

muhimu sana, taarifa ya ukaguzi kuishia tarehe 30 Juni, 2009 ziweze kuwekwa katika kisanduku kwa ajili ya rejea.

Mwisho, nilimtuma Mheshimiwa Naibu Spika kwenda kumpokea mgeni mashuhuri ambaye amepokelewa asubuhi, mgeni huyo, kwa lugha yao wao wanamwita Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wananchi la Kitaifa. Sasa Baraza la Wananchi, ndio Bunge kule China na *Vice Chairperson*, maana yake, huyu ndiyo Naibu Spika wa Taifa la Uchina. Ni mtu mzito, tumemuandalia Itifaki zote na Serikali imefanya mambo mengi tu pamoja na kumpitisha kwa *motorcade* na taarifa nilizonazo ni kwamba amekwishawasilisi. Kwa hiyo, wale wote walioalikwa kwa chakula cha jioni ambacho Mheshimiwa Spika amemuandalia mgeni wetu huyu Naibu Spika wa China, tafadhali tuwe pale saa mbili kamili mara tukitoka hapa, ili tuweze kukaa naye. Ana ujumbe wa jumla ya watu ishirini na moja.

Kesho asubuhi, nitapata fursa ya kumtambulisha hapa akiwa katika *Speakers Gallery* na ujumbe wake, atakaa nasi kwa dakika chache kwa sababu tumemwandalia ratiba ya kuona mambo mengine. Kwa hiyo, nitakatiza kidogo wakati wa kipindi cha maswali ili tuweze kumtambua. Baada ya utambulisho, tumpe heshima anayostahili kwa kumpigia makofi kwa sababu ni Taifa rafiki na ni mtu mzito. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, sasa shughuli za leo zimeishia hapo na sasa naahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 20 Aprili, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*